

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Nane – Tarehe 19 Aprili, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali. Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 63

**Ujenzi wa Barabara ya Kakonko – Muhange**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Mji wa Kakonko hadi Muhange?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kakonko kupitia Vijiji vya Kinonko, Ruhuru, Nyakiyobe, Gwarama, Kabane hadi Muhange inasimamiwa na mamlaka mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara kutoka Kakonko – Kinonko – Ruhuru – Nyakiyobe – Gwarama yenye urefu wa kilometa 26 inasimamiwa na *TANROADS* na kipande cha barabara kutoka Gwarama – Muhange yenye urefu wa kilomita nane inasimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara inayosimamiwa na *TARURA* yenye urefu wa kilomita nane ipo katika hali nzuri kufuatia matengenezo yaliyofanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa gharama ya shilingi milioni 40.88.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, kipande cha barabara hii yenye urefu wa kilomita tano, kiasi cha shilingi milioni 10 imetengwa kwa ajili ya matengenezo ili kuhakikisha huduma za kiuchumi na kijamii zinaendelea kufanyika kwa wananchi kwa kipindi chote cha mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuboresha miundombinu ya barabara za Jimbo la Buyungu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

ya nyongeza. Lengo la barabara hii ni kufungua mawasiliano kati ya Burundi na Tanzania. Kufuatia hili, katika kikao cha ushauri cha Bodi ya Barabara iliamuliwa barabara hii ihamishwe, kipande hiki cha Gwarama – Muhange, kitoke *TARURA* kwenda *TANROADS*. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na suala hili?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa barabara hii ni muhimu, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufuatana nami, aweze kuiona hii barabara? Nina hakika akishaiona atakuwa tayari kuchukua hatua za muhimu kujenga barabara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Kigoma imeipendekeza kupandishwa hadhi; na kwa kuwa Serikali tunafanya kazi kwa pamoja, basi jambo hili tumelipokea na ninaamini wenzetu wa *TANROADS* na wenyewe wanalo. Kwa hiyo, endapo hii barabara itakuwa inakidhi vigezo vyote, basi Serikali italifanyia kazi na itekeleze kama ambavyo Bodi ya Barabara ya Mkoa imependekeza.

Mheshimiwa Spika, suala la mimi kuongozana naye, nipo tayari mara baada ya Bunge lako Tukufu tutakapomaliza. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Barabara ya kutoka Irula katika Jimbo la Kilolo kwenda Image mpaka Kata ya Ibumu ni barabara mbaya sana, haijawahi kuchimbwa hata siku moja: Ni lini

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Serikali itajenga barabara hiyo kwa kiwango hata cha changarawe tu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Grace Tendega, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Tendega ameanisha hii barabara ya kutoka Irula mpaka Ibumu kwamba ni barabara ambayo haijajengwa, basi tutakwenda kufuatilia ili tuone kama imeanishwa kwenye bajeti ili tuweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Napenda kujua ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara inayounganisha Wilaya ya Shinyanga Mjini na Shinganya Vijijini kutoka *Old Shinyanga* kwenda Solo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Dkt. Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba kila kitu kipo katika mipango na Serikali tumeainisha maeneo yote yenye vipaumbele. Kwa hiyo, kadri tutakavyoyafikia, maana yake

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

yote yataainishwa. Umuhimu wa hii barabara unafahamika na ndiyo maana mara zote tumekuwa tukifanyia matengenezo. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii na yenyewe itafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya kutoka Chala kwenda Mpalamao imekuwa ni ahadi ya viongozi wengi na iliwekwa kwenye ilani lakini mpaka sasa hatuoni kinachoondolea. Ni lini mtatekeleza ahadi hiyo ya barabara ya Chala - Mpalamao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya kutoka Chala mpaka Mpalamao ni kweli tumekuwa tukiizungumza mara kwa mara, na nimemwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo katika vipaumbele ambavyo tumeviweka. Kwa hiyo, tunatafuta fedha ili ianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kuwa Kata ya Kidatu kuelekea Kata Msola Stesheni katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara, barabara haipitiki kwa sasa:-

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kutengeneza barabara ile angalau kwa kiwango cha changarawe ili iweze kupitika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoanisha Mheshimiwa Mbunge ipo katika mipango ya Serikali ya kuhakikisha kwamba inajengwa. Kwa hiyo, tsubiri tu muda utakapofika na barabara hiyo itafanyiwa kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Barabara ya Tabora - Mwambali imeshafanyiwa usanifu tangu mwaka 2020, lakini mpaka leo haijaanza kujengwa. Ni lini barabara hii itaanza kujengwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu baadhi ya maswali, barabara zote ambazo tayari zimefanyiwa usanifu na ambazo zipo katika mpango wa Serikali ni kwamba sasa hivi kitu kimoja ambacho tunakitafuta ni fedha ili tuanze kuzitekeleza. Kwa hiyo, ninaamini kwamba mara fedha itakapopatikana, basi na hii barabara itaanza kujengwa. Ahsante sana.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamisi Taletale swali la nyongeza.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali barabara yetu Bigwa na barabara yetu Ngerengere, Matuli, Matulazi:-

Je, lini Serikali itatuangalia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi Taletale, Mbunge wa Morogoro Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ngerengere kwenda Matulazi ni moja ya barabara muhimu na ya kipaumbele. Moja ya kazi kubwa ambayo tunaifanya sasa hivi, ni kufanya usanifu ili sasa tuiweke katika mipango yetu ya kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya Kisesa, Bujola kwenye Makumbusho ya Machief wa Kisukuma imebaki kilometa 1.3.

Je, ni lini itakamilishwa na Serikali kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya ambayo ameianisha ni kwamba mpaka sasa Serikali imeshafanya kazi sehemu kubwa. Kwa hiyo, sehemu ndogo ya kilomita 1.3 iliyobakia na yenyewe ipo katika mpango ili iweze kukamilika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mohamed Lujoo Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilitaka kujua kuna barabara yetu ya Chemba - Soya ambayo kwa muda mrefu imekuwa na shida kubwa na mara kadhaa viongozi walipokuja waliahidi kujenga walau kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua *commitment* ya Serikali katika hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Monni, Mbunge wa Chemba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi zote ambazo viongozi wamezianisha zipo katika mpango. Kwa hiyo, hata hii ambayo barabara ameianisha Mheshimiwa Mbunge ya kutoka Chemba mpaka Soya ni miongoni mwa barabara zetu, zipo katika mipango yetu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako.

Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake, sasa aulize swali lake.



Na. 64

**Mgawanyo wa Mapato Yatokanayo na Tozo za Miamala**

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN** aliuliza:-

Je, mgawanyo wa mapato ya tozo za miamala upoje kwa pande za Muungano na vipi yataboresha huduma kwa upande wa Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Hamad Chande, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhan Seleiman Ramadhan, Mbunge wa Chake Chake, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha tozo ya miamala ya kutuma na kutoa fedha kwa njia ya simu kwa lengo la kugharamia miradi mbalimbali inayotekelezwa na Serikali, ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya na madarasa. Utaratibu wa mgawanyo wa fedha za tozo ya miamala kwa pande zote mbili za Muungano unasimamiwa na Kanuni ya saba ya Kanuni ya Tozo za Miamala ambapo fedha zinatoka na miamala inayofanyika Zanzibar huwasilishwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Februari, 2022 jumla ya shilingi bilioni 231.54 zilikusanywa kwa Tanzania Bara na shilingi bilioni 2.96 kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa upande wa fedha zilizokusanywa Zanzibar, mchanganuo wa matumizi yake utatolewa ufafanuzi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, kwa Tanzania Bara, fedha hizo zimeelekezwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Halmashauri ikiwemo ujenzi wa vituo vya afya na madarasa katika tarafa ambazo hazikuwa na miundombinu hiyo. Ahsante sana.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nichukue fursa hii kuzipongeza Serikali zote mbili ya Mapinduzi ya Zanzibar; na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayofanya. Kutokana na majibu ya Serikali sitakuwa na swali la nyongeza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu mazuri. Tunaenda Wizara ya Afya. Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Abukari Asenga. Sasa ndiyo unaruhusiwa kuzungumza baada ya kuitwa.

Na. 65

**Makazi bora kwa wahudumu wa Afya**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENKA K.n.y. MHE. NORAH W. MZERU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea wahudumu wa kada mbalimbali za afya nyumba bora ili kuboresha makazi yao?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Daktari Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Norah Waziri Mzeru, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali imejenga nyumba 176 na katika mwaka wa fedha 2022/2023 itajenga nyumba 300 za kukaa familia tatu kwa kila nyumba. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Asenga kwa ajili ya swali la nyongeza, nawapongeza sana Wizara ya Afya kwa majibu ya moja kwa moja kwenye swali lililoulizwa. Mheshimiwa, hili jibu lina mistari miwili, wamemaliza kile kilichoulizwa.

Mheshimiwa Abubakar Asenga, swali la nyongeza.  
(*Makofi*)

**MHE. ABUBAKARI D. ASENKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa majibu haya, dah, hadi maswali ya nyongeza yanakuwa na utata. Kwa ruksa yako nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wakati Serikali inaendelea na mchakato wa kuboresha huduma za afya nchini; katika Jimbo la Kilombero chini ya Kanisa Katoliki imejengwa Hospitali kubwa sana ya Kansa. Hospitali hiyo mpaka leo haijafunguliwa. Baba Askofu anaomba Viongozi Wakuu wa nchi yetu wakafungue Hospitali hiyo. Mheshimiwa Waziri ana majibu gani?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. *St. Francis Hospital* ni hospitali ya kanda, inatibu zaidi ya mikoa 10. Gharama zimekuwa kubwa na wananchi wanalalamikia kwa sababu Serikali imeondoa ruzuku iliyokuwa inatoa zamani:-

Je, Waziri anaweza kusema chochote kwamba wanaweza kukaa na Uongozi wa *St. Francis Hospital* ya Ifakara ili kuzungumza namna ya kurejesha ruzuku ya awali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakuita ujibu kwa sababu yeye ndiye ameuliza kwa niaba, lakini maswali yake yote mawili ni maswali ya msingi, kwa sababu hayahusiani na swali la msingi lililoulizwa hapa, lakini kwa sababu yeye ndio muuliza swali, majibu kwa hayo maswali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza amezungumzia hospitali ambayo imefunguliwa, mimi na yeye tutakwenda Kilombero kuiangalia hospitali hiyo na kukagua halafu tuje tushauri mamlaka husika ili taratibu anazosisema ziweze kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, pili, suala la ile ruzuku ambayo alikuwa anaipata, nafikiri hata juzi tulikuwa tunazungumza hapa na Mheshimiwa Jenista Mhagama kuhusu hata masuala ya watumishi na mambo mengi. Nalo hili tunaenda kulifikiria kwenye bajeti hii na wakati wa bajeti tutawajibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Albert Mwantona swali la nyongeza.

**MHE. ANTHONY A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Serikali ilianzisha ujenzi wa hosteli kwenye Chuo cha Uuguzi pale Tukuyu mwaka 2008. Ujenzi umekamilika, umefikia hatua ya kufanya *finishing* tu yaani kuweka madirisha na milango, wanafunzi 150 wanakaa nje ya chuo. Je, ni mpango gani wa Serikali kuhakikisha kwamba majengo yale yanakamilika na wanafunzi wale 150 wanaingia kukaa chuoni? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwantona kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo amesema Mheshimiwa Mbunge labda nimwambie tu kwa mwaka huu kwa ajili ya umaliziaji vyuo kama hivi ambavyo vimekaribia kufanyiwa *finishing* ili watoto waingie ndani, zimetengwa *around* bilioni 2.7 kumalizia vyuo ambavyo viko 17

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

vinavyotakiwa kumaliziwa nchi nzima. Kwa hiyo kitamaliziwa kabla ya mwezi wa 12 kila kitu kitakuwa kimekaa vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Jimbo la Lushoto wananchi pamoja na Serikali yao wamejenga vituo vya afya pamoja na zahanati, lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana za nyumba za watumishi. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga nyumba za watumishi katika Wilaya ya Lushoto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shekilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo swali la msingi lilieleza kwamba kwa mwaka huu wa fedha zinaenda kujengwa nyumba 300. Naomba tukae na Mheshimiwa Mbunge tuangalie katika hizi 300 kama Lushoto eneo analolizungumzia limeguswa kama halijaguswa, tuone mapema tunaweza tukafanya nini ili hilo litekelezeke.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Nyanghwale sasa hivi kuna mfumuko mkubwa sana wa vijana kuendesha vyombo vya moto na wamekuwa wakipata ajali mbalimbali. Hospitali yetu ya Wilaya ya Nyanghwale haina *x-ray*. Je, Serikali ina mpango gani wa kutunulia *x-ray*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Amar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja kwa sababu anazungumzia ajali kwanza yeye kama Mbunge na sisi kama Wabunge na wadau wengine kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Usafirishaji moja ni kwanza tuone tufanye nini kuhakikisha kwamba ajali zinaenda kupungua ambazo sio za lazima.

Mheshimiwa Spika, pili, hilo la kwamba ipatikane *x-ray* halina *excuse*, ni kwamba mimi na Mheshimiwa Mbunge tuje tukae ili ioekane ni namna gani hospitali hiyo inapata *x-ray* yake mara moja. Hilo halina *excuse*, hakuna cha kusema kesho wala nini na Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan ameshapeleka kama nilivyoeleza hapa hizo bilioni 333.8 na bado hazijatumika. Kwa hiyo ni wakati muafaka wa sisi kufanya hiyo kazi na ku-*plan* kwa ajili ya kupatikana hicho anachosema Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaelekea Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Ujenzi wa Kiwango cha Lami wa Barabara ya Dar es Salaam-Morogoro-Bagamoyo kuelekea Mzenga-Mlandizi**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya mzunguko katika makutano ya Barabara ya Dar es Salaam, Morogoro na Bagamoyo kuelekea Mlandizi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Constantino Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Makofia, Mlandisi hadi Mzenga kilomita 35, makutano ya barabara ya Dar es Salaam -Morogoro na Makofia- Mlandizi-Mzenga eneo la Mlandizi limesanifiwa kwa ajili ya kujenga barabara ya mzunguko yaani *round about*. Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza ujenzi wa barabara ya Makofia – Mlandisi hadi Mzenga utakaohusisha na ujenzi wa *round about* katika eneo la Mlandizi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Mwakamo swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa jibu la Serikali la mara zote ni kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utengenezaji wa barabara hizo zilizotajwa lakini kwa kuwa pale ni eneo muhimu na kuna ajali nyingi zinatokea. Je, Serikali haioni kwamba tunaweza kutanua maeneo yale kama ambavyo imetanuliwa barabara ya pale Picha ya Ndege, Kongowe na Chalinze ili kuweza kupunguza msongamano wa eneo lile la Mlandizi?

Mheshimiwa spika, swali la pili, kama tatizo ni fedha na barabara hii inayozunguzwa, amezungumza barabara ndefu na mimi shida yangu ni pale Mlandizi, hatuwezi kuweka taa za haraka barabarani za kuongozea magari ili kupunguza misongamano iliyopo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Kibaha na sote ni mashahidi ambao wengi tunapita kwenye barabara hii. Kutokana na hoja ya Mheshimiwa Mbunge na jinsi ambavyo amekuwa akifuatilia ni kweli tulichosema ndio mpango wetu wa Wizara, lakini Wizara baada ya kufuatilia tunajaribu kuangalia uwezekano, tutafanya *study* tuwe na mpango wa muda mfupi ili kupunguza ajali, lakini pia na msongamano.

Kwa hiyo tutaangalia kama njia sahihi na rahisi itakuwa ni kupanua barabara kwa maana ya njia nne kama sehemu nyingine ama kuweka taa ili kwanza kuokoa ajali, lakini pia kupunguza msongamano ambao sasa umekuwa ni adha kubwa kwenye hiyo barabara. Msongamano huo pia upo hasa katika hizi njia ndogo zinazotoka Bagamoyo kwenda Mzenga ambapo wananchi wengi sana wanachelewa kukatisha ile barabara na kuona magari makubwa tu ndio yanayopita kwa muda mrefu. Kwa hiyo, tumelichukua na Wizara tunachukua kwa umuhimu mkubwa ili kuokoa ajali na pia kupunguza msongamano. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Komanya, swali la nyongeza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itanza kujenga kilomita 25 kwa kiwango cha lami katika maingilio ya Daraja la Sibiti kwa kuwa bajeti yake imetengwa mwaka huu wa bajeti? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

swali la nyongeza la Mheshimiwa Leah Komanya, Mbunge wa Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tunategemea kujenga barabara za maingilio zenye urefu wa kilometa alizozitaja kama 23. Barabara imeshakamilika na tuko mbioni kwa muda wowote tutakapokuwa tumekamilisha fedha kwa sababu tunaendelea na hiyo mipango ya kuhakikisha kwamba maingilio yale yanajengwa kwa kiwago cha lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango upo, tumeahidi na tutautekeleza kadri fedha zitakapopatikana, kama si mwaka huu basi mwaka wa fedha tutakaouanza.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kenyengenda Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa wananchi wa Makambako wana mategemeo makubwa sana katika eneo la Idofi ambako Serikali imekuwa ikiahidi kwa muda mrefu, je, ni lini watajenga *one stop center* na kumalizia fidia ambayo ilibaki kwa wananchi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Forodha cha Idofi ni kati ya vituo vingi vya Tanzania ambavyo tunategemea kuvijenga na tayari vilishaainishwa. Sasa hivi tunachofanya ni kupata fedha na kwanza kuwalipa fidia wale ambao wanapisha ujenzi na baada ya hapo tunaanza kujenga Kituo hiki cha Forodha pale idofi katika Jimbo la Makambako. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Napenda kuuliza, je, ni lini barabara ya mzunguko kwenye Manispaa ya Mororogoro kuanzia Juniour Seminary mpaka Kihonda itajengwa ili kupisha msongamano wa magari sehemu za Msamvu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum Morogoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Ishengoma kwa jinsia anavyofatilia ujenzi wa hii barabara ya mzunguko Morogoro. Taratibu bado zinaendelea za kufanya usanifu wa hiyo barabara ili kupunguza msongamano katika barabara kuu inayopita Msamvu kwenda Dar es Salaam. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara usanifu utakapokamilika barabara hii itanza kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mkundi, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Je, ni lini Serikali itajenga kilometa saba kwa kiwango cha lami za barabara kati ya Nasio-Mutunguru-Masonga ili kuondoa shida zilizopo kwenye barabara ile? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hiyo aliyoainisha Nansio Mutunguru yenye urefu wa kilomita saba ipo kwenye mpango mkubwa wa kujenga barabara ya lami. Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango bado upo, utanza tu pale ambapo fedha tutakuwa tumeipata na ujenzi huu tutaanza na kukamilisha hizo kilomita saba za lami katika Kisiwa cha Ukerewe.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, ni lini barabara ya Utegi hadi Kilongwe inayounganisha Nchi za Tanzania na Kenya kwa upande wa Rorya itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna kila sababu ya kuunganisha barabara zetu za lami na nchi jirani, lakini tuna barabara za kawaida na barabara kuu. Barabara ambayo tumeunganisha na Kenya ni ile barabara kuu ambayo inatoka Tarime kwenda mpaka wa Kenya ambao tayari ni barabara ya lami. Hata hivyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa barabara hii inatumika sana na wananchi wa Rorya na Watanzania kupitia Utegi kwenda Rorya, barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami kadri Serikali itakapokuwa imefanya usanifu na kupata fedha kwa ajili ya kujenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Chaurembo Abdallah.

Na. 67

**Kukamilisha Ujenzi wa Barabara ya Buza-Kilungule  
hadi Nzasa**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO K.n.y. MHE. MARIAM  
N. KISANGI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya kutoka Buza-Kilungule hadi Nzasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Buza-Kilungule hadi Nzasa ina urefu wenye jumla ya kilomita tisa. Barabara hii imekasimiwa kwenye mtandao wa barabara zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kupitia Wakala wa barabara *TANROADS* Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipo katika hatua za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kuanzia Nzasa hadi Buza kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam yaani *Dar es Salaam Metropolitan Development Project*. Mradi huu wa *DMDP* unasimamiwa na Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini (*TARURA*). Aidha, kwa sasa mkandarasi yupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Chaurembo Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda wa ujenzi wa barabara hii umekwisha, je,

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha barabara hii inaisha haraka ili kuondoa msongamano katika Barabara ya Kilwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali itamalizia kwa kiwango cha lami kipande cha kilometa tano cha Mbande- Kisewe mpaka Msongora?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chaurembo Abdallah, Mbunge wa Mbagala, kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tutahakikisha kwamba barabara ile kipande ambacho kimebaki cha kilometa tano chote tunakijenga kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na kukamilisha daraja ambalo limeshakamilika na sasa tunachoendelea ni kuweka lami pale juu kwenye daraja ambalo tunalijenga.

Kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kufikia mwakani barabara ile yote tutakuwa tumeijenga kwa kiwango cha lami ikiwa ni pamoja na kukamilisha hilo daraja ambalo lilikuwa ni changamoto kubwa sana kwa wananchi ambao wanatumia barabara hiyo.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, swali la nyongeza

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ujenzi wa barabara ya mwendokasi kwenda Mbagala pamoja na magari yanayotoka bandarini na kuingia bandarini na uwepo wa mizani katika eneo la bandari linaleta usumbufu mkubwa sana kwa wakazi wa Kigamboni ambao wanatumia Daraja la Nyerere. Je ni nini mkakati wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kuhakikisha kwamba adha wanazozipata wananchi zinaondokana na changamoto hizi?

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba barabara zote na hasa za mjini zinajengwa na kupanuliwa kwa maana ya magari yaweze kupita ama mawili ama matatu ama manne. Hata hivyo, kama kuna suala ambalo liko *very specific* kwa barabara ambayo ameinisha Mheshimiwa Mbunge, nitamwomba tuweze kuonana naye kama Wizara ili tuone kama kuna changamoto yoyote ambayo iko tofauti sana tuweze kuwa na mpango wa haraka kuweza kuondoa changamoto hiyo kwa hiyo barabara ambayo ameinisha Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Samweli Hayuma swali la nyongeza.

**MHE. SAMWEL X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Barabara ya Nangwa-Gisambalang-Kondoa inayotegemewa na Kata ya Gisambalang, Dirma, Simbai, Sirop na Wareta ina daraja ambalo limekatika toka mwaka 2019.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga hilo Daraja la Muguri B?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hhayuma, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, daraja alilolitaja ambalo liko sasa hivi kwenye usanifu na tunategemea kwenye mwaka wa fedha ujao daraja hilo lianze kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Napenda kuuliza swali moja barabara ya kutoka Kolandoto mpaka Meatu ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Napenda kuuliza swali moja.

Ni lini barabara ya kutoka Kolandoto mpaka Meatu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kolandoto kwenda Meatu ni kati ya barabara ambazo zimeainishwa kwenye Ilani, na pia zipo kwenye mpango wa kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kuanzia na kilometa 92. Kwa hiyo, sasa hivi kinachosubiriwa ni Serikali kupata fedha ili ujenzi wa barabara hii uanze. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Barabara ya kutoka Kinyerezi kupitia Segerea hadi Tabata Relini ni barabara ambayo imekuwa na changamoto kwa muda mrefu; na Serikali wamekuwa wakiahidi mara kwa mara bila ya utekelezaji.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, napenda kufahamu kauli sahihi kuhusiana na barabara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lambert, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Segerea kwenda Relini nilijibu wiki iliyopita wakati Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Segerea alipoliuliza. Nilichosema na bado naendelea kusema, barabara ilikuwa imefumuliwa na kulikuwa na changamoto ya Mkandarasi. Tunapongea sasa hivi, Mkandarasi yupo *site* kukamilisha vipande vyote ambavyo vilikuwa vimefumuliwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo barabara inaendelea kutengenezwa. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kyombo swali la nyongeza.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Kwa nyakati tofauti viongozi wetu wa kitaifa waliahidi wananchi wa Wilaya ya Misenyi kutengeneza barabara ya Mutukula kwenda Minziro, na kwa bahati nzuri Naibu Waziri alikwenda kutembelea eneo hilo, akapokelewa kwa shangwe, lakini mpaka leo barabara hii haijatengenezwa pamoja na kuingizwa kwenye bajeti.

Je, ni lini barabara hiyo ya Minziro - Mutukula itatengenezwa wananchi wapate huduma na kuinua shughuli za kiuchumi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.



*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kyombo, Mbunge wa Misenyi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwell barabara hii nilitembelea. Ni barabara ambayo inafunguliwa upya. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kuwa haikuwa kwenye mtandao, kwa hiyo, inaweza isionekane, lakini azma ya Serikali ni kuifungua na kujinga hii barabara. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Mgakorongo kwenda mpaka Mrongo ni barabara muhimu ya kiuchumi kwa Mkoa wa Kagera lakini pia inaunganisha nchi jirani ya Uganda. Barabara hii ni lini itaanza kujingwa kwa kiwango cha lami? (*Makoff*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bilakwate, Mbunge wa Kyerwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja ni barabara kuu inayounganisha Tanzania na Uganda kupitia mpaka wa Murongo ambayo inaanzia Umugakarongo - Kigarama hadi Murongo.

Mheshimiwa Spika, tunavyoongea sasa hivi, taratibu za manunuzi zinaendelea na ikiwezekana barabara hii itatangazwa kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jafari Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Barabara ya Utegi – Kowaki – Kinesi ni barabara iliyoahidiwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli toka akiwa Waziri wa Ujenzi. Nataka nijue ni lini sasa utekelezaji wa ujenzi wa lami wa barabara hii kutoka Kowaki mpaka Kinesi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii iliahidiwa na kiongozi. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeratibu ahadi zote ikiwepo na hii barabara ambayo ameanisha. Nimhakikishie kwamba barabara hii itajengwa kadri Serikali itakapopata fedha. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pallangyo swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Barabara ya Guguni inaanzia Tengeru Sokoni hadi Mererani, inaunganisha mikoa miwili ya Arusha na Manyara.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Pallangyo Mbunge wa Meru, kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri barabara hii naifahamu, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii ipo kwenye mpango wa kujenga kwa kiwango cha lami na tukizingatia inakwenda kwenye migodi yetu kule Tanzanite. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Uenge, Mbunge wa Viti Maalum. Litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi.

Na. 68

### **Mkakati wa Kuunganisha Barabara za Mkoa wa Tanga na Mikoa Jirani**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuunganisha barabara za Mkoa wa Tanga na mikoa jirani?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'azi Uenge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Serikali ni kuiunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Mkoa wa Tanga unapakana na Mikoa ya Pwani, Morogoro, Manyara, Kilimanjaro na nchi jirani ya Kenya. Tanga imeunganishwa na barabara zifuatazo: Tanga – Chalinze (Mkoa wa Pwani), Handeni – Tuliani hadi Magole (upande wa Mkoa wa Morogoro), Handeni - Kibilashi – Kibaya, (Mkoa wa Manyara),

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Tanga – Korogwe hadi Same (Mkoa wa Kilimanjaro) na kwa upande wa Kenya ni Tanga - Horohoro.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zipo barabara nyingine ambazo zinaunganisha Mkoa wa Tanga na mikoa ya jirani. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ukurasa 177, ipo barabara ya kutoka Same – Mkomazi - *Umba Junction* - Maramba hadi Tanga.

Je, ni lini upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utafanyika kwa barabara hii kuunganisha Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga kupitia Wilaya ya Lushoto na Mkinga? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili: Je, ni lini Serikali sasa itakamilisha upembuzi wa kina na usanifu katika kipande cha kutoka Mlalo kwenda *Umba Junction* kuungana na barabara hii ambayo nimeishaitaja? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Same - Kisiwani kuja Mkomazi ilikuwa inajengwa kwa vipande. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro hasa Mheshimiwa Mama Anna Kilango ambaye inamhusu sana barabara hii, kwamba barabara hii ambayo ina urefu usiopungua kilometa 92 inatangazwa yote

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kujengwa kwa kiwango cha lami na ipo kwenye hatua mbalimbali za kutangaza zabuni.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa swali lake la pili, kuhusu barabara hii ya Mlalo - *Umba Junction* Serikali inaanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Aleksia Kamguna, swali la nyongeza.

**MHE. ALEKSIA A. KAMGUNA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Serikali hutumia fedha nyingi sana katika kutengeneza barabara, lakini barabara hizo kwa muda mfupi tu huwa zinamomonyona na kuota manyasi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha kwa ajili ya *maintance* ya barabara hizi ili kuzinusuru? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kamguna kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi ambazo ni za changarawe ama za vumbi ni kweli kwamba hazidumu kwa muda mrefu na ndiyo maana zinatengewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya kila mwaka. Azma ya Serikali ni kujenga barabara zote kwa kiwango cha lami, lakini barabara hizi ni gharama, kwa hiyo, inategemea na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, zile barabara kubwa za mkakati ndiyo tutaanza kuzijenga kwa lami, lakini kadri bajeti itakavyoruhusu, mpango ni kuzijenga barabara zote kwa lami zikiwepo na barabara za Mheshimiwa Mbunge. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani muwe na utaratibu hasa kwa barabara ambazo zimeshajengwa kwa

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kiwango cha lami, ziwe zinatengewa fedha kwa ajili ya matengenezo madogo madogo. Kwa sababu mkishakamilisha, mnakuwa mmeshatumia fedha nyingi sana kwenye hizo barabara, halafu mashimo yale yanaanza kidogo, kama jiwe hivi, baadaye shimo linaendelea kuwa kubwa.

Sasa katika mazingira hayo, tunarudi tena kule nyuma, fedha zinatumika nyingi sana kuja kutengeneza upya hiyo barabara. Ukiacha hii ya kutoka hapa kuelekea Iringa, hilo ni janga, hiyo wala siyo ya mashimo, ni ya kuondoa yote; lakini barabara ya kutoka Mbeya Mjini kuelekea Chunya, ile barabara zimetumika fedha nyingi sana na sasa ina mashimo na zile kona kule na mashimo, maana yake magari yatakuwa yanapitiliza tu kule bondeni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hoja ya Mheshimiwa Mbunge ni kwamba mnavyotengeneza barabara za changarawe mtenge na fedha za matengenezo. Mnavyotengeneza barabara za lami, pia mtenge fedha za matengenezo ili ikionekana dosari ndogo ishughulikiwe mapema kabla tatizo halijawa kubwa sana, kwa hivyo mnamtumia fedha nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa fursa hii. Mkoa wa Tanga haujaunganishwa na Mkoa wa Manyara pamoja na Mkoa wa Morogoro kwa barabara ya lami. Ni lini Serikali itajenga barabara Handeni – Kibilashi – Kiteto – Kondoa - Singida na ile ya Handeni kwa Magome...

**SPIKA:** Sasa huwezi kutaja... *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mbunge!

**MHE KWAGILWA R. NHAMANILO:** Naam!

**SPIKA:** Moja tu, kwa sababu ni swali la nyongeza. Kwa hiyo, ni ile uliyoitaja mwanzoni kabisa.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Shukrani sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niseme Serikali imepokea ushauri ulioutoa. Nikuhakikishie kwamba katika bajeti ijayo limezingatiwa na tutaendelea kuzingatia zaidi ili kuokoa hizi barabara ambazo tayari zimeshajengwa.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Reuben Kwagilwa Mbunge, nataka nikuhakikishie kwamba barabara hii ambayo tumeitaja kutoka Handeni - Kiberashi kwenda Kibaya ni barabara ya changarawe na tayari tupo kwenye hatua za manunuzi, kilometa 50 kuanzia Handeni kuja Kiberashi kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami; na kama taratibu zote zitakamilika, barabara hii itaanza kujengwa mwaka huu wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtemvu, swali la nyongeza. Samahani, Mheshimiwa Omari Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nataka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, barabara ambayo inaanzia Dumila kupita Turiani kupita Kata ya Negelo hadi Vibaoni Handeni, ni barabara muhimu sana. Kwa upande wa Morogoro imeshakamilika kwa kiwango cha lami: Je, ni lini kilometa 120 kwa kiwango cha lami itakamilishwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Omari Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoiainisha imeshafanyiwa usanifu; na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kwa umuhimu wa barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, hapo ni upatikanaji wa fedha tu, *once* tutakavyopata barabara hii itaanza kujengwa. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Mkoa wa Tabora hadi leo haujaunganishwa na Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Songwe; na kipande muhimu kabisa ambacho kinaunganisha mikoa mitano ni kipande cha kutoka Ipole mpaka Rungwa ambacho usanifu wa kina ulikamilika na tayari shilingi bilioni tano zikatengwa mwaka huu.

Ni lini hiyo barabara itajengwa ili Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Mbeya na Songwe ziunganishwe? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakunda, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kipaumbele ni kuunganisha mikoa na mikoa na barabara aliyoitaja siyo tu kwamba ni mkoa, lakini pia ni kati ya zile barabara kuu kutoka Tabora - Ipole hadi Rungwa ambayo inaunganisha na barabara inayotoka Manyoni - Singida kwenda Makongorosi.



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, kipande cha Manyoni - Itigi kuja Rungwa tunategemea muda wowote kutangazwa; na kipande cha Ipole kuja Rungwa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami ili barabara hiyo ambayo inaunganisha siyo tu na Tabora, ila na mikoa mingi ya Kaskazini iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniface Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Bariri kwenda Hunyali na kwenda mpaka Mgeta ni barabara ambayo iko kwenye barabara inayotoka Mwanza kwenda Musoma na barabara inayokwenda Serengeti. Kipande hicho cha barabara Mheshimiwa Rais Samia alipokuwa Bunda tuliomba kwamba kipande hiki kijengwe kwa kiwango cha lami. Ni lini barabara hii itajengwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni ahadi ya Rais, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara inaendelea kuifanyia kazi ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kama Mheshimiwa alivyokuwa ameahidi. Kwa sababu hayo sisi kwetu ni maelekezo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutatekeleza kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, swali la nyongeza.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kuhusu ujenzi wa barabara ya kutoka Maramba kwenda Humba kwenda Mlalo. Ni ipi kauli ya Serikali juu ya kipande cha kuunganisha kutoka Maramba - Mashewa kwenda *Old Korogwe* mpaka Korogwe Mjini? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, barabara aliyoinisha ipo kwenye mpango wa kukamilisha usanifu wa kina wa barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge inayoanzia *Old Korogwe* hadi Mabokweni kama nimemwelewa. Nadhani ndiyo hiyo barabara; ipo kwenye ukamilishaji wa kufanya usanifu ili iweze kuanza kwa kiwango cha lami baada ya kukamilisha usanifu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara ya kutoka Masasi - Nachingwea kwenda Liwale ni barabara ya mkakati: Je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hiyo? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maimuna, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara aliyoitaja inaanzia Mtwara - Mnivata - Newala hadi Masasi, ina urefu wa kilometa 210. Kilometa 50 atakubaliana nami zimeshajengwa; na tunavyoongea sasa hivi, tupo kwenye hatua za mwisho, *African Development Bank* wanaijenga hiyo barabara; na

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

kuanzia mwezi Tisa ama wa Kumi hii barabara itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami kilometa zote 160. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge wa Nungwi sasa aulize swali lake.

Na. 69

### **Hitaji la Gari na Nyumba za Polisi – Kituo cha Polisi Nungwi**

**MHE. SIMAI HASSAB SADIKI** aliluliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua changamoto ya ukosefu wa magari na nyumba za Askari Polisi Kituo cha Polisi Nungwi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Jumanne Sagini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Nungwi ni kituo cha Daraja C na kipo Mkoa wa Kaskazini Unguja. Pamoja na kufanya kazi mbalimbali za kipolisi, hushughulikia pia na kusimamia majukumu ya utalii.

Mheshimiwa Spika, Kituo hiki kinacho gari Na. PT. 3388, Toyota *Landcruiser* ambalo hutumika kwenye kazi za kila siku za polisi. Kutokana na udogo wa eneo la kituo, hakuna sehemu inayoweza kutosheleza kujenga nyumba za makazi ya askari polisi. Hivyo, Serikali inawashauri wadau wenye

nyumba za kupangisha wapangishe askari wetu. Aidha, uongozi wa Mkoa Kaskazini Unguja unaombwa ushirikiane na uongozi wa jamii kupata eneo linalofaa kujenga nyumba za askari ili Serikali iingize ujenzi wa nyumba hizo katika mpango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hassan Sadick Simai, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa sasa Nungwi imebadilika hadhi kutoka kijiji kuelekea mji na kwa kuwa sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la watu pamoja na wawekezaji katika sekta ya utalii wa Kimataifa.

Je, Serikali haioni haja ya kuongeza majengo na watendaji ili kukiongezea daraja Kituo cha Polisi Nungwi kutoka daraja C kwenda B?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa Nungwi kumekuwa na changamoto kubwa mno ya upatikanaji wa maji jambo ambalo limewapelekea maaskari wengi kuondoka kituoni kwenda sehemu za mbali kutafuta maji hayo. Je, Serikali haioni haja ya kuwachimbua kisima au kutafuta njia mbadala ili kuhakikisha kuna upatikanaji wa maji ya kudumu katika eneo lile? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Simai, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja tunatambua kweli maeneo mengi ya vijijini ikiwemo Kijiji cha Nungwi kimekua na kuwa Mji Mdogo na watu wameongezeka, lakini kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, eneo hili ni dogo, kama tunadhamira

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya kupanua, basi Mheshimiwa Mbunge atusaidie kushirikiana na Mamlaka ya Wilaya pale ili tupate eneo la kutosha kuweza kujenga kituo kinachokidhi mahitaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la upatikanaji wa maji, naomba nishauri kwamba, kazi ya Jeshi la Polisi sio kuchimba visima, lakini kule kuliko na polisi kama walivyo wananchi wengine mamlaka za ugawaji wa maji ziwafikie kwa ajili ya kuangalia uwezekano wa kuwachambia kisima. Tutawasiliana na wenzetu wa upande wa Zanzibar ili kuona uwezekano wa kuwapatia kisima wenzetu hawa ili wasiende umbali mrefu kutafuta maji. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Juma Usonge, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Mwaka, 2013 Kituo cha Polisi cha Mkokotoni kilipata majanga ya kuungua kwa moto na hadi kufikia tarehe 29 Machi, kituo hicho tayari kimekamilika kwa asilimia 95. Je, ni ipi kauli ya Serikali ili kukamilisha asilimia hizi tano ili kituo kile cha polisi kiweze kufanya kazi vizuri kama inavyotakiwa? (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Usonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ikiwa wananchi wamejitahidi kukamilisha kituo kwa kiwango cha asilimia 95, nachukua dhima ya kuwasiliana na wenzetu wa Jeshi la Polisi kupitia Mfuko wao wa Tunzo na Tozo kukamilisha asilimia tano zilizobaki ili kituo hicho kiweze kukamilishwa. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Licha ya juhudi kubwa anazofanya Mbunge wa Jimbo la

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Peramiho, je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi pale Peramiho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Thea Ntara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hitaji la kuwepo Kituo cha Polisi katika eneo la Peramiho ni kubwa kutokana na kukua kwa kasi ya shughuli za kibinadamu kwenye eneo hilo la Peramiho. Namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Ruvuma, tutaona uwezekano wa kuingiza eneo la Peramiho katika mpango wa ujenzi wa kituo cha polisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Sasa tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, sasa aulize swali lake.

Na. 70

**Hitaji la Kambi ya JWTZ Tunduru**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kurejesha Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Tunduru ili kuimarisha ulinzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stargomena Tax, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini, kama iufatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuimarisha ulinzi katika mipaka ikiwa ni pamoja na mpaka wa Kambi ya Wananchi wa Jeshi la Tanzania Tunduru na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ipo katika mchakato wa kurejesha Kambi ya Jeshi la Wananchi Wilayani Tunduru. Tayari Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekwishaomba fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kambi hiyo toka Wizara ya Fedha na Mipango.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali la kwanza; kwa kuwa, Waziri amesema tayari mipango ya kufufua Kambi ile inaendelea na sasa hivi hali ya usalama upande wa kusini hasa upande wa Msumbiji sio nzuri katika Vijiji vya Wenje, Lukala, Nasomba, Makandi na Kazamoyo watu hawa wanaishi kwa kutokuwa na amani. Je, haoni sasa ni muhimu kuweka angalau makambi ya *temporary* ili kurejesha amani ya wananchi wa vijiji hivyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa vijiji hivyo kwa sasa ulinzi umekabidhiwa kwa mgambo ambao wako 30 katika vijiji hivyo na wanapewa sh.50,000/= kwa mwezi na Halmashauri.

Je, Serikali haioni sasa ni muhimu kuwalipa mshahara mgambo wale ili waweze kuendelea kulinda mipaka?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali ilivyo katika mipaka yetu yote ikiwa ni pamoja na mpaka wa Kusini na tayari hatua mbalimbali zimechukuliwa kuimarisha ulinzi, hatukai tu tukisubiri kambi. Kambi itakuja lakini hatua za kuimarisha ulinzi katika mipaka hiyo zinaendelea na ulinzi umeimarishwa.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu malipo, kwa mgambo kuwa na mishahara upo utaratibu unaotumika kulipa Jeshi la Mgambo na utaratibu huo utaendelea kutumika. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haji Amour Haji, swali la nyongeza.

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nina swali moja la nyongeza. Kule Zanzibar kuna Kambi inaitwa Ubago sasa Kambi ya Ubago kwa sasa hivi wapo katika hatua za kutaka kuongeza maeneo ya kambi katika eneo la Dunga pamoja na Bimbuni, ambapo wananchi mpaka sasa hivi wanakosa amani na wanaendesha shughuli zao mle za kuendesha maisha yao na harakati zao.

Je, Serikali inawaambia nini wananchi wale ambao wapo katika maeneo yale ya Dunga pamoja na Bimbuni? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haji hilo ni swali la msingi, kwa sababu hapa swali la msingi linauliza kuhusu kurejesha Kambi ya Jeshi huko. Sasa nilifikiri kuna mahali wanaihitaji hiyo Kambi ya jeshi, huko unakoulizia si ni kwamba Kambi ipo tayari?

**MHE. HAJI AMOUR HAJI:** Mheshimiwa Spika, huko kunakotaka kuchukuliwa sio kwamba kuna Kambi, isipokuwa kwamba ni maeneo tu ambayo yanataka kuchukuliwa na Jeshi la Wananchi ambayo wananchi wanaendesha shughuli zao, Kambi iko mbali Bumbuni iko mbali na Dunga iko mbali. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wale ambao wako katika maeneo yale?



## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Sawa swali lako litajibiwa kama swali la msingi, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, ahsante sana kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 71

### **Kufufua Kilimo cha Zao la Muhogo – Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kufufua kilimo cha zao la muhogo katika Mkoa wa Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ilianzisha Mradi wa Kufufua Zao la Muhogo katika Kanda ya Ziwa Victoria na Kanda ya Pwani ukiwemo Mkoa wa Mtwara mwaka 2015. Awamu ya Kwanza ya mradi huo iliisha mwanzoni mwa mwaka 2021, awamu ya pili imeanza Disemba, 2021 na inategemewa kwisha mwaka 2024. Kupitia mradi huu uzalishaji wa muhogo katika Mkoa wa Mtwara umeongezeka kutoka tani 611,210 kwa mwaka 2016/2017 hadi tani 866,676 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongeza utoaji wa huduma za ugani na uzalishaji wa mbegu za muhogo. Jumla ya vipando bora vya muhogo pingili milioni 30.4 kwa mwaka 2019/2020 hadi pingili milioni 40 kwa mwaka 2020/2021 zenye

uwezo wa kutoa mavuno mengi kuhimili mabadiliko ya tabia nchi na magonjwa zilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; ili zao hili liweze kufufuka na kuleta tija sio kupeleka mbegu bora tu ni pamoja na kutafuta masoko mazuri nay a uhakika ili wakulima waweze kuuzwa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha masoko ya uhakika yanapatikana?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; sisi Mkoa wa Mtwara muhogo ukilimwa unastawi kweli kweli lakini tunashindwa kulima kwa sababu hakuna kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la muhogo. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inajenga kiwanda yenyewe ama kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza thamani ya zao la muhogo? Nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika swali la kwanza la kuhusu masoko hivi sasa Wizara tumeendelea kuimarisha huduma za masoko kwa kuhakikisha kwamba mazao yetu mengi tunayatafutia masoko, ili wakulima wetu wakilima kwa tija mwisho wa siku mazao yao yaweze kupata masoko ya uhakika. Nataka nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba moja kati ya mkakati tulionao hivi sasa ni kufanya muhogo kama sehemu ya malighafi kuu katika viwanda vyetu ambavyo tumeanza mazungumzo nao kwa ajili ya kutengeneza wanga ambao hivi sasa tunaagiza karibuni tani 8,000 kwa mwaka. Kwa hiyo, tumeanza mazungumzo na

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

viwanda vilivyoko hapa nchini kwa ajili ya kufanya muhogo kama malighafi ya utengenezaji wa wanga. Zoezi hilo linakwenda vizuri na mwikio umekuwa mkubwa na ndio maana sasa tumeendelea kuhamasisha wakulima wengi zaidi kulima muhogo.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu viwanda. Ni kweli mwisho wa siku kama Wizara katika mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ya mazao yetu na kwa upande wa muhogo viko viwanda ambavyo mwanzoni vilionesha nia ya kuanza kufungua katika upande wa kule Kusini. Kwenye Kijiji cha Malamba katika Jimbo la Mtama ipo kampuni ambayo ilifungua kiwanda, Kampuni ya *Cassava Starch of Tanzania Corporation* bahati mbaya sana walipata changamoto ya mtaji na hivi sasa wana *administration order* ya Mahakama ya Biashara *Management* wameamua kukichukua kiwanda kile na wanatafuta wawekezaji. Wameshakuja wawekezaji kutoka Japan na maeneo mengine na sisi kama Wizara tunaendelea kuwasaidia kutafuta wawekezaji ili kiwanda kile kifufuliwe na kiwe sehemu ya uchakataji wa muhogo ya wakulima wa Mkoa wa Mtwara, Mkoa wa Lindi na Mikoa yote ya Kusini. Nakushukuru sana. (Makofi)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu kwa maswali hayo ya Mheshimiwa Mbunge. Tumalie na Wizara ya Maji Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake.

Na. 72

### **Hitaji la Maji Kata za Namajani, Mpanyani Mlingura, Msikiri na Chingulungulu (Kata ni Namalutwe) – Ndanda**

**MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka maji katika Kata za Namajani, Mpanyani, Mlingula, Msikiri na Chingulungulu (Kata ni Namalutwe) zilizopo katika Jimbo la Ndanda?

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca, Mahundi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mlingula ina Vijiji vitano vyenye huduma ya maji ambavyo ni Mlingula, Chikoweti na Nambaya. Aidha, katika kuboresha huduma ya maji kwenye Kata hiyo vijiji vya Namichi na Masikunyingi vinapata huduma ya maji kupitia bomba kuu linalopeleka maji kwenye maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (NAWASA). Kazi ya usanifu wa miundombinu ya maji itakamilika mwezi Juni, 2022 na ujenzi utafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Mheshimiwa Spika, Kata za Namajani zina vijiji vitano ambavyo vinapata huduma ya maji ni Namahinga, Ngalele, Namajani. Kata ya Mpanyani ina vijiji vitano ambapo Vijiji vya Muungano Nambawala A na Nambawala B vinapata huduma ya maji. Kata ya Nsikisi ina vijiji vitatu ambapo Kijiji cha Namalembo kinapata huduma ya maji. Vile vile katika Kata ya Namalutwe pale pameandikwa Chingulugulu, naomba isomeke Namalutwe kwa sababu Chingulugulu ni kijiji na Kijiji cha Chingulugulu kina huduma ya maji. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 kazi ya utafiti wa maji chini ya ardhi imekamilika katika vijiji nane katika Kata hizo nne na uchimbaji wa visima unaendelea na miundombinu ya maji itafanyika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe, swali la nyongeza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwa namna ya pekee nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri na Wizara nzima ya Maji kwa utekelezaji wa miradi

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii aliyoitaja swali lake na majibu ni mazuri sana. Hivi sasa Kata ya Nanganga, Mumburu unatekelezwa mradi wa maji wa shilingi milioni 500, Ndanda shilingi milioni 400, Chiwata mradi unaendelea shilingi milioni 500. Hata hivyo, napenda kufahamu toka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, wakati wa usanifu wa miradi ya Kata ya Mpanyani alipokuja Katibu Mkuu tulikubaliana kwamba Kijiji cha Mraushi patawekwa tenki. Je, ni lini kazi ya ujenzi wa tenki Kijiji cha Mraushi itaanza kufanyika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kati ya Mwena na Liloya kuna mradi unaoendelea. Kwa bahati mbaya sana mradi huu unafanya kazi vizuri sana wakati wa mvua na wakati wa kiangazi haufanyi kazi vizuri, unahitaji tena kufanyiwa marekebisho. Je, ni lini Serikali itakwenda kuufanyia marekebisho Mradi wa Liloya-Mwena? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nipokee pongezi, nafahamu anayeshukuru anaomba tena, tutarudi Ndanda tutaendelea kufanya kazi pamoja Mheshimiwa Mbunge na nampongeza Mbunge kwa uwajibikaji wake mzuri.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa tenki tunautarajia ndani ya mwaka wa fedha 2022/2023 uweze kukamilika. Vile vile katika ule mradi ambao tayari unatoa huduma japo maji kidogo yana chumvi na wakati wa kiangazi inaleta shida, Mheshimiwa Mbunge hili tumeshaliongea mara nyingi, amefika ofisini na sisi tayari tumeshalifanyia kazi, tumeshatoa maagizo pale Mtwara. Kwa hiyo, litaendelea kuangaliwa kwa jicho la kipekee kuhakikisha wananchi wanakwenda kupata maji safi, salama na ya kutosha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ghati Chomete swali la nyongeza.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Shule nyingi za sekondari na *primary* Mkoani

Mara hazina miundombinu ya maji. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha miundombinu hiyo inawafikia ili kuepuka magonjwa ya milipuko? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ghati Chomete, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Mara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Ghati amekuwa ni mlezi mzuri sana wa watoto mashuleni na amefuatilia sana hili suala la huduma ya maji mashuleni. Naomba nitumie Bunge lako Tukufu kuwaagiza Viongozi wa Mkoa wa Mara kwa maana ya *MD* na *RM* wahakikishe wanapeleka maji mashuleni, hili tulishaagiza, ni ufuatiliaji na utekelezaji tu, hivyo waweze kufanya kuanzia sasa na mwaka ujao wa fedha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwita Kembaki, swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni kwamba, katika mji wetu wa Tarime Mjini tunacho chanzo cha Nyandurumo ambacho ndicho kinacholisha maji katika Mji wetu wa Tarime, lakini Nyandurumo hii ipo katika Kata ya Kenyamanyori. Wakazi wa Kenyamanyori hawana maji.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, wakazi wa Kenyamanyori wanapata maji ili waweze kutunza chanzo hiki ambacho ni muhimu sana katika Mji wetu wa Tarime? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Spika ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Michael, Mbunge wa Tarime, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nampongea Mheshimiwa Michael, alishaniona katika hili. Sera ya Maji inataka vijiji vyote vilivyopo katika eneo la chanzo wawe wanufaika namba moja. Naendelea kutoa maagizo kwa *MD* na *RM*s waweze kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao. Tunakwenda kuhakikisha watu wote wanaopitiwa na mtandao wa bomba wananufaika na maji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba niulize swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Kata ya Kazuramimba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nashon, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miradi yote ambayo ipo kwenye utekelezaji, tunaendelea kwa kasi nzuri sana kuhakikisha inaisha ndani ya wakati. Mheshimiwa Mbunge kama tulivyozungumza, tutasimama kwa pamoja kuhakikisha mradi huu unaisha ndani ya wakati. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Felista Njau, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Katika Kata ya Mbezi Juu, Mtaa wa Mbezi Mtoni na Sakurveda kuna changamoto kubwa ya

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

maji. Ni lini Serikali itapeleka miundombinu hii ili wananchi waweze kupata huduma hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Felista Njau, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi lengo letu ni kuona tunatua akinamama ndoo kichwani na Mheshimiwa Felista amefuatilia hili, ameshaongea nami. Kama tulivyozungumza, mantahofu, haya maeneo yote maji yatapelekwa na tunataka kuhakikisha ukifika mwaka 2025 maeneo yote ya vijijini yatapata maji kwa asilimia 85 na asilimia 95 kwa maeneo ya mijini. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu yako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Waheshimiwa Wabunge ninalo tangazo hapa la Waheshimiwa Wabunge ambao wamekaribisha wageni hapa.

Kwanza ni wageni 23 wa Mheshimiwa Anna Lupembe, ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwenyekiti wa Wanamaombi, Ndugu Isaya Njendaluzi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi 10 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Ndugu Livingstone Gwamagila. Karibuni sana. Tunaamini mmeweza kujifunza mambo mawili, matatu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na ratiba iliyo mbele yetu, sisi sote tunatambua siku ya jana, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amezindua Makala Maalum ya kuhamasisha utalii nchini Tanzania; na kwa sababu, Waheshimiwa Wabunge huwa



## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

mnachangia sana kuhusu kuongezq idadi ya watalii wanaokuja kwa niaba yenu wote, sisi kama Bunge, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua anazozichukua kwenye hili eneo la kuongeza watalii. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa sababu bajeti ya Wizara hii ya maliasili na utalii itakuja baadaye, ni muhimu sana kila Mbunge afuatilie mambo yanayoendelea huko ili kama kutakuwa na la kushauri hapa na pale, itakuwa rahisi zaidi baada ya kujua hatua mbalimbali ambazo zimeshachukuliwa na zile tunazotamani ziongezeke baada ya hapo. Kwa hiyo, ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge kufuatilia ziara hii ya Mheshimiwa Rais nchini Marekani ya kutangaza taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kutoa pongezi hizo, tunaendelea na ratiba iliyo mbele yetu.

Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshaletewa hapa majina ya Wabunge ambao wameomba kuchangia kwenye hoja hii ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa orodha iliyoko hapa mbele watachangia kwa dakika nane, Wabunge wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na upande wa upinzani ama Kambi ya Walio Wachache watachangia kwa dakika zao kumi.

Tutaanza na Mheshimiwa Ikupa Alex, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa jinsi anavyonilinda, anavyonitetea na anavyonipigania katika majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyoendelea kumpa hekima, busara na maarifa ya kuliongoza Taifa letu. Nina hakika tunaona ni kwa jinsi gani anavyoendelea kuupiga mwingi kwenye maeneo mbalimbali, yaani kwenye sekta mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie nafasi hii kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi ambavyo imeendelea kuyapa kipaumbele masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu. Tukianza kwenye Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ilieleza mambo mengi kwenye eneo la watu wenye ulemavu; na pia kwenye Hotuba hii ya TAMISEMI, imeeleza mambo mengi ambayo yanatarajiwa kufanyika na yale ambayo jameshafanyika.

Mheshimiwa Spika, mojawapo ambalo lilikuwa ni changamoto kubwa kwenye maeneo ya shule zetu, ni uzio. Shule nyingi zilikuwa hazina uzio ambapo sasa ilikuwa inasababisha kuhatarisha maisha ya watoto mbalimbali na hasa ikizingatiwa kwamba, watoto wengi kwenye maeneo hayo unakuta ni walemavu wa akili, pia kuna watoto wenye ualbino, kwa hiyo, ilikuwa ni changamoto kubwa. Naipongeza sana Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba changamoto hii inaenda kutoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, naipongeza na kuishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya kujenga

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mabweni kwenye shule za watoto wenye ulemavu. Kwenye maeneo mengi watoto wanashindwa kwenda shule kwa sababu ya umbali, lakini sasa uwepo wa mabweni haya utawezesha watoto wengi wenye ulemavu kuweza kusoma na hatimaye kuwa na uhakika wa masomo yao kwa kadiri ambavyo wanaendelea. Kwa kweli sisi kama watu wenye ulemavu Tanzania, tunaishukuru sana Serikali na tunaendelea kuiomba mipango hii iweze kutekelezeka kwa wakati kama ambavyo imepangwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii pia limeongelewa suala zima la utambuzi wa watu wenye ulemavu. Pale ambapo suala hili la kuwatambua watu wenye ulemavu limefanyika imekuwa ni vizuri kwa sababu, wanapotambuliwa inakuwa pia ni rahisi kufahamu na mahitaji yake. Hotuba imeeleza wazi kwamba, wamewatambua na hatimaye wameweza kuwapatia mahitaji mbalimbali miongoni mwa wale waliotambuliwa. Hivyo pia, nikiwa kama mwakilishi wao, ninawashukuru sana na kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, limeendelea zoezi la uandikishwaji watoto kwa maana ya kuanzia elimu ya awali, msingi na kuendelea; na tunaona kabisa kwamba idadi ya uandikishwaji inaongezeka. Ilikuwa ni kilio cha muda mrefu na changamoto kubwa kwamba, watoto wengi wenye ulemavu walikuwa hawaendi shule, lakini kwa *trend* hii inayoendelea, tunaona kabisa kwamba kundi hili la watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma na hatimaye na wao wanaenda kupata elimu kama watoto wengine. Ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, yako mambo mengi ambayo yamefanyika kwa mujibu wa hotuba hii, na kwa kadiri ya ambavyo tunayaona sisi watu wenye ulemavu. Kipekee kabisa nilete salamu nyingi za watu wenye ulemavu kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Tunamshukuru Rais wetu kwa sababu aliweza kutualika Ikulu ya Chamwino, tukakaa naye, tukazungumza naye,

tukawasilisha changamoto zetu mbalimbali ambazo kwa kweli, Mheshimiwa Rais changamoto zile, nyingi zimeshaanza kufanyiwa kazi na nyingine zimeshapata suluhisho na nyingine ziko katika hatua ya utekelezaji. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo kuna baadhi ya changamoto ambazo ninaomba niziwasilishe mbele ya Serikali. Changamoto ya kwanza ni utolewaji wa mafuta ya watu wenye ualbino kwenye Halmashauri zetu. Hii imekuwa ni changamoto ya muda mrefu; miongozo ipo, kanuni zinaongea wazi, lakini suala hili halitekelezeki kwenye Halmashauri zetu. Nimekuwa nikipokea simu mbalimbali kutoka kwa watu wenye ulemavu wakilalamikia suala hili kwamba, Halmashauri hazitoi mafuta haya.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikisema kwamba mahitaji ya watu wenye ulemavu ni kama chakula. Vile ambavyo binadamu mwingine anahitaji kula, hivyo, mahitaji haya ni ya muhimu sana kwa kundi hili la watu wenye ulemavu. Naiomba Serikali, suala hili liweze kutekelezeka kwa maana ya kwamba, Halmashauri ziweze kutenga, kununua na kusambaza mafuta haya kwa watu wenye ualbino. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, namwomba Waziri anapokuja kuhitimisha, basi aweze kulielezea suala hili kwa kina, ni kwa nini halitekelezeki? Pia, niseme wazi kwamba, maelezo ya Mheshimiwa Waziri yasiponitoshela, nitashika shilingi yake na nitaondoka na huo mshahara wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile ieleweke wazi kwamba familia nyingi ama watu wenye ulemavu walio wengi wanaishi kwenye kipato cha chini sana kiasi cha kushindwa kumudu matibabu yao. Naishauri na kuiomba Serikali iweze kufanya zoezi ambalo lilifanyika kwa wazee, kuwatambua na kuwapatia vitambulisho wale ambao hawana uwezo wa kupata matibabu ili basi, vitambulisho vile viwawezeshe kutibiwa kwa urahisi.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, suala hili ni muhimu sana kwa sababu, wengi wanapata changamoto kubwa. Sasa unakuta mtu anakupigia simu, Mbunge nisaidie matitabu; na idadi ilivyo kubwa unajikuta unashindwa kusaidia kwa ukamilifu wake kwa wale ambao wana uhitaji. Hivyo, naiomba Serikali iweze kuwatambua watu wote ambao wanashindwa kumudu matibabu kama ilivyofanya kwa wazee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kabisa, kwa sababu muda umekuwa siyo rafiki, niwahamasishe watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kuweza kuhesabiwa, lakini pia elimu hii kwa wale viongozi wa watu wenye ulemavu waweze kuitoa kwa wenzao. Kwa maana kuhesabiwa ni muhimu, yamkini mambo mengi hayatekelezeki kwa sababu Serikali haina idadi yetu kamili. Hivyo, niwaombe sana watu wenye ulemavu wajitokeze kuhesabiwa; na pia watu ambao wanaishi na watu wenye ulemavu wasiwafiche kuhesabiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula na Mheshimiwa Neema William Mgaya ajjandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii ambayo umenipa ili nami niweze kuchangia Wizara hii ya TAMISEMI. Kwanza kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Innocent Bashungwa pamoja na Manaibu Mawaziri wake; Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Festo John Dugange na wataalamu wote wa Wizara hii ya TAMISEMI. Naomba ifahamike wazi kwamba, Wizara hii ni muhimu sana na ni roho ya wananchi wa Tanzania na tunawategemea sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie pia, nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, kwa uongozi wake mahiri wa mwaka mmoja ambao

umekwenda kupita sasa. Tunapompongeza Mheshimiwa Rais, wako baadhi ya watu wanadhani pengine tunafanya utani.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa upande wa Jimbo la Lupembe, ndani ya huu mwaka mmoja wa Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, tulikuwa na Kata kama ya Ikondo ambayo tangu kuumbwa kwa ulimwengu wa dunia hii hakujawahi kuwa na kituo cha afya wala shule ya kata, lakini Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amewafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa hatuna shule shikizi kwenye maeneo kama ya Madeke na maeneo ya Itova. Ndani ya mwaka mmoja, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amewafikia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, wananchi wangu wa Mtwango pale Lunguya wamekuwa na shida ya muda mrefu ya barabara ya Lunguya kwenda Welela. Ndani ya mwaka huu mmoja tu Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amewafikia wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, Njombe *DC* tulikuwa hatuna Makao Makuu ya Halmashauri, Mheshimiwa Silinde alikuja mwaka 2021 kule; tulikuwa hatujaanza hata kujenga msingi, lakini ndani ya huu mwaka mmoja pekee, Mheshimiwa Rais ametuletea fedha shilingi bilioni 1,900 na hivi sasa ujenzi wa makao makuu upo kwenye *level* ya lenta. Nani kama Samia Suluhu Hassan? Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais tunapompongeza Mheshimiwa Rais tunamaanisha na kazi anazifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaposhukuru hivi, ni ishara pia ya kuomba tena. Unaposhukuru ni kwamba, unataka kuomba tena. Halmashauri ya Njombe *DC*, pamoja na kazi nzuri ambazo Mheshimiwa Rais na Serikali imefanya, tunazo changamoto katika maeneo kadhaa ambayo napenda kuyabainisha. Kwanza alipokuja Mheshimiwa Silinde, Naibu Waziri, ikapendekezwa kujenga Makao Makuu ya Halmashauri. Eneo hili halina kituo cha afya. Kwa hiyo, eneo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambalo tunakwenda kujenga Makao Makuu ya Halmashauri patakuwa na watumishi wengi sana. Tunaiomba Serikali ipeleke Kituo cha Afya katika Kata ya Kidegembye.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, alipokuja Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Ummu, alituhidi kutupatia kituo cha afya kwenye Kata ya Ikuna na tulishauriwa kwamba, tusiendelee na ujenzi wa kile kituo cha afya badala yake tuelekeze nguvu kwenye ujenzi wa kituo cha afya kikubwa cha pale Mtwango kwa mapato ya ndani. Napenda kutoa taarifa, Halmashauri ya Njombe DC chini ya usimamizi wa Mkurugenzi wetu mahiri sana, Dada Sharifa Yusufu Nabarang'anya, tumeshajenga kituo cha afya kwa mapato ya ndani chenye majengo zaidi ya nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri yetu imejenga kituo cha afya kwa mapato ya ndani kwa majengo zaidi ya nane, naiomba sana Serikali iwasaidie wananchi wa Mtwango, Ilunda, Welela, Sovi na Itunduma, kupata vifaatiba kwenye hospitali hii. Kama itapendeza pia wananchi hawa wangepata watumishi wa afya na vifaatiba na vifaa tendanishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya Waziri amezungumza mafanikio mengi sana ambayo yamepatikana. Nilikuwa napenda kumshauri Mheshimiwa Waziri kwamba ufanisi huu wa TAMISEMI unasaidiwa pia na Wakurugenzi kwenye Halmashauri zetu. Napenda kutoa ushauri kwa Wizara, wapo Wakurugenzi ambao wamemwelewa sana Mheshimiwa Rais na wanafanya kazi nzuri sana, akiwemo Mkurugenzi wangu wa Njombe DC, dada yangu Sharifa. Nilikuwa namshauri, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, tunakokwenda, aanze kutoa zawadi maalum kwa Wakurugenzi wanaofanya vizuri kwa ajili ya motisha. Hili jambo litakuwa ni muhimu sana kuwatia motisha ili na Wakurugenzi wengine wajifunze kufanya kazi kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kushauri kuhusu asilimia 10. Kwenye mchango uliopita hapa ndani, Mbunge

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Makete alisema kwa ufasaha kwamba fedha nyingi za mfuko za asilimia 10 hazirudishwi kwenye Halmashauri zetu. Ninayo maoni kwamba, utaratibu huu wa kutoa fedha kwenye vikundi pengine hauwezi kuwa na ufanisi sana. Nilikuwa napendekeza, hivi sasa wako wananchi wengi binafsi wenye uwezo wa kuwa na mawazo ya biashara, wanaoweza kubuni mradi, na kadhalika, badala ya kuendelea kutoa fedha kwenye vikundi vya watu watano hadi kumi, tungeruhusu hizi fedha akopeshwe mtu mmoja mmoja ambaye ana wazo zuri la biashara. Ninaamini mtu mmoja mwenye wazo zuri la biashara anaweza kuajiri hata watu 100 kuliko watu kwenye vikundi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo historia katika nchi hii, hizi biashara za watu wengi zimeshindikana huko nyuma. Tulikuwa na mashamba ya vijiji, tulishindwa kuyaendesha; tulikuwa na matrekta ya vijiji, tulishindwa kuyaendesha. Biashara ya watu wengi ni ngumu sana kufuatilia. Kwa hiyo, napendekeza tubadili sheria, tuanze kutoa mikopo kwa mtu mmoja mmoja mwenye ujuzi au mwenye mradi mzuri ilimradi tu ana sifa za kupewa mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale mwanzo palikuwa na hofu kwamba, kuwafuatilia itakuwa ni vigumu. Dunia inakwenda mbele. Sasa hivi tupo kwenye mchakato wa kuandikisha anuani za makazi. Wananchi wetu wana vitambulisho vya *NIDA* vya Taifa. Watu hawa wanajulikana waliko, tuwaamini, tuwakopeshe waweze kufanya maendeleo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, atafuatiwa na Mheshimiwa Neema William Mgaya na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, ajiandae.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kukushukuru sana lakini kumshukuru sana Mungu kwa kuendelea kutupa afya njema. Bunge lako



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii ni awamu nyingine ya bajeti na nitumie nafasi hii kama wenzangu waliopita walivyokwisha sema, Wizara hii iko chini ya Mheshimiwa Rais tumpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ya kazi kubwa sana inayofanywa na wasaidizi wake. Nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake, lakini Katibu Mkuu pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Bunge lako kupitia Wizara hii kama itafanya kazi yake vizuri kwa namna inavyokwenda nina hakika hakuna Mbunge ndani ya Bunge hili atashindwa kurejea hapa kwa sababu hii ndiyo Wizara mama ambayo sote tunaitegemea. Kwa leo naomba nigusie maeneo mawili au matatu.

Mheshimiwa Spika, la kwanza ni eneo la *TARURA*. Nchi yetu ina barabara nyingi sana ambazo hazijajengwa kwa kiwango kinachostahili. *TARURA* wamebainisha zaidi ya kilomita 1,044,000 za kiwango cha vumbi ambazo zinatakiwa zijengwe kwa lami. Bajeti tuliyoiona safari hii tunashukuru kwamba imeongezeka kufikia angalau bilioni 800.

Mheshimiwa Spika, lakini ukienda Nyamagana peke yake tuna kilomita zaidi ya 944 ambazo hazijajengwa kwa kiwango cha lami na ni barabara mbaya kabisa. Sasa nadhani umefika wakati kwa Serikali iangalie vizuri Wizara hii ya TAMISEMI na taasisi hii ya *TARURA* kuhakikisha angalau tunakuwa na mpango wa miaka minne kuongeza fedha angalau zifikie angalau trilioni 1.3 mpaka trilioni 1.4. Kwa kufanya hivyo, ukitazama bajeti ya mwaka huu tumekusudia kujenga kilomita 411 peke yake za lami, lakini kuna miji ina zaidi ya kilomita hizo na mimi nishukuru sana kwa mpango wa *TACTIC*.

Mheshimiwa Spika, mpango wa *TACTIC* nafahamu uko kwenye Jiji lako la Mbeya lakini nafahamu uko kwenye Majiji ya Dodoma na maeneo mengine. Mradi huu ni sawa na mradi uliomalizika wa *TSP* ambao kiukweli umetuachia matokeo makubwa sana na nautarajia sana mradi huu,

Mheshimiwa Waziri amesema utaanza mwezi wa Saba baada ya bajeti, nami ninayo barabara ambayo itanufaika na mradi huu, barabara ya kutoka Buhongwa kwenda Rwanima-Kishiri kupita Fumagila mpaka Igoma, lakini barabara hii ni sambamba na ujenzi wa soko la mazao ya majini na nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, sasa hii ndiyo miradi ambayo inaweza ikatusaidia, kwanza kupunguza adha na kero kwa wananchi wetu kwa sababu Serikali inafanya mambo mengi mazuri, lakini kama hatutakuwa na barabara bora zenye sifa yote itakuwa ni kazi bure na huko ndiko wananchi wanakopata ghadhabu nyingi.

Kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na niishukuru sana Wizara yake na wasaidizi wake kwa kuliona hili na kusukuma fedha na makubaliano ya *TACTIC* yamefikia mwisho ili tuweze kuona sasa matokeo ya miradi hii.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo peke yake, nigusie jingine kwenye sekta ya afya. Tumejenga vituo vya afya vingi sana, tumejenga zahanati nyingi sana kabisa na rekodi ukianza mwaka 2017 awamu ya kwanza ilijenga vituo 44 ambavyo tunashukuru sana kwa sababu vyote vilipata vifaa tiba. Awamu ya Pili karibu 80%, hivi lakini awamu ya tatu na kuendelea vituo vingi sana havijapata vifaa tiba na kupelekea halmashauri zetu kulazimika kutafuta fedha kwa wadau na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia Jiji la Mwanza peke yake Nyamagana na niombe sana Wizara ukienda Igoma toka kimekamilika leo ukienda hakina vifaa vya msingi vinavyoweza kutoa huduma, ukienda Fumagila na kule Bulale, sasa haya ni maeneo ambayo tunadhani kwa mpango huu ambao Wizara imekuja nao leo.

Nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri wamefikiria vizuri kwa fedha walizozitenga kwa kuongeza kwenye vifaa tiba tufike wakati ikiwezekana bajeti ya ujenzi ipungue, irudi nusu ya tulipo sasa ili fedha nyingi tuielekeze kwenye vifaa.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu, nitoe mfano, mtu kwa mfano unaenda kwenye kituo kilichoko jirani yako karibu kilometa tano, unafika unaambiwa hatuwezi kukufanyia vipimo uende hospitali ya wilaya, unalazimika kutembea zaidi ya kilomita zingine saba, sasa kuna faida gani ya kuendelea kujenga wakati vituo vingi tulivyovijenga, zahanati na vituo vya afya havina vifaa tiba. Maana yake hapa ni kwamba hatujawasaidia wananchi. Nilikuwa naonegea na Daktari mmoja anasema kwa mfano ukiwa na kituo halafu hauna tu peke yake ile mashine ya *ultra sound*, tunataka kupunguza vifo vya mama na mtoto, kama hatuna kifaa hiki hatuna *state* ya wazazi kuja kujifungua, hatuna vitanda vya akinamama kujifungulia, bado itakuwa ni kazi bure hatutapambana na wimbi la vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niishukuru sana Wizara kwa kuja na mpango huu wa kuendelea kupunguza fedha kwenye ujenzi na kuongeza fedha nyingi zaidi kwenye kupeleka vifaa ili kila mtu na siyo Nyamagana peke yake, ukienda kule Mbeya kwa mfano kwenye hospitali yako ya Igawilo ambayo imepandishwa hadhi kwenda kwenye hospitali kutoka hospitali ya kawaida kama ilivyokuwa, ina majengo mazuri lakini haina vifaa sasa hivi. Ukienda Iyumbu vile vile kituo cha afya kizuri, lakini hakuna vifaa. Kwa hiyo haya maeneo yote haya ni lazima tuwekeze nguvu ukienda Magu kwa Kiswaga na kwingine kote maeneo mengi naamini, tumeona fedha kwa ajili ya kupeleka vifaa kwenye zahanati 300 na vituo vya afya 159, tunatamani sana tuone orodha hi ili tumshauri Mheshimiwa Waziri na tuhakikishe kila eneo limeguswa ili tuweze kuwa na maana nzuri hasa ya utekelezaji wa maeneo haya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ningependa sana nizungumzie habari ya machinga. Sisi tunaotoka kwenye miji mikubwa, sisi tunaotoka kwenye majiji na nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ameona juzi hapa kuna kitendo ambacho nashukuru Mungu sana alikiingilia haraka na sisi tukahakikisha kwamba haya siyo malengo ya Serikali, malengo ya Serikali ni kuwapanga wafanyabiashara kwenye maeneo mazuri, wafanye biashara ili waweze kujikwamua kutoka daraja moja

kwenda daraja lingine. Kwa hiyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Mkuu wangu wa Mkoa wa Mwanza kwa kuchukua haraka tukio la unyanyasaji la juzi ambalo lilikuwa siyo tukio zuri na naamini haya siyo malengo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu sasa tunafikiria kwamba katika maeneo haya yote tunayoenda nayo, maeneo mengi tu wafanyabiashara wamekubali kwenda kwenye maeneo yao. Kwa mfano, nimepata milioni 500 kwenye Jimbo langu hii peke yake haitoshi kuwafanyia kuwatengenezea wafanyabiashara mazingira bora ya kukaa na kufanya biashara.

Mheshimiwa Spika, naomba waweke kipaumbele kwenye miji mikubwa Jiji la Mwanza, Mbeya, Dodoma, Tanga, Arusha, kama tumeamua kuwapanga watu hawa itengwe fedha maalum ya kuhakikisha tunaboresha maeneo. Halmashauri zetu Mheshimiwa Waziri hazijitoshelezi kuweka fedha ya kukarabati miundombinu yote. Tusukume fedha kwa wingi tuwasaidie vijana ili tuwawekee mazingira. Wamekubali kutoka barabarani na wanafanya vizuri sana...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. STANLAUS S. MABULA:** ...hata hivyo tuwalinde kwa sababu ni vijana wa Taifa la leo na tunawategemea sana.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa muda na Mungu akubariki sana nafahamu changamoto za Jiji la Mwanza ndizo changamoto za Jiji la Mbeya, kwa hiyo tushirikiane kuhakikisha kwamba vijana wetu na ndugu zetu wanafanya kazi vizuri na kusaidiwa sana. Mungu akubariki sana na ahsante. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Stanslaus Ng'oma Mabula. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Neema William Mgaya atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza na Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya TAMISEMI. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikianza na *TARURA* tumeona kuna ongezeko kubwa la bajeti ya *TARURA*, ukilinganisha kuanzia mwaka 2020/2021 bajeti ya *TARURA* ilikuwa bilioni 275, ikaja 2021/2022 ikapanda mpaka bilioni 722 na hivi sasa tunavyozungumza bajeti ya *TARURA* 2022/2023 ni bilioni 802. Hi ni hatua kubwa sana ambayo itasaidia kuboresha barabara zetu za vijijii. Napenda kuwaambia *TARURA* Mkoa wa Njombe, sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe ni wazalishaji wazuri sana wa vyakula pamoja na zao la chai. Kwa kuwa tumekuwa na changamoto kubwa sana kwa wakulima wetu wa chai, chai kuharibika zinapotoka kule mashambani kwenda kwenye viwanda, zinafika zikiwa hazina ubora kutokana na changamoto za barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi naamini kwa bajeti hii na kwa mwendo huu mzuri wa Serikali ya Rais Samia kuhusiana na suala zima la kuboresha barabara zetu za vijijini, naamini sasa barabara hizi zitakwenda kuwa mkombozi wa chai zetu kutoharibika na kufika kwa ubora na wakulima wetu wa chai wataweza kupata pesa nzuri wanapokwenda kuuza kule viwandani. Ushauri wangu kwa *TARURA* Njombe ni wakati sasa wa kufanya *survey* za barabara zetu mapema ili barabara zetu za vijijini ziweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie suala la afya ya msingi. Katika suala la afya ya msingi nimeona kwenye bajeti ya TAMISEMI wanaendelea kukamilisha ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali zetu, lakini sambamba na kupeleka vifaa tiba katika hospitali, zahanati na vituo vya

afya ambavyo vimekamilika. Ni jambo zuri ni kazi nzuri wanayoifanya, lakini ushauri wangu nawaomba kuna changamoto kubwa sana ya wauguzi kwenye vituo vyetu vya afya, kwenye hospitali zetu, kwenye zahanati zetu na Mkoa wa Njombe kwa kweli tatizo hili limekuwa ni kubwa mno kwa Majimbo yetu yote sita ndani ya Mkoa wa Njombe na hata ukizungumza na baadhi ya Wabunge kwenye mikoa yao bado changamoto ya wauguzi ni kubwa sana. Kwa hiyo naiomba Serikali wajikite katika kuhakikisha kwamba wanamaliza tatizo la wauguzi, wakae pamoja na Wizara ya Utumishi ili waone namna gani wanaweza kuongeza wauguzi katika zahanati zetu, vituo vya afya na hospitali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niende kwenye elimu msingi; katika elimu msingi nataka nizungumzie masuala ya majengo, Walimu na wanafunzi na niseme jamani, kusema ukweli katika suala la majengo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameupiga mwingi. Ndani ya mwaka mmoja amejenga madarasa 15,000, madarasa 3,000 kwa ajili ya elimu ya awali na hii imesaidia watoto wetu wale walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kufuata elimu sasa changamoto hii imekwenda kwisha.

Mheshimiwa Spika, vile vile tulikuwa na changamoto watoto hapa walikuwa wanaenda *second selection* madarasa 12,000 yamejengwa ajili ya shule za sekondari. Kwa kweli Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan anahitaji pongezi nyingi sana haijapata kutokea ndani ya mwaka mmoja Serikali kujenga madarasa 15,000. Ushauri wangu sasa pamoja na kuwa tumejenga madarasa mengi 15,000 ndani ya muda mfupi, naiomba Serikali sasa iangalie umuhimu wa kuongeza walimu wa sayansi. Walimu wa sayansi ni changamoto sana kwenye shule zetu. Nashukuru juzi nimeona Waziri wa Utumishi ametoa kibali kwa ajili ya kuajiri Walimu naomba sasa Wizara hii ya TAMISEMI ikae na Wizara ya Utumishi ione namna ya kutoa kipaumbele kwa Walimu wa sayansi. Ukizingatia sasa hivi ulimwengu wetu huu ni ulimwengu wa sayansi tujitahidi tuajiri Walimu wa sayansi ili kusudi watoto wetu tuwaandae vizuri katika kukabiliana na ulimwengu huu wa sayansi.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri kuna salamu zake kutoka Kata ya Igwachanya kwa Mheshimiwa Diwani Mawata. Tarehe 22 mwezi wa kwanza mwaka 2022 alienda pale shuleni, kuna changamoto ya bwalo. Bwalo lile limeanza kujengwa tangu mwaka 2012 kwa nguvu za wananchi pamoja na Serikali wameshajenga *foundation* wameweka na nguzo. Vile vile Mheshimiwa Jafo alipita pale mwaka 2020, akaahidi kwamba watawapa milioni 100 mpaka leo hawajawapa na kukamilisha ujenzi ule wa bwalo lile inahitaji milioni 275 tu, kwa nyie watu wa Kagera ni hela ya mboga tu. Naomba wajitahidi wapeleke pesa ili kusudi bwalo lile likamilike na Mheshimiwa Diwani aamini kweli alinituma na salamu zimefika.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaomba sana pamoja na bima za afya ambazo wametoa kwa Madiwani lakini bado kuna umuhimu wa kuwaongezea posho Madiwani hawa kutokana na kazi kubwa wanayoifanya. Niwaombe sana sana katika hili.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, nilisahau kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa zile bilioni 1.5, kila Jimbo la mkoa wa Njombe za *TARURA* tulizipata, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mzava na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magesa ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa kupata nafasi ili niweze kutoa mchango wangu. Kwanza nianze kwa kupongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya. Vilevile kipekee kabisa nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba anawapatia maendeleo Watanzania. Nimpongeze sana kwa kampeni yake ambayo ameanza ya kuwapanga wamachinga ili

waweze kupata maeneo bora kwa ajili ya kuweza kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze pia wewe mwenyewe binafsi pamoja na Bunge lako. Wewe na Bunge lako mmekuwa mstari wa mbele sana katika kuhakikisha kwamba mnasimamia masuala ya usawa wa kijinsia ndani ya Bunge. Bunge lako linazo Kamati mbalimbali na katika hizo Kamati pamoja na Wabunge mbalimbali hakuna Kamati hata moja ambayo Mbunge wa Viti Maalum anazuiliwa kuingia ndani ya Bunge hili. Wabunge wa Viti Maalum wanaingia mpaka kwenye Kamati ya Bajeti, lakini katika hali ya kusikitisha iko shida kubwa sana katika halmashauri zetu Wabunge wa Viti Maalum tunakatazwa kuingia kwenye Kamati ya Fedha. Kamati ambayo ndiyo inapanga mipango yote ya maendeleo ya halmashauri zetu, Kamati ambayo ndiyo inayopanga hata zile asilimia 10, kwa maana nne kwa ajili ya akinamama, nne kwa ajili ya vijana, lakini asilimia mbili kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, hali hiyo inasikitisha sana na sisi kama Wabunge na nakumbuka kwa sababu mimi ni Mbunge wa kipindi cha pili sasa, tumekuwa tukizungumza sana hata Bunge lililopita tuliongea, lakini mpaka sasa hivi hakuna ambalo limefanyika.

Mheshimiwa Spika, kazi nzuri na kazi kubwa ya Mbunge ni kusimamia maslahi ya watu anaowaongoza. Kwa hiyo na sisi Wabunge wa Viti Maalum tumeaminiwa na wanawake wa mkoa yetu. Mimi Shonza ni Mbunge wa kipindi cha pili, nimeaminiwa na wanawake wa Mkoa wangu wa Songwe ili niwasimamie maslahi yao na namna ya kusimamia maslahi yao ni Bungeni na kule kwenye halmashauri zetu, ambapo huko ukiingia Mbunge wa Viti Maalum wanasema kwamba sheria inakataza Mbunge wa Viti Maalum kuweza kuwa mjumbe wa Kamati ya Fedha. Sasa matokeo yake fedha hizo ambazo zinatolewa ni nyingi lakini fedha hizo zimekuwa hazirejeshwi. Aliongea hapa juzi Mheshimiwa Festo kwa uchungu mkubwa sana, fedha zinazotolewa ni nyingi lakini shida ipo kwenye marejesho, kwa



sababu sisi ambao ndiyo viongozi ambao tunakaa na hao watu tunajua changamoto zao...

**SPIKA:** Mheshimiwa Shonza, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Leah Komanya.

## **T A A R I F A**

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa hata kwenye kukabidhi fedha hizi katika mkoa mmoja sehemu moja anakabidhi Mkuu wa Mkoa sehemu moja anakabidhi Mbunge, kwa hiyo kunakuwa na *double standard* lakini makundi yale ya jamii hayashirikishwi katika ule mwongozo uliopewa, kazi hii tungeachiwa Wabunge kwa sababu tunawajua wananchi ili vijiji vyote viweze kutendewa inavyotakiwa.

**SPIKA:** Ilipaswa kuwa taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge lakini naona Mheshimiwa Leah Komanya ameamua kuchangia ameamua kuchangia.

Waheshimiwa Wabunge hoja hiyo huwa inakuja na kuondoka, inakuja na kuondoka, lakini nafikiri ni muhimu Wabunge wanawake kwa sababu Wabunge wanawake wako wa Viti Maalum na wapo na wa Majimbo, pengine sisi tukikutana tukiliweka sawa linaweza likaleti tija. Kwa nini nasema hivyo kwa sababu mimi ni Mbunge wa Jimbo na Mbunge wa Viti Maalum unawakilisha halmashauri zote kwenye mkoa wako na wewe huwezi kuwa mjumbe wa Kamati ya Fedha kwenye halmashauri zote. Kwa hivyo ndiyo maana nasema lazima tukalizungumze mahali kwa sababu Mbunge atakuwa mmoja tu na maana yake kama unataka kuingia Kamati ya Fedha utaingia kamati ya Jimbo moja tu. Kwa hiyo hayo...

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Hapana, msiitikie tu ndiyo kwa sababu nilikuwa naangalia nani wanaopiga makofi, si niko hapa mbele. Ndiyo maana nimesema ni muhimu wanawake tukakae,

tukajadiliane kule, kwa sababu wa Majimbo wapo na wa Viti Maalum wapo, tutaweza kushauriana vizuri kuhusu jambo hili kuliko kufikiri pengine kwamba ni jambo rahisi, ndiyo maana nasema kwa sababu huwa linakuja na kuondoka, kila bajeti inapokuja hapa ya TAMISEMI jambo hili linazungumzwa na halifanyiwi maamuzi, kwa nini mnafikiri halifanyiwi maamuzi? Ni kwa sababu ziko changamoto ambazo ni lazima tuziungumze.

Mheshimiwa Juliana Shonza, endelea na mchango wako kwa sababu Mheshimiwa Leah Komanya naona aliamua kuchangia badala ya kukupa taarifa. Ahsante sana.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Niseme kwamba nakubaliana kabisa na taarifa ambayo amenipa na maelezo ambayo umeyatoa.

Mheshimiwa Spika, changamoto imekuwa kubwa kwa sababu fedha hizi kama ambavyo nimesema, huwa hazirejeshwi, kwa sababu hakuna *intervention* ya Wabunge kwenye kusimamia hizi fedha. Nitatoa mfano mmoja. Kwenye Jimbo la Tunduma ambalo anatoka Mheshimiwa David Silinde, Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuwa akizisimamia hizi fedha na tumeona juzi alitoa fedha nyingi sana; alitoa bodaboda, akatoa bajaji akatoa na zaidi ya shilingi milioni 300 kwa ajili ya kusaidia makundi ambayo yapo kwenye Mkoa wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto kwenye Halmashauri nyingine na Majimbo mengine Wabunge hawashirikishwi. Nami kama Mbunge wa Viti Maalum, nilipigiwa simu na nikaambiwa kumbe ni kweli hizi fedha huwa zipo. Kwa sababu wengine wanaona kama ni historia, ni kitu ambacho hakipo, kumbe ni fedha ambazo zipo na Serikali inafanya kazi kubwa sana kutoa hizi fedha, lakini changamoto ni kwamba *intervention* ya Wabunge hakuna. Kwa hiyo, tumeona kwamba maeneo ambayo yamepata fedha hizi na kuna *intervention* ya Mbunge, mafanikio ni makubwa sana. Nampongeza Mheshimiwa David Silinde kwa sababu ni Waziri

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hawezi kusema, lakini mimi kama Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wake, ninampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kwamba hizi fedha haziendi kwa wahusika, yaani unakuta kuna watu wanapata fedha lakini hawana vigezo vya kupata hiyo mikopo. Pia kuna maeneo mengine Wilaya moja ina vijiji 100, lakini kwenye kuzigawa hizi fedha utashangaa mgao ni shilingi milioni 100. Shilingi milioni 50 yote inakwenda kwenye Kijiji kimoja, kwenye kikundi kimoja. Kwa hiyo, bado unakuta kuna *double standard* kwenye kugawa hizi fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema, kwa kweli wakati umefika, sisi kama Wabunge tukae, tujadili. Hili suala naomba lifike mwisho ili sisi Wabunge, wakiwepo Wabunge wa Viti Maalum wanawake, Wabunge wanaowakilisha Vijana na wa Majimbo, sisi ndio tuwe wasimamizi wa huu mfuko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa nijikite kwenye kutoa ushauri kwa Serikali. Kwa kuwa Wabunge kwa miaka mingi tumekuwa tukilalamika juu ya suala la Wabunge kutokuingia kwenye Kamati ya Fedha, naomba sasa, kwa sababu Mawaziri wapo hapa na wanatusikia, ni wakati muafaka sasa hili suala lifike mwisho, mtoe miongozo. Kama ni suala la kikanuni, basi hizo kanuni ziletwe humu ndani ya Bunge zibadilishwe; na tukishabadilisha humu ndani ya Bunge, hiyo miongozo ichukuliwe ipelekwe kule kwenye Halmashauri zetu ili tuweze kuondoa hii changamoto. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili; kwa kuwa kumekuwa na changamoto kubwa sana kwamba sisi Wabunge Viti Maalum hatuna Mfuko wa Jimbo, Wabunge wa Viti Maalum vile vile hatuna miradi yoyote ambayo tunasimamia kwenye Halmashauri zetu; ukiwa Mbunge wa Viti Maalum, huwezi ukasema hata uende kukagua hospitali, haiwezekani. Utaulizwa, umekuja kukagua kama nani? Kwa hiyo, hatuna kazi *specific* ambayo Wabunge Viti Maalum tunapewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka nitoe ushauri kwa Serikali, ninaamini kwamba Serikali inatusikia; naomba Serikali, ikiwezekana hii asilimia nne kwa ajili ya akina mama isimamiwe na Wabunge wa Viti Maalum. Kwa sababu ilivyo sasa hivi, asilimia nne kwenye hicho kikao, tena ikiwezekana iwe ni Mfuko wa Jimbo, kama ambavyo Wabunge wa Majimbo wana Mfuko ya Jimbo, nasi asilimia nne hii iwe ndiyo Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya Wanawake. Kwa sababu sisi ndio tunajua changamoto za wanawake, tunajua makundi gani ambayo yanapaswa kupatiwa mikopo na tunajua makundi gani ambayo hayana sifa. Kwenye hiyo Kamati, Mwenyekiti wake awe ni Mbunge wa Wanawake ili aweze kuisimamia vizuri hiyo asilimia nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe unafahamu, kwenye chaguzi zetu huwezi kuwa Mbunge wa Wanawake kama siku ya uchaguzi hujajipanga vizuri kwenda kuwaeleza wanawake utawasaidiaje waweze kupata mikopo ya asilimia nne? Kwa hiyo, huwa tunaongea tunawaambiwa wanawake, lakini kimsingi hatuna *instrument* ya kuweza kuwasaidia waweze kupata hii mikopo. Malalamiko yamekuwa mengi, kikundi kina sifa zote, kinaomba mikopo zaidi ya miaka mitano, miaka kumi, hakipati, lakini vikundi vingine ambavyo havina sifa vinapata mkopo. Hii ndiyo sababu ambayo inapelekea hata marejesho yake yanakuwa ya kusuasua sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa mwisho kwa Serikali; naomba, kwa sababu tumeshuhudia sasa hivi Mheshimiwa Rais, Mama yetu Samia Suluhu Hassan ameanzisha kampeni nzuri sana ya kuwapanga Machinga ili waweze kupata maeneo mazuri, wafanye wafanye biashara zao kwa amani ili hizi fedha ambazo zinakopeshwa kwa Machinga ziweze kurejeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashauri, kwa sababu Halmashauri inatenga 10%, naomba Serikali iangalie uwezekano wa *ku-top up* angalau 3% kwenye ile 10% ambayo inatengwa na Halmashauri ili hiyo 3% iende ikaboreshe miundombinu kule kwa wafanyabiashara kwenye kujenga masoko, kujenga

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

viwanda, ili Serikali inapotoa fedha kuweza kuwakopesha, basi hawa vijana, akina mama na watu ambao wana makundi maalum, waweze kuwa na sehemu ya kuzifanyika hizi kazi. Nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juliana Shonza. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa na Mheshimiwa Tunza Malapo, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Awali kabisa, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, ambaye ametujalia uzima, ametuwezesha kuwa pamoja humu kuifanya kazi hii nzuri ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ndiye msimamizi wa Wizara hii, maana ni Wizara iliyo chini ya Ofisi yake kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwa nchi yetu na kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza sana Ndugu yangu Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa TAMISEMI, na Manaibu wao kwa kuendelea kuaminiwa. Naamini kazi hii ataifanya vizuri, ana timu nzuri TAMISEMI. Nampongeza pia Katibu Mkuu, Profesa Shemdoe na timu yake ya Manaibu Katibu Wakuu, wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nitumie nafasi hii kutoa mchango wangu kwenye maeneo machache. Eneo la kwanza ni miundombinu ya barabara vijijini. Hapa naizungumzia *TARURA*. Kipekee kabisa, naipongeza sana Serikali kwa kazi nzuri tuliyoifanya ya kuongeza fedha kwa ajili ya kushughulikia barabara za vijijini. Nikitoa mfano, kule Korogwe tulikuwa na bajeti ya shilingi 670,000,000 kwa miaka kama mitatu mfululizo, lakini kwa

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwaka wa fedha tuliokuwa nao, tumepokea zaidi ya shilingi 1,400,000,000/= kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini, pia tumepokea shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa daraja kubwa kule Mswaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, kwenye fedha hizi namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali kutoa zile shilingi 500,000,000 za Jimbo kupitia kwa Wabunge kwenda kufanya matengenezo ya barabara. Kwa kweli *TARURA* wamejitahidi kufanya kazi nzuri. Pamoja na kujitahidi kufanya kazi nzuri, yapo maeneo manne naomba nishauri. Eneo la kwanza, pamoja na kuwa fedha zimeongezwa, lakini ukweli ni kwamba bado mahitaji ya fedha kwa ajili ya barabara za vijijini ni makubwa. Naiomba Serikali iendelee kuangalia namna ya kuongeza bajeti kwa ajili ya *TARURA* ili waendelee kupata fedha nyingi zaidi kufanya miradi mingi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili tuwaombe *TARURA*, Serikali imekubali kuongeza fedha, na kama Wabunge tunaendelea kuomba fedha iongezwe zaidi; tujitahidi kubuni na kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi ya hizi fedha ili kazi inayofanywa kwa fedha hizi iwe na thamani halisi ya fedha ambayo imetolewa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni la teknolojia. Wakati fulani tumemsikia Mheshimiwa Rais akishauri kwamba kuna teknolojia nzuri iliwahi kuja hapa lakini haikuwahi kufanya kazi, ikaenda maeneo mengine. Ni kweli tunatoa fedha nyingi tunatengeneza barabara na kukarabati, lakini ukweli ni kwamba barabara zetu za vijijini, wanamaliza kutengeneza, ikinyesha mvua ya siku moja, barabara hazipitiki tena. Ni lazima kama nchi tufikirie teknolojia nyingine sahihi zaidi itakayosaidia matengenezo yanayofanywa kwenye barabara zetu yaweze kukaa muda mrefu na wananchi wetu wanufaike na matunda ya kazi hii nzuri iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne na la mwisho la kushauri kwenye *TARURA*, tumeona iko miradi mingi ya barabara inafanyika kwa maeneo ya mijini hasa kwenye

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maeneo ya Makao Makuu ya Halmashauri ambazo ni za Miji na Manispaa. Maeneo yetu sisi tunaotoka maeneo ya vijijini, tunayo miji ambayo pia ni *centre* kubwa na nzuri za kibiashara, tuwaombe TAMISEMI kuwaomba *TARURA*, fikirieni namna ya kuwa na maandiko ya kutafuta fedha kwa ajili ya maeneo haya. Siyo maeneo haya tu peke yake, nimeona kwenye bajeti mnaendelea kuzungumzia kuhusu miradi maalum ya maeneo yale ya uzalishaji, na sehemu kubwa nimeona mnazungumzia eneo moja tu la kule nyanda za juu Kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Handeni, Korogwe na Muheza ndiyo zinaongoza kwa kilimo cha Mkonge. Leo tunavyozungumza, moja ya changamoto kubwa wanayopata wanachi wetu na wakulima wadogo wadogo wa Mkonge, ni miundombinu ya kutoa mkonge kutoka mashambani kupeleka kwenye viwanda vya kuchakata. Pia eneo la Lushoto na eneo la milimani la Korogwe kuna kilimo kikubwa sana cha chai, lakini kwa muda mrefu tumesahaulika. Tunaomba *TARURA* ije na miradi ya namna hii pia kwenye maeneo ya mkonge na maeneo ya chai ili tusaidie kuongeza thamani ya mazao ya wananchi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni Afya. Tunaishukuru Serikali imefanya kazi nzuri kwenye eneo la ujenzi wa vituo vya afya na pia kwenye kukamilisha maboma ya Zahanati. Nimemsikia ndugu yangu, Mheshimiwa Mabula hapa amesema tuendeleo kupunguza bajeti ya ujenzi. Mimi nasema mwendeleo kupunguza bajeti ya Ujenzi lakini kwa wale wa mjini kama Nyamagama.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi wa vijijini kama Korogwe, miundombinu ni muhimu na vifaa tiba ni muhimu na vyote hivyo ni lazima viende kwa pamoja. Leo ninapozungumza Korogwe vijijini, nina maboma zaidi ya 24 ambayo...

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa,

**SPIKA:** Mheshimiwa Mnzava kuna taarifa kutoka kwa Mbunge wa Nyamagana, Mwanza Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

## **T A A R I F A**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa mzungumzaji ya kwamba hoja ya kupunguza ujenzi haimaanini kuacha ujenzi. Kwa hiyo, kama Korogwe wana uhitaji zaidi wa ujenzi, watajengewa, lakini hoja yangu ya msingi ni kwamba ujenzi uambatane na vifaa zaidi. Sasa sijui kama yeye anaiona hiyo haifai au inafaa, ataichukua. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mnzava, unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, naipokea na ninajua imemsaidia na yeye kufafanua jambo hili kwa wapiga kura wake kule, sasa wamemwelewa. Mwanzoni hawakuwa wamemwelewa, ndiyo maana nimesema, ujenzi huu uendane na vifaa tiba. Vifaa tiba ni muhimu na ujenzi ni muhimu. Nimesema, kwa mfano Korogwe Vijijini, nina maboma sasa hivi zaidi ya 24 ya Zahanati ambayo yanahitaji kukamilishwa ili wananchi wetu waweze kupata huduma. Ukiwaambia wananchi unaacha, unaweka nguvu kwenye vifaa tiba, tunawavunja moyo. Mambo haya yaende kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais, pamoja na Sera na Ilani kusema tuwe na Kituo cha Afya kwenye kila Kata, tuwe na Zahanati kwenye kila Kijiji, utekelezaji wake ulionekana ni mgumu. Alipoingia Mheshimiwa Rais, Mama Samia, amesema angalau tujihakikishie kila Tarafa kuwa na Kituo cha Afya. Nasi tunashukuru, Tarafa yetu ya Korogwe ambayo ilikuwa haina kituo cha Afya hata kimoja, imepata Kituo cha Afya cha Mnyuzi, shilingi milioni 500, tunaishukuru Serikali. Naiomba sana TAMISEMI, tusimchonganishe Mheshimiwa Rais na wananchi wake. Nikitoa mfano wa Korogwe, nina Tarafa nne; Tarafa



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

moja ya Bungwi ina Kata tisa; ina Kituo cha Afya kimoja; hawajapata kituo afya kingine kwa sababu tayari wana kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, lakini kituo hicho walichokuwanacho, hata *operation* hakifanyi. Huduma za upasuaji hakuna, ni cha muda mrefu, ni kikongwe na chakakavu. Kuna kituo cha Afya cha Magoma. Pamoja na miradi hii ya vituo vya afya tuliyokuwa nayo ya kila Tarafa na inavyoendelea, tunaomba sana, vituo vya afya za zamani, vikongwe na vichakavu, viboreshwe ili wananchi wetu waweze kupata huduma. Kwenye hili la Vituo vya Afya, siyo tu majengo, pamoja na hivyo vifaa tiba, lakini tuna changamoto kubwa sana ya watumishi kwenye sekta ya afya na kwenye sekta ya elimu. Tunawaomba sana TAMISEMI tulingalie hili kwa uzito wake liweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni la usimamizi wa Serikali za Mitaa. Tunaendelea kusema, Wabunge wote ni mashahidi, muda tunaotumia Majimboni ni mdogo sana, muda mwingi tupo kwenye vikao vya Bunge karibu nusu ya mwaka, tupo huku Bungeni. Wanaotusaidia kufanya kazi vizuri ni Waheshimiwa Madiwani. Naiomba Serikali, tuangalie namna ya kuboresha maslahi ya Madiwani wetu. Fedha wanayopata, kiwango cha posho yao ni kidogo na kimekaa kwa muda mrefu. Tuna Madiwani karibu 4,500; Serikali ikiamua kutenga shilingi bilioni 30 kwa mwaka, tunawaongezea nguvu hawa Madiwani wanafanya kazi yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia na Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa, naomba nao tuangalie namna ya kuweza kuwaongezea uwezo waweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tumaini Bryceson Magessa, atafuatiwa na Mheshimiwa Tunza Issa Malapo na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ajiandae.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Vile vile namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa nafasi ambayo amenipatia leo kuweza kuzungumza ndani ya Bunge hili tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hoja yangu kubwa ni kujikita kwenye Elimu ya Msingi, lakini napenda kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kupitia Waziri wa TAMISEMI na Manaibu Waziri wawili, wataalam ambao tumejumuka pamoja nao hapa kwa kazi kubwa ambayo wanafanya.

Mheshimiwa Spika, nimepitia hotuba hii, ni dhahiri kwamba katika ukurasa namba 12 na 13 ni lazima tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa aliyofanya kwa kutupatia fedha katika Mpango wa Maendeo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO 19. Jimbo letu la Busanda lilipata takribani madarasa 209 ambayo yana thamani ya shilingi bilioni 4.2. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kupitia Wizara hii kwamba tuna madarasa ya kutosha Sekondari na sasa wanafunzi wanaendelea kusoma. Vile vile nampongeza Mheshimiwa Rais kupitia Wizara hii, ametupatia fedha kupitia *TARURA* zaidi ya shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya barabara. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niseme wazi kwamba Wizara hii inafanya kazi kubwa na nimeona kwenye mpango kwamba fedha mwaka huu imeongezwa. Ninaamini barabara zitaendelea kujengwa vizuri kuliko ilivyofanyika mwanzo, lakini niombe sasa tuna miji yetu midogo, kwa mfano, Mji wa Katoro barabara zake nyingi hazipitiki. Naomba *TARURA* walichukue hili na Manaibu Waziri wote wawili wamekuja Katoro, Mawaziri amepita Katoro, ameona hali halisi iliyopo, kwamba mji ule haupitiki. Tuna shilingi 600,000,000/= ambayo ilikuwepo kutoka ardhi mji unaanza kupangwa. Tunaomba ujengwe na barabara zake zipitike ili mji uweze kuonekana ni mji mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa namba 15 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri unaonesha wazi kwamba kuna vituo vya afya 304 ambavyo vimejengwa na vinaendelea kujengwa,

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lakini 234 vinatokana na tozo. Tulipendekeza mwaka 2021, vituo vya kimkakati kutoka kwenye Kata zetu, mimi binafsi kwa maana ya Busanda nilipendekeza Rwamgasa, Nyakagomba na Magenge, lakini sijaviona kama vimejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na pongezi kubwa ya kazi kubwa ambayo mnafanya, vituo hivi vya kimkakati viangaliwe kwenye maeneo yetu kutokana na jioografia. Jimbo letu la Busanda ni kubwa, nategemea kwamba mkitupatia vituo vya afya ambavyo tumevisema tutakuwa kwenye mazingira ya kuweza kuhudumia wananchi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu ya msingi ambayo nilisema nataka niizungumzie, mahali popote ambapo msingi unakuwa na mashaka, ni lazima ujenzi kwenda juu, nyumba hiyo itakuwa inayumba. Elimu ya msingi ndani ya nchi hii ambayo ninaamini kwamba inasimamiwa na Wizara hii ina changamoto nyingi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya elimu ya msingi Tanzania, ukipita kwenye shule za msingi utagundua mambo yafuatayo: wanafunzi ni wengi lakini madarasa ni machache. Hotuba hii inatuonesha wazi kwamba mwaka 2021 tulipanga kudahili wanafunzi kama 1,272,513 lakini tulidahili zaidi ya hapo na mwaka uliofuata ambao ni mwaka huu, tumedaili zaidi tuna asilimia 103; shule za msingi mwaka 2021 tulidahili vile vile zaidi ya asilimia 102, mwaka huu tumedahili kwa asilimia 108. Maana yake hata malengo tunayoyaweka, tunazidi, wanafunzi ni wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwenye shule zetu za msingi ambazo tunategemea ziwe zimeandaliwa vizuri sana, kwa sababu kama hazijaandaliwa vizuri, hao walimu wanaokuja Sekondari watakuwa na kazi kubwa sana ya kushughulika na hao wanafunzi, kwa sababu wanatoka wakiwa hawana msingi wa kutosha. Kwa mfano, Jimboni kwangu kuna shule inaitwa Bwawani, ina wanafunzi 3,100 lakini ina vyumba vya madarasa sita. Sasa ukijuliza, tunataka

kuendesha shule, tunaiendesha shule hii? Kwamba tuna wanafunzi 301, lakini madarasa yapo sita.

Mheshimiwa Spika, tuna shule nyingine inaitwa Ibwezamagigo, ina wanafunzi 3,111, nayo ina madarasa sita. Tuna shule nyingine inaitwa Mchongomani, ina madarasa tisa lakini ina wanafunzi 3,319. Ukifikiria tu unaweza ukajua kama hapo ndipo tunapotaka kuwaandaa wanafunzi kwa maana ya msingi; tutakuwa tuna changamoto kubwa. Tutawachukua wanafunzi wengi watakaoenda kwenye Kidato cha Kwanza lakini watakuwa wana kasoro nyingi kwa sababu ya uhalisia huu ambao unaonekana huku chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni ombi langu kwa maana ya nchi hii, huu ni mfano mdogo tu; ina maana tukiwauliza Wabunge wengi hapa kwenye maeneo yao, watagundua kabisa hakuna madawati ya kutosha, tutagundua kwamba hakuna vyumba vya madarasa vya kutosha. Hii elimu ya msingi sasa Serikali ijikite hapa, kama ilivyofanya kazi kwa Sekondari, iende sasa elimu ya msingi kuhakikisha kwamba tunaweza kuboresha, kwa sababu pamoja na madarasa kuwa machache, lakini hata walimu huko kwenye shule za msingi nao bado hawatoshi. Pamoja na kwamba tunaona sasa hivi imetangaziwa walimu wanatakiwa kuongezeka, lakini walimu hata wakiongezeka bado walimu watakuwa hawatoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali, kama kuna kitu sasa tunatakiwa kufanya, tujitahidi sana kuboresha elimu ya msingi ili msingi ukiwa bora, watoto wetu wanaokwenda juu, waende wakiwa na msingi ulio bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa leo niishie hapa. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, atafuatiwa na Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, ajiandae.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ya TAMISEMI ndio ina jukumu kubwa sana katika ustawi wa maisha ya wananchi kwa kwa sababu ndio inagusa moja kwa moja kila kitu ambacho kinafanyika kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la fedha kutengwa na fedha kwenda na zikishakwenda kule kwenye halmashauri zetu, zile fedha zinatumiwa sawasawa? Hiyo ndiyo hoja ya msingi. Kodi ya wananchi ambayo inakwenda kule tunataraji iendee ikatekeleze miradi ya maendeleo yenye tija kwa wananchi swali la kujiuliza je, zile fedha zikifika kule, zinafanya lile ambalo limekusudiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma ripoti ya CAG hii aliyoiwasilisha juzi kwenye miradi ya maendeleo ukurasa wa 137 CAG anasema kumefanyika uwekezaji wa bilioni 533.68 ambao hauna tija. Uwekezaji huu umefanyika kwenye mambo gani? Uwekezaji huu umefanyika kwenye ujenzi wa masoko, kwenye ujenzi wa vituo vya mabasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakutolea mfano mdogo kule kwetu Mtwara, kuna soko limejengwa linaitwa Soko la Chuno, limejengwa kwa kodi ya Watanzania bilioni 5.5. Kwanza katika hali ya kawaida, unaweza kujiuliza huyo mtu ambaye alikuwa amependekeza lile soko lijengwe kule alikuwa anawaza kitu gani? Ni tofauti na uelekeo wa watu wanakoelekea, watu wanaokaa kule ni wachache, kwa sababu sisi Watanzania tumezoea, unatamani sokoni unatoka kwenye shughuli zako *you just go there* una-*pick* unaondoka. Sasa kama amekujengea tofauti na uelekeo wa watu wengi wanaokaa unategemea hilo soko wateja wake wanatokea wapi? Maana yake nini bilioni 5.5, zimelala pale, hazina tija. *(Makofi)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo kuna taarifa kwa Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru napenda kumpa taarifa mzungumzaji, kwamba changamoto iliyoko Mtwara haina tofauti na changamoto ya Jiji la Dodoma. Soko limejengwa Nzuguni, lakini ukiangalia kata nyingi zilizoko zipo upande huu wa magharibi, kwa hiyo, uwekezaji unaofanywa na Serikali na wataalam wetu wanao-*design* miradi hii wamekuwa wakipoteza kodi kubwa za Watanzania pasipokuwa na tija. Nakushukuru ilikuwa atambue tu hilo Mheshimiwa mchangiaji anayeendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili. Serikali inachotakiwa kufanya ni kujitathmini kwa sababu hizi ni kodi za wananchi, tunataraji ziende zikawekeze kwenye miradi ambayo ina tija. Kabla Serikali haijapeleka fedha nyingi kiasi hicho, ifanye tathmini hapa tunapokwenda kuwekeza uwekezaji huu utaleta tija. Hilo ni suala la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la pili, tukienda kusoma ripoti ya *CAG* hii mpya siyo kwamba kila mwaka hakuna ubadhirifu, lakini hii nayo imesheheni kwa ubadhirifu. Kila ukienda kwenye halmashauri shida ni watu wanapiga fedha, maana yake ni nini? Wizara inatakiwa ijitathimini ina Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, waende wakafuatilie fedha zinazopelekwa. Nikupe mfano mwingine mdogo, nili-*take time* nikasoma, kule kwetu Mtwara kulikuwa na mradi wa kufunga taa za barabarani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye mkataba, nakupa mfano mdogo, kwenye ripoti ya maendeleo ukurasa wa 54, ripoti ya *CAG*, malipo ya ziada ya taa za barabarani Mtwara hiyo Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani; taa moja ilitakiwa ilipwe milioni 7.5, taa moja imeendwa kulipwa milioni

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

18,142,000, hata kama ni tofauti kwamba bei imeongezeka, bei imepanda kutoka milioni saba mpaka milioni 18.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo fedha zimepotea shilingi milioni 588, si zinajenga kituo cha afya kabisa hizi, kwa sababu kituo cha afya kilikuwa kinajengwa kwa shilingi milioni 450 mpaka 500, hizi mtu kalipwa tu kwa matakwa ya watu wachache. Ndio maana nimesema pamoja na hizo fedha kidogo ambazo zinakwenda, wao kama Wizara wana kazi kubwa sana ya kufuatilia kuhakikisha fedha zinazokwenda kule zinaleta tija kwa wananchi. Naambiwa Mawaziri vijana, maana yake vijana tunatambua mchakachaka, wanapaswa wakimbie. Kama walikuwa wanakimbia kwa *speed* mia moja, inatakiwa waende mia moja ishirini, mia moja hamsini. Hali huko, chini sio shwari sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee *issue* ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; kwa mwaka huu wa fedha hii bajeti tunayokwenda kuipitisha, sina uhakika kama itapita, hii bajeti ambayo tunaijadili sasa hivi kwa makusanyo ya ndani asilimia 10 ikitengwa kwenye halmashauri ni bilioni 75.98 zinatakiwa ziende kule kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hoja ni kwamba, Wizara inatakiwa ifanye tathmini, je, hizi fedha nyingi zinazokwenda kule, kweli zinabadilisha maisha ya wananchi hawa? Tusiseme tu zinatengwa, zinaenda na zingine, hazirudi, zinakwamia wapi? Wakati tuko kwenye Kamati kwa sababu ni mjumbe wa Kamati hiyo wakati tupo kwenye Kamati tumemweleza mengi, waende wakafanye utaratibu wa kuhakikisha fedha hizi zinakwenda kuleta tija, zile ambazo hazieleweki, ziliko zirudi kwa sababu zote walipewa watu hazikupotea angani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda nina suala moja, vitu huko mtaani vimepanda bei. Naomba Serikali ifanye tathmini, sasa hivi ndio wa wale wachumi wetu, wale maprofesa wa uchumi waliopo Tanzania watuambie hivi mafuta, kwa mfano, mafuta ya *petrol* yameongezeka labda

kwa shilingi 500 mpaka 800 ndio inahalalisha mafuta ya kula leo ndoo ya lita kumi iliyokuwa inauzwa 28,000 iuzwe 70,000? Hivi vitu haviendani mafuta ya gari yamepanda sawa, lakini kwa hicho kiwango ambacho yamepanda yanahalalisha leo, kitu kilichokuwa kinauzwa 10,000 kiuzwe 30,000? Ndio hoja yangu ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri watuambie tu kuna *remedy* gani ambazo zinaweza zikafanyika. Mimi Mtanzania wa kawaida ungeniuliza nikiona maisha yangu magumu, naacha kujenga, naangalia watoto wangu wale na watibiwe. Kwa hiyo watu wa uchumi washauri nchi, sasa hivi mtu akipata 10,000 anajiliza 10,000 hii nitafanya nini ili aweze kula na watoto kwa namna vitu vilivyopanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, muda ni mchache na mambo ni mengi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, atafutiwa na Mheshimiwa Bona Ladislaus Kamoli na Mheshimiwa Boniface Mwita Getere ajiandae.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa fursa kuweka mchango wangu leo kwenye Wizara hii nyeti katika maendeleo ya nchi yetu. Awali ya yote nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais mama yetu shupavu, Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ipo Ofisi ya Rais, kupitia Mheshimiwa Rais tumeona fedha nyingi zimepelekwa kwenye halmashauri zetu kwa ajili ya miradi mbalimbali. Zimeenda fedha nyingi kwenye miradi ya afya, miradi ya elimu na miradi ya maji, hususani katika hizo huduma muhimu kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kwa dhati kabisa ni muda wa kumpongeza na kumtia moyo sana yeye pamoja na wanaomsaidia katika hii ili tuweze kupata tija kubwa zaidi katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, pamoja na fedha nyingi ambazo zinapelekwa kwenye halmashauri zetu, tuna changamoto kubwa sana ya miradi viporo, tuna miradi ya muda mrefu ambayo inasuasua. Inawezekana tunashindwa kusimamia vizuri, namna gani ambavyo tunaweza tukasaidia halmashauri zetu kuhakikisha kwamba miradi inayoanzishwa isikae muda mrefu sana bila kukamilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ili kuweza kutengeneza usimamizi mzuri, miradi inayoanzishwa iweze kukamilika kwa wakati kuna haja kubwa sana ya kuboresha kada ya Madiwani. Madiwani ndio wasimamizi wakubwa wa shughuli katika halmashauri na kwa mujibu wa majukumu yao, Madiwani ndio kiungo kati ya wananchi na halmashauri yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mengine ambayo yameainishwa katika Kanuni za Kudumu za Madiwani namba 72(1) na (2). Madiwani wana hali mbaya, wana hali mbaya kwa sababu hawajawezeshwa kufanya kazi kwa maana ya kuzunguka kwenye kata zao, kijiji kwa kijiji kusimamia miradi ya maendeleo ambayo inaendelea kwenye maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Diwani aweze kufanya kazi vizuri, anahitaji kusafiri kutoka eneo moja hadi eneo lingine, lakini posho ambayo wanalipwa, ni ndogo sana na mwisho wa siku tumeishia kuwalaumu Waheshimiwa Madiwani katika maeneo yetu kwamba pengine kada hiyo ipo lakini hatuoni tija kutokana na nafasi ambayo wamepewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kwenda kupata tija kwenye halmashauri, Wizara ya TAMISEMI, tukizungumzia TAMISEMI, tunazungumzia halmashauri zetu nchini, tunazungumzia Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa kwa ujumla wake. Sasa ili waweze kuleta tija kwa nafasi zao, kuna haja ya kutazama upya, kuangalia namna gani tunaweza tukasaidia kuboresha maslahi ya Madiwani, maslahi ya Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa... *(Makofi)*

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilitaka nimpe taarifa Mheshimiwa Husna Sekiboko kuhusu maslahi ya Madiwani, nataka kumwambia kwamba kazi wanaoifanya yote hiyo lakini bado hawana mshahara na posho wanayopewa ni ndogo sana kiasi kwamba utekelezaji wa kazi kwao unakuwa mgumu. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo taarifa kwa mikono miwili. Nataka nimwambie Mheshimiwa Neema, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Madiwani, kanuni 84(1) na (2) kifungu cha kwanza kinasema wajumbe wa Baraza la Madiwani watalipwa posho kulingana na mapendekezo ya halmashauri zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tayari ni tatizo na ni kichaka baadhi ya Wakurugenzi kubana maslahi ya madiwani. Kwa maana kwamba halmashauri inazingizia kuwa imepewa nafasi itawalipa kulingana na makusanyo au kulingana na uwezo. Hivi, ni nani alichagua kuzaliwa Mbeya, Dar es Salaam au Kakonko ambako makusanyo ni madogo, hakuna ambaye amechagua kuzaliwa Singida, wote hao wamezaliwa kwenye hayo maeneo bila kuchagua. Kwa nini walipwe kulingana na makusanyo ya halmashauri? Ikiwa wanatumika, wanafanya kazi zinazofanana katika muda wote na wanaisaidia Serikali katika majukumu ambayo yameainishwa katika kifungu cha 72A. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Diwani aweze kufanya kazi vizuri, pamoja na posho ambayo tumeihamisha kutoka kwenye halmashauri inalipwa sasa Serikali Kuu tulete usawa, Madiwani nchi zima walipwe kama ni mshahara, sio kwenye posho

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

waende kwenye mshahara walipwe sawa, lakini posho zao ziwe na tija hapo tutaweza kuona uwajibikaji wao na mwisho wa siku, hizi fedha ambazo tunapeleka TAMISEMI, *trillions of money* kwenda TAMISEMI, zitakuwa na wasimamizi wazuri na tutaona tija ya miradi ambayo tumeipelekea fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia *ten percent*, ambayo tunazopeleka kwa akinamama, vijana na wenye ulemavu, msimamizi *number one* ni halmashauri na ndio mtekelezaji, lakini nataka nikuhakikishie wako Waheshimiwa Madiwani ambao hata hii *ten percent* hawajapata nafasi ya kuelimishwa vizuri na kujua namna gani wanaenda kuisimamia. Hii inatokana na nini? Ni udhaifu, tumeshawatengenezea Madiwani udhaifu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimekuwa Diwani kwa miaka mitano, tangu 2010 mpaka 2015, Mkuu wa Idara ambaye sasa anapaswa kusimamiwa na Diwani, yeye ndiyo mkubwa kwenye halmashauri. Mtendaji wa Kata ambaye ni Katibu wa *Ward C* Diwani ni Mwenyekiti, yeye ndiyo mkubwa kwenye kata? Kwa nini? Kinachomjengea heshima ni kipato anachopewa. Madiwani wetu siwasemi kwa ubaya, lakini wanakopa kwa watendaji, hivi leo umetoka kwa Mtendaji wa Kata, umekopa kwa Mkuu wa Idara, kesho utakwenda kumsimamia afanye kazi? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna haja kuamua kwa dhati kabisa kama tunataka kuleta tija, TAMISEMI tuangalie upya kada ya Madiwani. Madiwani wapewe nafasi ya kuwajibika baada ya kuboreshewa maslahi yao. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusiana na vifaa tiba, pamekuwa na mjadala kidogo baina ya Mheshimiwa Mabula, kuhusiana na Mheshimiwa Mzanva kuhusu vifaa tiba. lakini nataka nikupe mifano, kuna zahanati zimekamilika ni mwaka wa pili sasa hazifanyi kazi, majengo yanachakaa kwa sababu hamna vifaa tiba. Tuna vituo vya afya vimekamilika, tuna *hostel*, pale Magamba Wilaya ya Lushoto, inaanza kubomoka, hakuna vifaa. Sasa tukianza kujigawanya na kuamua ni wakati gani tununue vifaa tiba

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

na wakati gani tujenge majengo tutakuwa pengine hatufanyi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ambalo nataka niishauri Serikali ni kwamba, tukamilishe miradi yote ambayo imeshaanzishwa kabla hatujaanzisha miradi mipya, ili tupate nafasi ya kuhakikisha kwamba miradi iliyopo inakamilika lakini vilevile na vifaa ambavyo vinatakiwa kwenye miradi hiyo na vyenyewe vinaweza kupelekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nikushukuru sana lakini niendeleo kuipongeza Wizara ila nitoe...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, ila nitoe ombi moja kwa Wizara ya TAMISEMI watazame upya...

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga, ni jambo jipya unaanza au unamalizia sentensi?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere na Mheshimiwa Saimon Songe Lusengikile ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa ajili ya kuiletea nchi yetu maendeleo. Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza Wizara ya TAMISEMI kwa kazi kubwa wanayoifanya katika majimbo yetu. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo ningependa kuongelea suala la *TARURA*. Kwanza nawapongeza sana *TARURA* kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, hususan kwenye Jimbo la Segerea. Pamoja na pongezi hizo kwa kazi kubwa wanayoifanya *TARURA* Jimbo la Segerea au Wilaya ya Ilala, kuna mambo mengi au kuna barabara nyingi ambazo ningependa kwa mwaka huu *TARURA* waziangalie. Kuna barabara nyingi sana ambazo *TARURA* wamezijenga na wamebakisha vipande vidogo vidogo sana. Ukichukulia kama barabara ya Kata ya Liwiti, barabara ya Chang'ombe, wamejenga kilomita moja lakini imebaki kipande kidogo sana. Kwa hiyo, naomba kwa mwaka huu wa bajeti *TARURA* waweze kumaliza hicho kipande. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia kuna kipande kingine ambacho kinapita Kisukulu, kuelekea Bonyokwa, naomba na hicho kipande kiweze kumaliziwa kwa sababu ni vipande vidogo vidogo sana. Haiwezekani kipande kama cha kilomita moja kikakaa kwa muda wa miaka mitatu yaani kuna na barabara kilomita mbili wameitengeneza ya lami, lakini kuna na barabara ndogo sana ambayo wameiacha, kwa hiyo ile barabara ya kilomita mbili ambayo wametengeneza na kuaca kipande kidogo hicho kinaondoa kabisa maana ya ile barabara waliyotengeneza. Kwa hiyo, nawaomba *TARURA*, hivi vipande vidogo vidogo katika Jimbo la Segerea, waweze kuvimaliza kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine nilitaka kuongelea kuhusiana na Miradi ya *DMDP*. Tumezungumza hapa mwaka 2021 nikiongelea Bonde la Mto Msimbazi kwamba litaanza kujengwa mwezi wa Tatu mwaka huu, lakini mpaka sasa hivi halijaanza kujengwa. Bonde la Mto Msimbazi lilikuja na barabara zake ambazo tulikuwa tumeahidiwa na wataalamu wetu kwamba litajengwa pamoja na barabara ambazo zimefuatana, nikiongelea barabara ya Segerea - Seminari ipo kwenye mradi wa Bonde la Msimbazi na pia ukichukua barabara ya Kisukulu – Maji Chumvi – Migombani, ipo kwenye Bonde la Mto Msimbazi. Mpaka sasa hivi tunavyoongea,

bado hili Bonde la Mto Msimbazi halijaanza kujengwa wala hizi barabara hazijaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nimemwulizia sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu ndiyo walikuwa wanapitisha huu mradi wa *DMDP*, mpaka sasa hivi hatujajua. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu, kwa sababu sisi tayari tulishawaahidi wananchi kwamba itakapofika mwezi wa Tatu litaanza kujengwa.

Mheshimiwa Spika, kama unavyojua, Mkoa wa Dar es Salaam mvua kidogo ikinyesha au isiponyesha Dar es Salaam, ikanyesha sehemu nyingine, yale maji yanapita kwenye Bonde la Mto Msimbazi na kwa sababu ya miundombinu chakavu iliyopo katika Jiji la Dar es Salaam, yale maji yanawafuata wananchi. Zamani tulikuwa tunasema kwamba Bonde la Mto Msimbazi watu wamejenga karibu na bonde, lakini hapana, ni kwa sababu lile bonde sasa hivi limekuwa chakavu sana, kwa hiyo, maji yanaenda kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulikuwa tunaomba sana majibu, tutakapomaliza huu Mkutano wetu wa Bajeti, tunarudi kwa wananchi na watatuuliza, mlituahidi kwamba Bonde la Mto Msimbazi litaanza kujengwa, lakini halijaanza kujengwa mpaka sasa hivi pamoja na hizo barabara nilizozitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna barabara moja ya Banana - Kitunda – Kivule ambayo inapitisha zaidi ya magari 3,500 kwa siku. Nimeona hii barabara ni ambayo ni ya lami, sasa hivi imetengewa shilingi milioni 560 kwa ajili ya kuiwekea changarawe. Sasa utaona kwamba barabara iliyokuwa ya lami inarudishwa kwenye changarawe; na hii barabara mwaka 2021 ilitengewa shilingi milioni 400, ikatengenezwa kwa changarawe; na mwaka huu imetengewa shilingi milioni 560 inatengenezwa kwa changarawe.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aweze kuangalia barabara zetu ambapo kuna maeneo

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambayo wananchi wengi wanaishi. Mfano kama hii barabara ninayoisema, ina kilometa 12.5 na wananchi ambao wanaishi kule ni zaidi ya 300,000. Kwa hiyo, sasa ukisema kwamba unaitengea barabara shilingi milioni 560 ili iwekewe changarawe, bado hujatatua tatizo, kwa sababu baada ya hapo, mvua itakaponyesha, ina maana matatizo yataendelea. Kwa hiyo, tulikuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri, kwa sababu barabara hii ipo katika mradi wa *DMDP*, tunaomba huo mradi uweze kusainiwa mapema ili hizi barabara ziweze kujengwa. Barabara zetu... *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mtemvu.

### T A A R I F A

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji juu ya *DMDP*. Ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam siyo tu eneo hilo analolizungumza la nyimbo la Segerea, lakini hata kwenye Jimbo la Kibamba ahadi ilitokea kilometa 107 mwaka 2020 mbele ya Rais aliyepo sasa akiwa Makamu wa Rais kwamba zitajengwa na *DMDP III* lakini mpaka sasa bado kuna mtu kakalia kwa miezi minne kusaini mkataba huo. Ni kweli nakuunga mkono ili tupate majibu Mheshimiwa Waziri akija kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa hiyo. Nami nataka niongezee tu kwamba, sisi wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam tukija hapa tunaomba barabara na maji. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri aangalie ni jinsi gani atatuboreshea barabara zetu ambazo tunaona zinawasaidia wananchi kwa ajili ya kufanya shughuli zao za maendeleo za kila siku. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, barabara hizi tulizosema kwamba zimeingia kwenye mradi wa *DMDP*, ni barabara kubwa. Mfano, hiyo barabara moja ambayo inatoka Kimanga ya kilometa 3.5, *obvious* huwezi kuiweka kwenye *TARURA*, itachukua muda mrefu. Tuna barabara nyingine ya Bonyokwa - Kimara ambayo ina kilometa 4.6, na yenyewe pia imewekwa kwenye mradi *DMDP*. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba hizi barabara ambapo hatuombi zote zitengenezwe lakini hizi ambazo zitawasaidia wananchi waweze kufanya shughuli zao kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichokuwa nataka kuongelea, kwanza niishukuru wizara kwa kutujengea vituo vya afya Kinyerezi, Segerea pamoja na Kiwalani. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri Jimbo la Segerea ndiyo lenye wananchi wengi Tanzania nzima. Kwa hiyo, kuwa na Kata ambayo haina hata zahanati inakuwa ni changamoto sana. Kwa sababu unakuta Kata moja; mfano, Kata ya Buguruni ina wananchi karibu 300,000, lakini hawana zahanati. Kwa hiyo, tunaomba wapate zahanati. Pia Kimanga pamoja na Kisukulu, hizi Kata zote hazina zahanati. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje na haya majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara ya TAMISEMI. Awali ya yote tumshukuru Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa Rais ambaye anafanya kazi nzuri sana katika Tanzania hii, nami namwombea kwa Mungu aendelee kumtunza. Watanzania wamwache Rais afanye kazi yake kadri anavyoona yeye, kwa sababu ni muda wake wa kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naishukuru Wizara hii kwa sababu inafanya kazi vizuri. Wapo Mawaziri vijana kabisa hapa. Yupu



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Katibu Mkuu, tunamfahamu Profesa, amefanya kazi mpaka kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri mbalimbali, ana uwezo huo. Makatibu wake wapo vizuri sana na wanafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la TAMISEMI ni *coordination*. Bahati nzuri ukurasa wa 90 mpaka 93 wameongelea ubadhirifu wa mali ya Umma TAMISEMI. Watumishi wazembe; mahusiano yao na Halmashauri ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kimenishangaza sana juzi hapa. Tarehe 07 Aprili, 2022 Mheshimiwa Rais alikuja Bunda, tukaongea, Mheshimiwa Bashungwa alikuwepo. Kukawepo na fedha ya Sekondari kati ya Tingirima na Kyandege, bahati nzuri Mheshimiwa akazungumza, hela ikaletwa. Hela ya sekondari imekuja toka tarehe 07, vifungu vya kufungua hiyo hela itumike vimefunguliwa tarehe 12 mwezi wa Nne, halafu nimeona hapa wanasema tuna *call center*, tuna maeneo maalum. Tatizo la TAMISEMI ni *coordination*. Mahusiano yake na watu wa chini ni shida sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, viongozi tuliowaweka hapo; Waziri ni kiongozi mzuri sana, bajeti yake tutapitisha, nami naunga mkono hata kabla sijamaliza. Yupo vizuri, tatizo, ashughulike na walaji wa Halmashauri. Halmashauri ya Bunda ni mbaya na imepata hati mbaya. Siyo chafu, ni mbaya. Amekuja Rais amesema, lakini mpaka leo hakuna mtu ametoka kwenye ofisi ya Mheshimiwa Waziri kwenda pale kushughulika na ile Halmashauri. Juzi Mkurugenzi ameulizwa mtu aliyekula hela za Afya; *DMO* amekula hela za Afya, anaulizwa Mkurugenzi, anakimbia na mafaili. Sasa ni vurugu zinatokea. Kwa hiyo, *coordination* ni mbaya sana katika Halmashauri zetu. Kwa hiyo, naomba kwenye hilo, mshughulike nalo vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna jambo limezungumzwa hapa la Utawala Bora na nyie mmelizungumza vizuri hapa. Utawala Bora maana yake Wizara hii ndiyo inatafsiri *D by D*. Wao ndio wanatakiwa wapeleke maelekezo ya Utawala Bora kwenye

Kata, Tarafa, Vijiji na kwenye Vitongoji. Shida iliyopo hapa naona tunazungumzia sana Madiwani, hivi Wenyeviti wa Vijiji wanaishije? Wenyeviti wa Vitongoji wanaishije? Wenyeviti wa Mitaa wanaishije?

Mheshimiwa Spika, hivi kweli leo kijiji kina mnada, kina madini, kina mifugo na kila rasilimali zilizopo hapa, Halmashauri inakusanya zote, inapeleka Halmashauri, Mwenyekiti wa Serikali, Serikali yenyewe haina chochote inachopata. Hata kuwalipa mishahara basi, achieni mapato yao yale ya kisheria ya Na. 7 mpaka Na. 8 wayapate wao. Kama kuna mnada mahali, kijiji kilicho na mnada kipate mapato. Kama kuna mawe wanakusanya, wapewe. Sasa...  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

#### **T A A R I F A**

**MHE. ALLY A.J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Getere kwamba hata sasa kwenye zoezi linaloendelea la anuani za makazi, watendaji ndio wanaofanya kazi, lakini Wenyeviti na wale Wenyeviti wa Vitongoji wameachwa pembeni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, naipokea sana, kwa sababu ni mwelewa, naye anayajua haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako, kama inawezekana, siyo lazima, kama ulivyosema kwa Viti Maalumu wakae, nasi siku moja tukae basi na hii TAMISEMI hata kama ni katika ukumbi wa Pius Msekwa, tulizungumze hili jambo la Utawala Bora. Uchaguzi upo karibu, 2024 nadhani tunaanza uchaguzi wa Serikali za Mitaa, unakwenda kusimamia watu, unatumia *billions of money* kusimamia watu; wanapatikana Wenyeviti wa Vijiji, zinapatikana Serikali,

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanapatikana Wenyevidi wa Vitongoji, halafu unawa-*dump*. Hakuna semina, hakuna mafunzo, hakuna vitabu vya kujifunza, hakuna chochote. Haiwezekani! Sasa tunakuwaje na Serikali? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huku juu sisi tunatembelea magari, wao hata kuwasimamia basi wapate chochote. Halmashauri inakusanya chochote; mchanga inakusanya, mawe inakusanya, minada ni yao, kila kitu inabeba. Inawaacha wamekaa pale bure. Sasa Utawala Bora huu utakuwaje jamani? Haiwezekani. Kwa hiyo, nafikiri kwamba hili nalo tuliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeona Wizara imetenga fedha nyingi sana za sekondari; na sera zetu zinasema tujenge Sekondari kwenye Kata, tujenge sijui vituo vya afya kwenye Tarafa, sioni shida. Naomba twende mbali zaidi, tujenge sekondari kwenye maeneo maalum. Inawezekana tukawa na Kata tatu zina sekondari moja. Umbali wa kutoka Kata hiyo mpaka sekondari ni kilomita tatu. Inawezekana kwa mfano Bunda, ukitoka Vijiji vya Mahanga na Machimero kwenda Sekondari ya Mihingo ni kilomita 17, halafu leo unasema huwapi sekondari. Watoto wanaokwenda kujiunga kutoka hivyo vijiji wanaweza kuwa 60, wanamaliza 20.

Mheshimiwa Spika, umbali wa kutoka pale ni mrefu, mvua ikinyesha hakuna mahali pa kujikinga, ni porini. Kwa hiyo, tuwe na dhana ya kujenga sekondari kwenye Kata na kwenye maeneo maalum ili tusiwe na fedha na lengo tu kwamba tunajenga kwenye Kata, hapana, ni maeneo maalum.

Mheshimiwa Spika, leo Sekondari ya Sanzate ambayo wanaiita Mama Samia, inajengwa na hapa tunapozungumza wananchi wanachimba msingi. Naomba Serikali itambue hiyo Sekondari. Wananchi wamechoka, Sekondari ya Mahanga na Machimero wanachimba msingi, Sekondari ya Nyaburundu wanachimba msingi, Sekondari Maliwanda na Kisarakwe wanachimba msingi. Wananchi wamechoka, wanataka kujenga sekondari kwenye maeneo maalum.

Umbali wa kutoka kwenye maeneo hayo kwenda hapo, ni suala kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza vituo vya afya, kuna vitu vinashangaza sana. Nami nimekuwa Bungeni hapa wakati fulani najiuliza maswali mengi sana. Tuliomba vituo vya afya vikajengwa 2016, tukaambiwa vituo vya afya vinajengwa kwa shilingi milioni 700. Kwa mfano, Kituo cha Afya Mgeta, shilingi milioni 700, tukaambiwa tutakupa shilingi milioni 400, halafu shilingi milioni 300 itapelekwa MSD kuleta vifaa tiba. Tumepewa shilingi milioni 400 tumejenga Kituo cha Afya Mgeta, kipo mpaka leo, vifaa hakuna. Wameleta vifaa vya shilingi milioni 161, wame-*dump* hapo ndani. Hata majokofu ya kufanyia *mortuary* hamna.

Mheshimiwa Spika, nauliza, tuliambiwa hapa zile fedha siyo kwamba zilikuwa za makusanyo, tulikuwa tumepata msaada sijui wa Canada sijui wapi, shilingi milioni 700 kila kituo. Waliopewa shilingi milioni 500, watapewa shilingi milioni 200; waliopewa shilingi milioni 400, watapewa shilingi milioni 300, hizo fedha ziko wapi? Ziko wapi? Tuliambiwa kwamba zimekwenda MSD, ziko wapi? Kwa hiyo, nafikiri Mheshimiwa Waziri akija hapa aje na tafasiri ya kwamba hizi fedha zinapatikana wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwamba katika ile haja ya kujenga TAMISEMI, nyie vijana msimwanguushe Rais, amewaamini sana. Jamani mimi niseme, Rais Samia amewapa mamlaka yote Mawaziri. Kwa hiyo, kama Waziri anazingua, ni yeye; nasi humu Bungeni tutamzingua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hatuwezi kusema kwamba mnakosa nini, mnapewa msaada. Juzi Mheshimiwa Bashungwa nimeona Mheshimiwa Rais anakwambia, Inno! Anakuita Inno, *take care*. Sasa nasi tunakwambia, umepewa hiyo kazi, Rais amekuamini sana. Tutekelezee yale ambayo yanayoitajika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, tujengewe Sekondari Jimbo la Bunda. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, nami nashukuru kwa kunipa nafasi leo nichangie hotuba ya Waziri wa TAMISEMI. Kwanza nianze kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya katika Taifa letu. Amenikumbusha maneno ya Biblia, ukisoma Ezra 10 mstari wa 4 inasema: *“inuka sasa maana kazi hii inakuhusu wewe; na sisi tu pamoja nawe; na uwe na moyo mkuu, ukaitende.”*

Mheshimiwa Spika, haya maneno yananikumbusha kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Rais kwa sababu ameamua kuamka; ameinuka na kazi hii inamhusu yeye na ameenda kuitenda, nasi tuko pamoja naye kuhakikisha kwamba kazi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kaka yangu Mheshimiwa Innocent na wasaidizi wake wawili; Mheshimiwa Dugange pamoja na Mheshimiwa David, wanafanya kazi kubwa sana kwenye wizara hii ya TAMISEMI. Tunawapongeza kwa sababu tunaona matunda makubwa ya kazi ambayo mnafanya kwenye Majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Katibu Mkuu wa TAMISEMI, Profesa Shemdoe. Kwa kweli Profesa ni msikivu sana; tunapoenda sisi Wabunge na kazi zetu pale kwake anatusikiliza na hata ukimpigia simu anapokea wakati wowote, hata akiwa hana nafasi, anasema atapiga baadaye na kweli anafanya hivyo. Nampongeza sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA*, kaka yangu Seif. Kwa kweli kaka huyu ni wa mfano sana kwetu; ni mtu anayesikiliza, ni

mtu ambaye ukipeleka shida yako anatatua. Anawasiliana na watu wa wilaya kuhakikisha kwamba maeneo yetu yanakuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami sasa nichangie kidogo kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nianze na posho ya Madiwani. Nimezungumza na dada yangu hapa, nami naomba niseme kwamba Madiwani wanafanya kazi kubwa sana kwenye Majimbo yetu na kwenye Wilaya zetu. Ni watu ambao wanasimamia miradi yote ambayo inapelekwa na Serikali. Utamwona asubuhi Mheshimiwa Diwani anajikokota na baiskeli yake, anaenda kuangalia mradi umefikia wapi? Leo sisi kama Wabunge ni lazima tutafakari kwa maslahi mapana sana ya hao Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimekuja na hesabu ndogo hapa. Tuna Madiwani 5,287; ukiwapa tu posho yao hata shilingi 800,000/= kwa mwezi, tutakuwa tunawalipa kwa mwezi shilingi bilioni 4,200. Tuki-*calculate* hii kwa mwaka, tutawalipa shilingi bilioni 50.7. Ninaamini kwa Serikali yetu inawezekana kuwalipa kiasi hiki Madiwani ili waweze kufanya kazi nzuri kwa ajili ya Watanzania, kwani Madiwani wanafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata huko Mbeya najua wanakulindia Jimbo na wanafanya kazi kubwa kuhakikisha kwamba wewe unapokuwa hapa wao wanafanya kazi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba eneo linabaki kuwa salama. Kwa hiyo, niseme, sasa ni wakati muafaka wa Wizara kulichukua hili na kwenda kulifanyia kazi ili Madiwani wetu posho yao iimarike, nao hata wakienda Halmashauri kusimamia miradi, wawe na kitu ambacho wanaweza kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Madiwani wengi wanatumia baiskeli, kuna haya hapa mwanzoni wanapokuwa wameshinda watafutiwe hata mkopo wa bila riba, walau wapate pikipiki. Madiwani wanapoenda kusimamia miradi, wawe na usafiri ambao sasa ni chanya kwao kutembelea vijiji na Kata zao ili waweze kusimamia miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine naomba nizungumzie kidogo sehemu ya afya. Nimesoma Bajeti ya TAMISEMI, naishukuru sana Serikali kwa kutuletea vituo vya afya. Tuna kituo cha afya pale Busega tunajenga, Ngasamo, lakini kwa bajeti hii Waziri kwa kweli hajaweka kituo cha afya hata kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba Naibu Waziri wa TAMISEMI, kaka yangu, Mheshimiwa Dugange amekuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, anaifahamu Kata ya Kabita. Hii ni Kata ya kimkakati yenye wapiga kura wengi sana. Ni Kata ya pili kwa wingi wa wapiga kura katika Jimbo la Busega. Ni muda muafaka sasa Serikali ione Kata hii ya mkakati kuipelekea kituo cha afya. Najua hatuwezi kujenga kila Kata lakini walau Kata za kimkakati tuweze kupata kituo cha afya. Nami ukiniuliza leo, nitakwambia kwa Jimbo la Busega kipaumbele kianze pale Kabita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha pili, kwenye Jimbo langu la Busega tuna maboma mengi ya zahanati wananchi wamejenga. Tuna zaidi ya maboma 15, lakini kwenye bajeti hii nimeona ukamilishaji wa maboma ya zahanati katika Jimbo la Busega imepangiwa zahanati moja ambayo itakamilishwa. Sasa kuna haja ya kuhakikisha kwamba tunaongeza walau tufanye kama ilivyokuwa mwaka wa fedha huu unaoisha tupate zahanati tatu ili tuweze kuzipunguza zile zahanati ambazo wananchi wameanzisha. Wananchi wanatumia gharama kubwa, wanajitoa kwa mioyo, muda mwingine hawapati chakula, wanahakikisha kwamba wanatoa michango kwa ajili ya kujenga zahanati. Sisi kama Serikali, kama wadau ambao wananchi wametuchagua, sasa tuweze kuwapangia fedha ili aweze kukamilisha zahanati zao. *(Makofi)*

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simon Songe kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge wa Busega ni sahihi kabisa kwamba wananchi wamejenga majengo ya zahanati, vituo vya afya na madarasa ambayo wametumia nguvu zao na hata sasa yanashindwa kumaliziwa, nguvu za wananchi zinapotea bure. Ninavyosema hivyo Kituo cha Afya Msindo, Wilaya ya Namtumbo wananchi wamejenga jengo la upasuaji, mpaka sasa hivi bado hawajapata pesa ya kumalizia na jengo lile lipo kwenye hatari ya kudondoka katika msimu huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Lusengekile unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, naipokea.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka nichangie ni eneo la *TARURA*. Pamoja na pongezi ambayo nimetoa kwa kaka yangu Seif lakini bado tuna kazi kubwa ni lazima tuongeze bajeti sasa eneo hili la *TARURA* ili tuweze kutengeneza barabara zetu. Vijijini bado kuna kazi kubwa ya barabara. Mfano, katika Jimbo la Busega tumetengeneza barabara za Kata zetu tatu lakini kwenye makutano ya zile barabara kuna tatizo la daraja pale Mwamigongwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati sahihi kutafuta fedha zaidi ya milioni 500 twende tukatengeneze lile daraja ili tuwe na mawasiliano ya hizi Kata tatu, Kata ya Malili, Kata ya Imalamate na Kata ya Mkula pale kwenye makutano ili kata hizi ziweze kufunguliwa ili tuweze kusafirisha mazao na tuhakikishe kwamba wananachi wanasafirisha mazao yao yakiwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara inayounganisha mikoa miwili, Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Simiyu. Barabara inayoanzia pale Sayaka inapita Nyaruande inapita Badugu inaenda mpaka Dutwa mpaka kule Bariadi. eneo hili pia tulitengee fedha ili tuweze kutengeneza kama ambavyo itakuwa imekusudiwa. *(Makofi)*



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo. naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dokta Christine Ishengoma atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara hii, Sekta hii ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa nchi yetu katika maendeleo. Pili, nakushukuru na kukupongeza wewe kwa jinsi ambavyo unatuongoza humu Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze ndugu yangu Waziri Bashungwa, kwa kweli tunamtegemea anafanya kazi nzuri pamoja na Manaibu wake na Makatibu wake wazuri. Nikianza hapo hapo nakuja kwa Manaibu Katibu Wakuu. Kuna Naibu Katibu Mkuu kwenye Afya anafanya vizuri sana, Naibu Katibu Mkuu kwenye mambo ya Elimu anafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mambo ya uzalishaji ambayo wananchi wengi wanategemea sana, haionekani wazi wazi Katibu Mkuu yuko wapi? Ambaye anaweza akasimamia wazi wazi kwa kusaidiana na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwenye mambo ya kilimo ambayo wananchi wengi wanakitegemea na mifugo ambayo watu wengi wanaitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kuwa tungekuwa na Naibu Katibu Mkuu ambaye yuko *assigned* kwenye mambo ya kilimo, mifugo na uvuvi, sekta hii ya uzalishaji ingefanya mambo mazuri sana. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akija kuainisha hapa ni vizuri atueleze vizuri Serikali imejipangaje kama tunaweza tukapata Naibu Katibu Mkuu ambaye anashughulikia mambo ya Sekta ya Uzalishaji. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwa kusema kuwa Wabunge tuko humu ndani kuwakilisha wananchi waliotutuma. Nimetumwa na Waheshimiwa Madiwani, Madiwani hasa wakiwakilishwa na Madiwani wa Mkoa wa Morogoro. Madiwani hasa wakiliwakilishwa na Madiwani wa Manispaa ya Morogoro. Madiwani wanafanya kazi kubwa sana na wewe mwenyewe na Wabunge wote tunaamini kuwa wanafanya kazi kubwa. Wanachoomba posho yao ni ndogo na maslahi yao, waongezewe kiasi na wenyewe waweze kufanya kazi vizuri. Tuko humu Bungeni lakini wenyewe ndiyo wanalinda majimbo yote. Tuko humu Bungeni ndiyo wanaofanya kazi zote za kijamii, za Serikali na za kichama. Kwa hiyo naomba sana tuwaangalie Waheshimiwa Madiwani kwa upande wa elimu na kwenye maslahi yao. Hapo hapo na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na wenyewe waangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siko mbali sana, naongelea asilimia 10. Asilimia 10 hiyo mahali inatumika vizuri, mahali pengine siyo vizuri. Ni kweli haitoshi vikundi ni vingi sana, lakini ingeweza kutosha kama ingesimamiwa vizuri sana. Kwa mfano miradi ya maendeleo kwa upande wa akinamama asilimia nne hiyo, miradi ya kimaendeleo kwa upande wa vijana asilimia nne hiyo na miradi ya kimaendeleo kwa watu wenye ulemavu ingeweza kuwanufaisha wanufaika hao.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano hela zinazorejeshwa hazina mpangilio mzuri wa marejesho. Halmashauri zingine hawajui jinsi ya kuzipangilia. Kwa hiyo naishauri Serikali iangalie jinsi ya kuwanufaisha walengwa kusudi waweze kunufaika na hizi asilimia 10. Pia uwepo ufuatijaji, ufuatiliaji mahususi wa kuona hizi fedha zinatumikaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu *TARURA*. Kwa upande wa *TARURA* wanafanya vizuri sana. Wameongezewa hela naamini kuwa watafanya vizuri hasa kwenye barabara za vijijini na hata kwenye barabara za mijini pembezoni. Nikichukua barabara ya Mjini Morogoro ambayo inaanzia Mziga mpaka Mgambazi ni mbaya sana. Nikichukua ya Fokoland ni mbaya sana na barabara zingine za

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pembezeni. Vijijini Bwakila Juu ni mbaya sana, Kweuma ni mbaya sana. Kwa hiyo, hiyo ni mifano midogo ambayo *TARURA* naamini wanafanya vizuri lakini kwa kuongezewa hela naamini watafanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makandarasi wanaofanya miradi ya barabara na wanaofanya miradi ya maji, naomba waangaliwe vigezo vyao kama wametimiza? Wakimaliza kazi zao walipwe kwa wakati wasiwacheleweshe kuwalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo ninaloongelea sasa ni upande wa elimu. Hapa elimu namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi aliyofanya kwa hiyo hela ya trilioni 1.3. Kwa kweli kila mmoja anayaona mambo mazuri anayoyafanya Mheshimiwa Rais kwa upande wa kujenga shule, madarasa na upande wa matundu ya vyoo, lakini kuna shule zingine za sekondari, kuna shule zingine za msingi kama *SUA* Sekondari bado hawana maabara, bado hawana matundu ya vyoo. Kwa hiyo ningepomba kuwa na wenyewe waangaliwe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la elimu ambalo natoa ushauri ni kwa upande wa chakula cha mchana. Chakula cha mchana hasa kwenye shule za kutwa bado ni changamoto kwenye baadhi ya shule. Kwa hiyo naomba waweke mkakati, waandike barua au mwongozo kwa shule zote za sekondari za kutwa na kwa shule zote za msingi waweze kupata chakula cha mchana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Walimu, ni kweli mgawanyo wa Walimu bado hauendi vizuri hasa kwa shule za pembezoni. Naomba waweze kupata Walimu wa kutosha hasa wa sayansi pamoja na sanaa tunaajiri. Pongezi sana Serikali kwa kuajiri, kuomba vibali, lakini mgawanyo uangaliwe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, tumejenga vituo vingi vya afya, tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais na hata Mkoa wetu wa Morogoro

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

tumejenga vituo vya afya zaidi ya vitatu. Tumejenga hospitali zaidi ya sita. Kwa hiyo tunampongeza Mheshimiwa Rais lakini tatizo bado ni wafanyakazi, wataalam wa afya. Tatizo unakuta kuwa hospitali au zahanati moja kwa mfano, Zahanati ya Mvuha. Zahanati ya Mvuha kuna Daktari mmoja na *Nurse* mmoja, siku Daktari akiumwa au *Nurse* akiumwa hakuna kazi siku hiyo. Kwa hiyo tunaomba waongezwe wataalam wa afya pamoja na dawa na vifaa tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwa upande wa afya hiyo hiyo, naomba waangaliwe hasa kinamama kwenye *maternity* zao. Kuna *maternity ward* nzuri sana ambazo zimejengwa, lakini wataalam na madawa hakuna. *(Makofi)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, nimemaliza bado? dakika tano?

**SPIKA:** Muda umeshaisha. Dakika nane zimeisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hiyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nasikiliza michango yenu hapa ya kuhusu Madiwani, lakini kuna hii kauli nadhani inarejewa mara kadhaa kwamba Waheshimiwa Madiwani wanalinda Majimbo ya Wabunge. Nadhani tutakuwa tunawaweka katika wakati mgumu, humu ndani kuna Madiwani ambao wamewatoa Wabunge. Kwa hiyo tusiwaweke kana kwamba wawe ni walenzi wa Majimbo kama vile wao hawana haki ya kugombea Ubunge. *(Makofi)*

Hata wao hiyo haki wanayo, kwa hiyo tusiwafanye wawe ni walenzi wa majimbo, lakini tukubaliane hoja ya msingi kwamba wanafanya kazi nzuri na wanafanya kazi za kwao kama Madiwani na isionekane kana kwamba sasa, maana kuna maeneo ambayo Wabunge wanagombana na Madiwani, kwa sababu gani, watu wanaona pengine Diwani

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

sijui amefanya nini, wasifiwe kwa kazi wanayoifanya nzuri kwenye maeneo yao ya uwakilishi. Kwa hivyo utetezi wao utakuwa kwa mtindo huo, lakini isionekane picha hivi tunayoijenga kana kwamba Wabunge tunao uwezo wa kuwazuia Madiwani kugombea kwa sababu wanatulindia sisi Majimbo. Ni haki yao kabisa na wao kugombea kama ambavyo kuna Madiwani humu ndani waliowatoa Wabunge na kuna Wabunge waliowatoa Wabunge wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ajiandae.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema. Pia nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Mawaziri. Nimpongeze sana kaka yangu Bashungwa pamoja na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya. Nimpongeze kaka yangu Katibu Mkuu Profesa Shemdoe na timu yake nzima kwa kweli wamekuwa wasikivu na kazi kubwa inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Singida Mjini tumepata miradi ya kutosha sana ya elimu, afya, barabara na kazi inafanyika na leo tukifanya ziara tunazungumza kwa vitendo na wala siyo maneno kama ilivyokuwa awali, niwapongeze sana kwa kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ukurasa wa 103, Serikali imezungumzia malengo mahususi yatakayotekelezwa mwaka huu wa fedha. Lengo la kwanza limezungumziwa Mfuko wa Jimbo. Wameweka nyongeza ya zaidi ya asilimia 45, ni jambo jema sana, hongereni sana. Tunatambua mchango mkubwa na CAG amesema tumetekeleza kwa asilimia 100 Mfuko wa Jimbo, ni jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipengele cha pili tumezungumzia bima ya afya ya Madiwani, kwamba bajeti iliyopita Madiwani sasa posho zao zilikuwa zinalipwa na Serikali kupitia Serikali Kuu, ilikuwa ni jambo zuri. Wakati wanalipa hawakuwa wame-include bima ya afya, mwaka huu wametenga milioni 600 kwa ajili ya bima ya afya, hili ni jambo jema sana, Serikali imetambua eneo muhimu.

Mheshimiwa Spika, hapa kwenye eneo hili la Madiwani nataka kushauri na umetoa ufafanuzi mzuri. Nami nataka nishauri na niwakumbushe Serikali, umuhimu wa maslahi ya Madiwani ni mkubwa kuliko tunavyofikiri sisi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapotangazwa tu na Tume ya Uchaguzi maana yake utumishi wako umekoma, unaingia kwenye utumishi mwingine, lakini huu utumishi mwingine tunautambua kwa posho wa Madiwani, hatuutambui kwa ajira. Nataka kuiomba Serikali, utumishi huu wa Madiwani tuutambue kwa ajira ya mkataba. Ukishazungumza ajira ya mkataba maana yake huyu mtu sasa hatuzungumzii mambo ya posho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tulipoamua sisi Serikali Kuu kulipa posho za Madiwani maana yake tumeua kabisa Kanuni ile ya Baraza la Madiwani ambayo inazungumza posho. Sasa kama tumeua hii, tuje na kanuni mpya itakayozungumzia mkataba wa ajira kwa Madiwani. Mkataba wa ajira kwa Madiwani utakuwa na nyongeza nzuri ya mshahara, utakuwa na nyongeza nzuri ya kila mwaka ambayo Serikali inaongeza. Tutaondokana na haya malumbano ambayo tunaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi kwamba wenzetu wanafanya kazi kubwa sana na wanafanya kazi nzuri sana ya kusimamia miradi ya Serikali. Miradi yote hii na hasa mchakato wa bajeti kuanzia chini, Mwenyekiti wa Kamati ya *Ward C* ni Diwani lakini wataalam wake ukizungumzia mshahara wa chini sana ana *TGS D*, ambapo hapa unazungumzia zaidi ya laki saba na kuendelea. Sasa

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anamsimamiaje mtu yeye ana posho! Kwa hiyo lengo la msingi la wote kuwaweka kwenye ajira, huyu atakuwa na ajira ya kudumu na huyu atakuwa na ajira ya mkataba.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali tukabadilishe miongozo yetu, tuje na mwongozo ambao unaonesha dhahiri kwamba tunahitaji sasa Madiwani wetu waingie kwenye ajira ya mkataba wa miaka mitano ili wao na malipo yao yaendane na ajira.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu suala la malipo ya mshahara na tofauti na posho, ukizungumzia posho, hii siyo *mandatory*, posho siyo lazima, huku chini maana yake tulikuwa tunategemea makusanyo ndiyo mtu aweze kulipwa, lakini tukienda kwenye ajira ni lazima, hata Diwani anaweza kwenda kuudai mshahara wake Mahakamani kama hajapewa, kwa sababu mshahara ni sheria lakini posho hii tumetengeneza utaratibu tu wa kuwawezesha kujikimu. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili hapa, ni mradi wa *TACTIC*. Mradi huu umeanza muda mrefu sana na nimeona Serikali imeeleza vizuri katika ukurasa wa 92. Mradi wa *TACTIC* wa Miji 45, Singida Mjini ikiwemo. Hata hivyo, kwenye huu ukurasa wa 45 tumeelezea sana *TARURA*. Kazi ya *TARURA* ni suala la barabara. Sasa mradi huu na fedha zote hizi tukizungumzia kwenye barabara peke yake watakuwa wametubana sisi ambao tayari tulijua mradi huu unaenda kuboresha maeneo yetu ya masoko, *unless otherwise* sijaona kwenye bajeti, nitaomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri watueleze, mwanzoni *component* ya mradi huu wa *TACTIC* ulikuwa unazungumzia masoko.

Mheshimiwa Spika, pale Singida Mjini tuna Soko la vitunguu, soko lile lilikuwa linajengwa kwa kuwa soko la kimataifa linagharimu zaidi ya bilioni sita na upembuzi yakinifu umeshafanyika na sisi tumewaeleza wananchi kwamba Serikali inafikia hatua za mwisho katika kuja kukamilisha ujenzi wa soko lile la kimataifa la vitunguu, lakini humu ndani sijaona, nitaomba Serikali ije na majibu.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, la pili lake, tuna soko kubwa pale la majengo ambalo nalo linatakiwa lijengwe kuwa soko la kisasa kupitia mradi huu huu wa *TACTIC*, sasa sijaona hapa wakizungumzia masoko, naona Miji 45 tunazungumzia habari ya barabara, lakini Miji 45 wameweka *phase* jambo jema sana. Sisi tuko kwenye *phase* ya pili, tutasubiri, lakini tutasubiri tukiwa na *component* zote Mji unakua, Mji ambao sisi tunatarajia uwe Jiji hauwezi ukawa Jiji kama masoko haya hatujayajenga kuwa masomo ya kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine nitaiomba sana Serikali au Mheshimiwa Waziri, Ofisi yetu ya Manispaa, jengo la Utawala tulishawaomba na tumeleta ramani na kila kitu, tunahitaji kujenga Jengo la Utawala ambalo linaendana na hadhi ya Singida Mjini. Kwa mazingira hayo nitaomba Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii atuzingatie tujenge Jengo la Utawala la kisasa. Sasa leo wenzangu wa Singida *DC* kule, wenzangu wa Itigi huko wana jengo zuri, mimi ndiyo mwenye Mji wa kisasa, una kila kitu, halafu jengo limebaki kuwa la kizamani, hapana. Niwaombe sana tuhakikishe tunaweka jengo la kisasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jambo jema sana. Sisi tulikuwa na changamoto ya Hospitali ya Wilaya na tukaomba Hospitali ya Mkoa ile tukabidhiwe. Hapa nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Ummy akiwa Wizara hii alitoa maelekezo hivi tunavyozungumza mwezi wa Saba kwa maelezo yao kwamba watatukabidhi majengo ya Hospitali ya Mkoa yawe Hospitali ya Wilaya na kuwa Hospitali ya Wilaya itakuwa chini ya TAMISEMI. Nataka niwaombe wenzangu wa TAMISEMI watusaidie, wametuletea fedha milioni 500 tutakwenda kujenga kituo cha afya kwenye Kata yetu ya Unyambwa ile milioni 500 waliyotuletea kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ili haya majengo ya Hospitali ya Mkoa tutakapokabidhiwa, watusaidie kuyasimamia. Hospitali ya Mkoa majengo yake yawe Hospitali ya Wilaya na hili jambo kuwa Hospitali ya Wilaya tutahitaji kuwepo na rasilimali watu, tunahitaji kuwa na watumishi wa kutosha. Wakati tunakabidhiwa tuwe na watumishi wa kuendesha Hospitali yetu ya Wilaya. Tuwe na vifaa tiba vya kuendesha Hospitali



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yetu ya Wilaya, tusije tukakabidhiwa majengo halafu nikarudi tena Bungeni kuja kuanza kutembeza bakuri na kuwaomba jamani naomba watumishi, naomba vifaa tiba, hapana. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kazi hii ambayo tunakwenda kuifanya na kuhakikisha Jimbo letu la Singida Mjini na sasa tunataka tuweke malengo makubwa ya Jimbo hili kuwa Jiji Ikiambatana na Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Robert Chacha Maboto na Mheshimiwa Anton Albert Mwantona ajiandae.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niwe miongoni mwa wachangiaji. Kwanza naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwaletea maendeleo wananchi wa Tanzania akisaidiana na Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wetu Mheshimiwa Majaliwa Majaliwa Kassim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee nampongeza sana Waziri wa TAMISEMI pamoja na wasaidizi wake wote wawili na Katibu Mkuu na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa ya kwenda kusimamia miradi ya fedha nyingi ambazo tumezipata kwenye Halmashauri zetu. Hongera sana Waziri na timu yako, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawaomba wananchi wako wa Jimbo lako watusaidie kuendelea kukuombea, nasi tunakuombea kwa kazi unayoifanya pamoja na wasaidizi wako kuwaletea maendeleo Watanzania. Hongera sana Mheshimiwa Waziri wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza *CEO* wa *TARURA* kwa kazi nzuri anayoifanya kusimamia kitengo hiki cha

*TARURA.* Kwa kweli mimi nasema Waheshimiwa Wabunge wenzangu, anafanya kazi nzuri na tunaomba sasa aongezewe fedha maradufu ili aweze kukamilisha kwenye Halmashauri zetu kufanya kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, pale upande wa afya, pale Mawande; Kijiji hiki cha Mawande ni kikubwa sana. Kina wakazi wengi sana, lakini hatuna zahanati. Wananchi wale wametoa eneo lao, wamesomba mawe, mchanga uko pale, naomba tupate fedha ili wananchi hawa waweze kujengewa zahanati ili waweze kupata huduma iliyo karibu zaidi, itapendeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile katika Kata ya Utengule eneo la Ikelu nao pia wamekusanya mawe mengi, wamekusanya mchanga, wametengeneza barabara mpaka kwenye eneo lilotengwa kwa ajili kujenga Kituo cha Afya. Naomba tupatiwe fedha ili wananchi hawa weweze kujenga Kituo cha Afya ili huduma iweze kuendelea kutolewa pale.

Mheshimiwa Spika, pia katika Jimbo langu la Makambako, Kata ya Mjimwema, katika bajeti hii tunayokwenda nayo, naomba sana tupewe fedha za kujenga sekondari katika Kata ya Mjimwema. Eneo wanalo, walishatenga, hawana fedha. Nakuomba sana tupewe fedha za kuanzia au za kutimia timu nzima ya kujenga madarasa ya shilingi milioni 600, utakuwa umetusaidia sana katika Kata yetu ya Mji Mwema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzangu wameongelea habari ya Madiwani, niliongea kipindi kilichopita, nirudie tena nami kusema. Madiwani hawa ndio wanaosimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao, wakisaidiana na Wenyeviti wa Vijiji, ndiyo mafiga yanakuwa yamekamiliika. Tunaomba sana katika mipango ya Waziri, tunaishukuru Serikali kwa kuwapa Bima ya Afya, ni jambo jema, wamefanya jambo jema zuri sana. Sasa mkae, muone namna ya kuwasaidia kuongeza posho za Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji ili timu hii

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uweze kusimamia vizuri fedha za maendeleo zinazopelekwa huko katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, na hili naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri. Sipendi kugombana na taasisi za dini. Kuna mtu mmoja nilimsikiliza juzi juzi hapa akielekezea namna ambavyo amesema kinapofika kipindi cha uchaguzi, CCM tunaiba kura. Nadhani wote mlilisikia hilo. Sasa nasema kwa uchungu mkubwa, mimi nimeshinda kwa kishindo, siyo kwa kuiba kura; na Waheshimiwa Wabunge wote hapa wameshinda kwa kishindo, siyo kwa kuiba kura na Rais alishinda kwa kishindo siyo kwa kuiba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu aliyozungumza maneno haya, anataka kutugombanisha na wananchi. Tumeshinda, ndiyo maana hata Jimbo la Sumbawanga tumeshindwa, ameshinda CHADEMA.

**MBUNGE FULANI:** Nkasi.

**MHE. DEO K. SANGA:** Nkasi, ameshinda CHADEMA. Kwa hiyo, kuelekezea jamii kwamba CCM wanaiba kura, siyo kweli. Tunashinda kwa kishindo. Watu wanakubali kwa sababu ya haya yanayotekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hivi kwenye maeneo yetu, Rais amepeleka miradi mingi, amepeleka fedha nyingi za maendeleo, watu wanakubali kwa kazi zinazofanyika, ndiyo maana wanatupa kura nyingi. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Haleluya!

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maana juzi wakati nachangia, nikasema Rais akakope tena fedha ili zifanye kazi ya kujenga nyumba za walimu; za watumishi, vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ndiyo nilisema siku ile hapa, ASAS wa Iringa ameunga mkono jitihada za mama, na ndio amesema anajenga darasa moja pale Makambako.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mbunge wa Mbarali naye akaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais, anajenga darasa moja pale Makambako. Haya ndiyo yanayofanya watu watuchague kwa sababu ya kazi zinazofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye mitandao, watu wameelezea jambo ambalo unashangaa. Wanasema, unaona Mama sasa anaongozwa Mheshimiwa Kikwete. Hivi ni kweli! Kwani Mheshimiwa Kikwete hakufanya kazi nzuri katika nchi hii? Awamu ya Nne Mheshimiwa Kikwete ndio watu walisema fedha zilijaa kwa wananchi, hakufanya Mheshimiwa Kikwete? kwani Mheshimiwa Kikwete ana matatizo gani? Tumwache apumzike vizuri kule Msoga. Tuache habari za kwenye mitandao, tuache Mama afanye kazi ya kuwaletea Watanzania maendeleo. Nimeona niliseme hili kwa hisia kali na kwa sababu watu wanataka kupotosha watu... *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga naomba ukae kidogo. Mheshimiwa Halima, Kanuni. *(Kicheko)*

### KUHUSU UTARATIBU

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, naomba utaratibu kwa kanuni ya 71 (1) (b) ambayo inasema: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayo..."

**SPIKA:** Kanuni ya ngapi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, ya 71(1)(b), "Bila kuathiri masharti ya Ibara 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge atazungumza jambo ambalo haliko kwenye mjadala."

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, tunajadili Wizara ya TAMISEMI, sasa naona anaanza kuzungumza mwenendo wa Rais na masuala ya uchaguzi. Sasa tukianza kufungua haya maneno ya uchaguzi na mwenendo wa Rais, nadhani tunaweza tukajikuta tunajitoa kwenye mjadala. Kwa sababu *whether* alishinda yeye ama hakushinda, anajua yeye na Jimbo lake. Kila Mbunge ana historia yake na Tume ya Uchaguzi ina majibu yake ya ukweli ama siyo ya ukweli. Hali kadhalika *whether* Mheshimiwa Kikwete anamsaidia Rais ama la, hiyo siyo ajenda hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nashauri, ni busara tungejikita kwenye mjadala wa TAMISEMI, azungumzie maeneo yake na maeneo mapana yote yanayohusiana naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hilo ili kutokutoka nje kidogo ya mjadala na kulielekeza Bunge lako liende kwenye mstari. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Halima Mdee kuhusu mchango aliokuwa akiutoa Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga ametupeleka kwenye Kanuni ya 71 inayozungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Yeye ameenda kwenye 71 (1) (b) inayozungumzia kwamba Mbunge hatazungumzia jambo ambalo haliko kwenye mjadala.

Waheshimiwa Wabunge, wakati Mheshimiwa Deo Sanga akichangia, alianza kwa kuzungumza kazi nzuri ambayo imefanywa na TAMISEMI; na katika kuelezea kazi hiyo nzuri, akaunganisha hoja yake ya kuashiria kwamba uchaguzi unapofanyika, watu wanakuwa wameziona kazi nzuri zinazofanyika katika maeneo yao. *(Makofi)*

Kwa muktadha huo, kwa sababu limezungumzwa hapa jambo linahusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, mchango wa Mheshimiwa Deo Sanga kwa namna yeye alivyoipanga hoja yake, amehusisha uchaguzi na yale yanayofanyika. Kwa hiyo, mchango wake uko sawa sawa.

Mchango wake uko sawa sawa kwa maana ya hoja yake namna alivyoiweka. *(Makofi)*

Sasa pengine kwa sababu nimeshasimama hapa, ameeleza kuhusu pengine ni kiongozi ama viongozi wa dini, mimi sifahamu, kwamba wamesema kura CCM inashinda kwa kuiba kura, kitu kama hicho; sasa kwa sababu mimi sijaona na wala sijasoma mahali popote, kwa hiyo, sijui kama walizungumza hayo wakiwa sehemu ya kuhubiri kwa maana ya Kanisani ama sijui ni wapi, ama kwenye mkutano wa hadhara ama sehemu nyingine. Hayo sasa ni Waheshimiwa Wabunge, tunatakiwa kuyapima kwa sababu pamoja na kwamba wamezungumza jambo ambalo ni la kisiasa na wakizungumza jambo la kisiasa, lazima wajibiwe kisiasa.

Vilevile wakizungumzia jambo la kidini, kidogo unakuwa unagusa zile hisia za imani. Kwa hiyo, hilo nalo nimeona nilifafanue ili isije ikaonekana kwamba sasa Bunge linaanza kijadili mahubiri ya viongozi wa dini mahali. Viongozi wa dini wakizungumza kuhusu siasa, maana yake watajibiwa kisiasa. Viongozi wa dini wakijikita kwenye mambo yanayohusu Imani, basi hayo tutawaachia kwa sababu ni uhuru wao na Katiba inawalinda kwa muktadha huo. Nadhani hilo litakuwa limeeleweka baada ya kutoa maelezo haya. *(Makofi)*

Bunge hili hatutafika mahali pa kuanza kujadili mambo ya dini kwa sababu Katiba yetu haijatutuma kusema hayo, lakini ikiwa kiongozi wa dini amezungumza mambo yanayohusu siasa; sasa nimesema hapa mwanzoni kabisa kwamba sijui kwa sababu sijaisikia, kwa hiyo, sijui yalizungumzwa katika muktadha gani? Ndiyo maana nimeweka huo mwongozo kwamba kiongozi wa dini akizungumza siasa atajibiwa kisiasa, kiongozi wa dini akizungumza dini aachwe azungumze mambo yake ya dini kwa sababu Katiba inamlinda.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, tunaendelea.

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**MHE. DEO K. SANGA:** Naomba nilindiwe dakika zangu.  
(*Kicheko*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ambacho nilikuwa nasititiza hapa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanga subiri kidogo. Kwa sababu hapa naambiwa kengele ya pili ilikuwa imeshagonga, kwa hiyo, nakupa dakika moja umalizie mchango wako.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Ambacho nakushukuru Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na timu yako kama nilivyosema, hakikisha wananchi wa Mawande wanapata zahanati; hakikisha Kata ya Utengule eneo la Ikulu wanapata Kituo cha Afya kutokana na kazi ambazo zimefanyika. Diwani wa eneo hili anafanya kazi nzuri sana pamoja na Madiwani wote wa Halmashauri ya Makambako.

Mheshimiwa Spika, naunga mkona hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Robert Chacha Maboto, atafuatiwa na Mheshimiwa Mheshimiwa Anton Albert Mwaintona na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ajiandae.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara ya TAMISEMI. Awali ya yote, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwenye Taifa letu ambapo mwezi wa Pili mwaka huu alipokuja Mkoa wa Mara pamoja na shughuli zote alizokuwa anazifanya, alizindua mradi mkubwa wa maji katika Mji wa Bunda.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo naiomba Wizara ya Maji ni kuhakikisha kwamba zile Kata 14 zote zinapata maji.kwa sababu mradi huu aliouzindua

Mheshimiwa Rais ulikuwa ni mradi wa fedha nyingi na wa muda mrefu. Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini, ni takribani kilometa tano kuona ziwa pale lakini maji bado yanatusumbua. Kwa hiyo, nawaomba watu wa Wizara ya Maji wahakikishe kwamba mradi huu unamaliza tatizo kubwa la maji ambalo tunalipata pale Bunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu fedha za UVIKO-19 ambazo kwenye Jimbo langu la Bunda Mjini lilipata takribani vyumba 51 vya madarasa ambavyo vimetekelezwa ndani ya miezi mitatu, na sasa vinafanya kazi, kwa sababu vimechukua watoto wetu kuingia madarasani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kikubwa ambacho nilitaka kukisema hapa ni kwamba watu wa TAMISEMI ni vizuri wakachukuwa mfano huu uliotumika kwenye hizi fedha za UVIKO-19, kuhakikisha kwamba miradi mingi ya vyumba vya madarasa inakuwepo kwenye Halmashauri zetu kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, hapo nyuma kabla ya fedha hizi za UVIKO-19 chumba cha darasa kilikuwa kinaweza kujengwa takribani miaka 15 ambapo leo kwa fedha hizi tumeona chumba hicho kinaweza kujengwa kwa muda wa miezi mitatu. Kwa hiyo, TAMISEMI pamoja na fedha zote hizi ambazo wanazipeleka kwenye Halmashauri, wao watoe kauli kwenye Halmashauri wakati wanapotuma fedha zao kwenda kutekeleza miradi kule.

Mheshimiwa Spika, watu wetu walioko kule chini uwezo wao wenyewe unaonyesha kwamba kujisimamia ni kazi, kwa hiyo, ni vizuri maelekezo mahususi yakatoka ili vyumba vya madarasa badala ya kujengwa kwa muda wa miaka 15 kumbe vinaweza kujengwa kwa miezi mitatu ili kupunguza tatizo hili; na kwa sababu vyumba vya madarasa vya kumalizia vipo vingi sana kwenye Halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa sababu bado inaendelea kutoa fedha kwa maana ya kumalizia



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

vyumba vile, lakini bado tatizo ni kubwa. Tunaomba TAMISEMI iendelee kutoa fedha ili vyumba hivyo viweze kukamilika na tatizo hili liendelee kupungua kwa kasi kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumzie kuhusiana na *TARURA*. *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana na hasa kwenye Jimbo langu la Bunda Mjini, muda mrefu uliopita barabara za mitaa zilikuwa hazipitiki kabisa; mitaro na barabara zake zilishaotea mpaka majani. Barabara ambayo magari yalikuwa yanaweza kuitumia Huwezi kuamini kama kuna gari lilikuwa linapita pale. Fedha tunazozipata zinapunguza tatizo, lakini bado tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililokuja kujitokeza kwenye suala hili la *TARURA* ni wale wakandarasi wetu wanaopewa miradi ile kuitekeleza kwenye Halmashauri zetu. Kwa mfano, Bunda Mjini pale, Mkandarasi wangu yule aliyepewa kazi pale, kasi yake bado ni ndogo sana. Vile vile fedha hizi za ujenzi wa barabara, leo unaambiwa barua ya kwanza fedha zimekuja shilingi milioni 150 kwa maana ya utekelezaji wa barabara za mitaa. Bado hizo hujajua zimeelekezwa kwenye barabara gani, kuna fedha zingine zimekuja.

Mheshimiwa Spika, bado hizo hujajua zimeelekezwa kwenye barabara gani kuna fedha zingine zimekuja. Wakati mwingine unapata wakati mgumu kwa sababu, siwezi kujua ni fedha zipi katika mradi huu na ni fedha zinazotekeleza mradi huu. Kwa hiyo, niwaombe watu wa *TARURA* wasimame vizuri na kwa sababu uwezo wa watu wetu hawa umeonekana bado upo chini, hivyo ni vizuri *TARURA* wao wenyewe wasimame imara kuzihakikisha kwamba fedha hizi zinafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais anatoa fedha kwa maana ya kuhakikisha kwamba barabara za mitaa zinakaa vizuri, halafu unapokuja kufika mwisho, atakapokuja kuangalia zile barabara akute wananchi wanamlalamikia kwenye maeneo hayo hayo, kwamba barabara hazitengenezwi, kumbe saa zingine fedha zipo na Mkandarasi

hajafanya kazi hiyo. Kwa hiyo ni jambo ambalo nawaomba *TARURA* wasimame vizuri hapa na Wizara hii ya TAMISEMI, wasimamie wakandarasi wetu vizuri ili waweze kutekeleza miradi yao vizuri ili iendane na thamani halisi ya fedha zile ambazo zinazotolewa na Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine hapa ni kuhusiana na vyumba vya madarasa. Vyumba hivi vya madarasa vimekuwepo kwa muda mrefu ambavyo wananchi wao wenyewe walivianzisha, tunaishukuru Serikali kwa sababu inakuwa ikitoa fedha kwa maana ya kwenda kupunguza tatizo lile, lakini bado tatizo ni kubwa. Tuiombe tu TAMISEMI iongeze fedha ili vyumba vile viweze kumaliziwa na kukamilika vyote ili watoto wetu wote waweze kusoma vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu vituo vya afya. Niishukuru TAMISEMI kwa sababu tumepata fedha hapa kwa ajili ya utekelezaji wa vituo vya afya, tumepata shilingi milioni 250 ambazo tulipeleka kule kwenye Kata yetu ya Waliku ambayo sasa tunaelekea kumaliza jengo lile. Niiombe tu TAMISEMI kwamba tutakapomaliza ujenzi wa lile jengo watulettee vifaa vile ambavyo vitaendana na lile jengo ili kwamba huduma ya afya iweze kutolewa kwa wananchi wetu wale, kwa sababu jiografia ya eneo lile Kata ywa Waliku ipo pembeni, wananchi kutoka kule waje Bunda Mjini ni takribani kilomita 16.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere na utoe taarifa kweli kwa sababu leo nitaanza na wewe, Mheshimiwa Getere, taarifa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa kwamba siyo tu kwamba wapeleke vifaa, ni kwamba tumepewa shilingi milioni 250 kujenga vituo vya afya na bado kuna milioni 50 inakuja. Kwa hiyo tunaomba watayarishie milioni 250 zilizobaki ziwahi mapema kumaliza majengo yaliyobaki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere wewe si ulipata nafasi ya kuchangia kuhusu eneo lako. Waheshimiwa Wabunge lazima tufahamu muda wa Utaratibu mimi ninao ni muda wangu hapa unaotumika, kwa sababu maana yake ni Kanuni zinavunjwa. Muda wa Taarifa ni wa Mbunge mwenzio, nadhani hilo pengine halijaeleweka vizuri ndiyo maana watu wanafanya hivyo. Kwa hiyo muda anaotoa taarifa Mbunge mwenzako ni muda wako wewe kwa sababu anakuongezea kwenye mchango wako na wewe Mbunge ufahamu, unapomsimamisha Mbunge mwenzio kuzungumza ukimpa taarifa ni kwamba unamwongezea kwenye mchango wake kwa hivyo unatumia muda wake.

Mheshimiwa Maboto.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na Mheshimiwa Getere kwa sababu tunatoka Wilaya moja taarifa yake naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hayo matatizo ya vituo vya afya ni pamoja na zahanati ambazo zimejengwa kule Mcharo na Kijambiga ambazo na zenyewe ziko kwenye hatua ya mwisho, ambazo tutaiomba TAMISEMI itusaidie kuzikamilisha vizuri na vifaa tiba viweze kupelekwa kwenye maeneo yake yale ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jiografia ya Mji wa Bunda hajjakaa vizuri sana na bado barabara zile za mitaa kama nilivyosema na zenyewe bado ni tatizo hasa barabara ile ya kutoka Guta kuja Kinyambiga, kutoka Kinyambiga kuja Kabasa, Kabasa kuja Bunda Mjini, hizo na zenyewe Wizara iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara baada ya kusema hayo, nakushuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anton Albert Mwantona atafuatiwa na Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu ajiandae.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nami pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya aliyotupatia. Pia nimshukuru Rais wangu, Rais mpendwa Samia Suluhu Hassan kwa yale ambayo anatufanyia kwenye Majimbo yetu. Nimshukuru mdogo wangu Waziri Mheshimiwa Bashungwa, Manaibu wake Mheshimiwa Silinde pamoja na Mheshimiwa Dugange, nimshukuru pia Katibu Mkuu wa Wizara hii Shemdoe Profesa. Vile vile pia nimshukuru sana sana *Engineer* ambaye ni Mkurugenzi wa *TARURA* Ndugu Seif, lakini pia kwa namna ya pekee sana nimshukuru *Engineer* wangu ambaye yuko kule Jimboni kwangu au Wilayani kwetu Rungwe ambaye anaitwa Kamara, anafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, leo kwa sehemu kubwa nitakuwa nashukuru maeneo mengi, lakini nitakuwa na changamoto moja au mbili ambazo naomba Waziri ambaye ni Waziri makini sana aweze kusikiliza kwa makini na aweze kunisaidia katika Jimbo langu la Rungwe. Kwanza nashukuru sana kwa kupandisha bajeti ya Mfuko wa Jimbo kwa asilimia 45. Mfuko wa Jimbo una mchango mkubwa sana kwa maendeleo katika Majimbo yetu. Kwa hivi nashukuru sana kwa kupandisha hii bajeti kwa asilimia 45, ila nashauri kwamba hizi pesa za Mfuko wa Jimbo zifike mapema zaidi kwenye majimbo yetu kwa sababu ni muhimu kuchoche maendeleo kule Majimbo.

Mheshimiwa Spika, pia kwa sababu pesa itaongezeka, naomba hizi pesa zije hata kwa awamu mbili, ije awamu ya kwanza mwezi wa Saba, lakini baada ya miezi sita hizi pesa ziweze kuja tena kuchochea maendeleo. Kwa sababu muda mwingi utakuta unakaa mwaka mzima hizi pesa zinakuja mara moja kwa mwaka kiasi kwamba wananchi wanasahau kwamba kuna vitu vingine vinatakiwa kufanyika. Naomba Mheshimiwa Waziri alichukue hilo, kwamba tuangalie kama tunaweza kupata hizi pesa kwa awamu mbili katika majimbo yetu ili majimbo yaweze kuchangamka mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la pili, nimeangalia kwenye utekelezaji wa bajeti ya mwaka jana kwenye

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

*TAMISEMI* bado mapato ya ndani kwenye halmashauri zetu siyo mazuri sana. Mwaka jana nilisema na mwaka huu naongea tena kuna chanzo kimoja cha mapato katika halmashauri zetu ambacho kipo *very potential* na kama tutakisimamia vizuri tunaweza tukaongeza mapato katika halmashauri zetu. Chanzo hicho ni *service levy, service levy* inakusanywa inafanana na Sheria ya *TRA* ambayo ni kodi ya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama tukishirikiana na *TRA* vizuri, tukafanya *assessment, TRA* wanafanya *assessment* zao na *service levy* wakafanya *assessment* kwa pamoja kama *parallel* tunaweza tukaongeza mapato kiasi kikubwa sana kwenye *service levy* na tukaongeza mapato ya Halmashauri zetu kwa kiasi kikubwa.

Naomba hilo lizingatiwe na Waziri aweze kuli-*note*, washirikiane na *TRA* kuhakikisha wanapo-*produce* zile *assessments* za *TRA* kwenye kodi ya mapato wa-*produce* pia *assessments* za *service levy* katika halmashauri zetu ili kuongeza mapato katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo natoa pongezi kwa Wizara ni kuanzia mfumo wa kielektroniki katika kusimamia Mifuko ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu. Hilo nawapa pongezi, naomba wakalisimamie kwa karibu kuhakikisha kwamba mambo yanayofanyika katika halmashauri zetu katika ngazi za *TAMISEMI* pia wanaweza wakayaona na wanaweza wakayashauri.

Mheshimiwa Spika, naomba niende kwenye afya. Mwaka huu wa fedha tumeletewa zaidi ya milioni 500 kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya Kiponjora, tumeletewa milioni 250 kwa pesa za tozo tunajenga Kituo cha Afya Ndanto, lakini tumeletewa bilioni 1.39 katika Hospitali yetu ya Wilaya Rungwe ambayo inaitwa Makandana. Milioni 300 ujenzi unaendelea, ilikuwa ni kwa ajili ya jengo la *emergency*, milioni 90 ujenzi unaendelea kwa ajili ya jengo la wafanyakazi, lakini bilioni moja kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa majengo pale katika hospitali yetu.

Mheshimiwa Spika, nilivyokwenda kwenye kampeni mwaka uliopita walinisitiza sana na walinitwisha jiwe kichwani ambalo linasema kuna matatizo makubwa ya kiutendaji katika Hospitali yetu ya Wilaya. Haya ni lazima niyaseme kwa sababu ni mwakilishi wa wananchi, matatizo ambayo nayapata katika maeneo yao lazima niyalete hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Naibu Shaka Abdul Shaka ambaye ni Mwenezi Taifa alikuja kutembelea pale kwetu, alitembelea kata tatu, alitembelea Kata ya Kiwira, Bagamoyo na Mpuguso, matatizo yote anayoeleza ni matatizo ya *service* ya pale katika Hospitali ya Wilaya ya Rungwe. Kuna matatizo makubwa sana, mimi mwenyewe nimefanya ziara kwenda kushukuru kwa wananchi, akinamama ndiyo waathirika wakubwa na wengine wanaambiwa kabisa kwamba bwana nenda ukamwambie Mama Samia hapa hatuna madawa.

Mheshimiwa Spika, tunajua kuna matatizo *MSD*, tumeambiwa hapa Bungeni, lakini kuna lugha za kuwajibu wananchi, ili tuwaambie wajue kwamba Serikali inapitia matatizo fulani ambayo tunayajua *MSD* kuna shida. Nampongeza Mheshimiwa Rais kwamba amebadilisha Mwenyekiti pamoja na Mkurugenzi *MSD*, hiyo napongeza sana kwa sababu tunategemea huko mbele ya safari tunapokwenda, tunakwenda kufanya marekebisho katika huduma zinazopatikana katika hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba kama hatutafanya marekebisho katika huduma zinazotolewa katika hospitali zetu nchi nzima, majengo tunayojenga ni bure, hayatatusaidia chochote, lakini kuboresha majengo na miundombinu mbalimbali inayofanyika katika hospitali zetu kwenye maeneo mbalimbali ni lazima yaende na elimu kwa watumishi wetu, tuwaambie wanatakiwa watoe *service* inavyotakiwa wananchi waweze kunufaika na matunda ambayo tunayapeleka katika maeneo yetu.

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu, wananchi watamlaumu bure Mheshimiwa Rais kwa sababu tu kwamba tunajenga majengo lakini hakuna *service* inayopatikana.

Kwa hiyo, naomba sana sana Waziri Mheshimiwa Bashungwa nafikiri nimeshamwona, waende wakafanye marekebisho kwenye Hospitali ya Wilaya ya Rungwe, tupate huduma zinazotakiwa kwa wananchi wa pale Rungwe ili tuondoe malalamiko ya wananchi ambapo kila siku wanalalamika kwamba huduma zinazopatikana hapa hazitoshelezi.

Mheshimiwa Spika, nimalizie upande wa barabara. Nimempongeza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, kengele ya pili.

**MHE. ANTON A. MWANTONA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Waziri kwa sababu TAMISEMI ni kubwa sana, haya malalamiko ya Mheshimiwa ya Mbunge mfanye uchunguzi kabla ya kufanya maamuzi kuhusu watumishi wa hiyo hospitali, kwa sababu wakati mwingine inategemea umekutana na nani anayelalamika kuhusu jambo fulani, anaweza akasema hapo na maneno yasiyohusika kabisa. Kwa hiyo kabla hamjachukua hatua kama mtachukua hizo hatua mfanye kwanza uchunguzi kuhusu hao watumishi waliyoko pale Hospitali.

Vivyo hivyo na sehemu nyingine kwa sababu TAMISEMI ni kubwa, mkisikia malalamiko kuhusu mtu fulani au sehemu fulani lazima mjiridhishe kwa sababu TAMISEMI ni

kubwa sana, upo uwezekano wa watu kusema maneno ambayo pengine mtu alimchoma vibaya sindano na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Pia niwashukuru sana Wizara ya TAMISEMI kwa kiunganishi kizuri wanachokifanya kwa wananchi wetu na kutufanya sisi Wabunge tuendelee kutiza majukumu yetu. Nitoe vile vile pongezi kwanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa utekelezaji mzuri ambao unaendelea kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nina mambo matatu. La kwanza nianze kuwapongeza sana *TARURA* kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanayoifanya kwenye maeneo yetu. Tulipiga kelele Bunge lililopita tukiona *TARURA* hawana uwezo, lakini baada ya kuwapelekea uwezo kila mtu ameona kazi wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwenye Mkoa wangu wa Simiyu, *TARURA* tuna maeneo makubwa ambayo yanatoa huduma hiyo, lakini changamoto kubwa ya kwanza ambayo Mheshimiwa Waziri na jopo lake niwaombe sana, hawana usafiri wa kutekeleza majukumu yao kwenye Mkoa wetu wa Simiyu. Meneja wa Mkoa anasubiriana na Mameneja wasaidizi kwenda kutekeleza majukumu na fedha wanazileta kwenye maeneo yetu. Tumeona kwenye Jimbo langu la Itilima wametuunganishia katika vivuko, eneo la Nhamango lipo kwenye mpango, Mnamala Mbugani wameshatoa fedha ujenzi unaendelea, Tagaswa ujenzi unaendelea na maeneo mengine mengi kwenye Jimbo langu ambayo yanaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ombi langu, unapokuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Itilima na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu analijua sana eneo la Mkoa wa Simiyu, unapoizungumza Itilima mtu anapotoka Golambesi kwenda Makao Makuu ya



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mkoa inabidi azunguke kwenda Makao Makuu ya Wilaya ambayo ni kilomita 110 na kuna Daraja la Nyangokorwa linaungana na Wilaya ya Bariadi, wakitutengea fedha kivuko kile kikatengenezwa, wananchi wetu hawa hawatatumia gharama ya kwenda kilomita 110 kwenda kupata huduma ya kiafya kwa maana Hospitali ya Rufaa pale Nyaumata. Kwa hiyo nikuombe sana mratibu wa *TARURA* utusaidie katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunapakana na Wilaya ya Magu na tunapakana na Jimbo la Sumve, kuna kivuko kinaitwa Solo ambako barabara imelimwa mpaka kwenye kivuko ukifika pale kulingana na bajeti tulizonazo ukomo unakuwa ni kidogo. Kwa hiyo wananchi wanaotaka kwenda Mwanza inabidi warudi kilomita 120 na ukitoka tena kilomita 120 kwenda Mwanza kilomita 200 jumla 320, lakini angetokea pale Solo kwenda Mwanza angetumia kilomita 95 akawa ameshafika na kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunayo ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni Mto Gomalong unaunganisha Kata ya Nkulu, Kata ya Mwaswale na Kata ya Laini. Nimwombe sana, maombi haya yamekuwa ya muda mrefu, yachukuliwe yafanyiwe kazi ili wananchi wanaoishi kandokando ya maeneo hayo waweze kupata huduma safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ningepomba sana kwenye mtandao wa barabara kwenye Wilaya yangu ya Itilima ulioingia ni mia tano na thelathini na kitu lakini mpaka sasa tuna mia nane na kitu, kwa hiyo 256 hazipo kabisa kwenye mtandao wa barabara na wananchi, wasamaria wema wamejitolea kufungua barabara. Ningeiomba Serikali, maeneo hayo yaingizwe kwenye mpango ili wananchi waweze kupata huduma inayostahili kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, wanapotufungulia barabara hasa Wabunge tunaotoka vijijini huko, wanaongeza uchumi na wanapunguza kasi ya gharama ya usafiri kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, niwaombe sana, lakini kuna miji inakuwa kwa kasi, nina Mji unaitwa Laini, nina Mji unaitwa Migato, nina Mji

unaitwa Luguru na Nyamalapa. Maeneo haya yanahitaji kupanuliwa kwa kuwa na barabara. Sasa kulingana na bajeti ya *TARURA* inayokuja tungeomba kama kuna uwezekano iongezwe ili wananchi wa Wilaya ya Itilima waweze kuneemeka na Serikali ya Awamu ya Sita. Maeneo haya niliyoyataja yana uchumi mkubwa wa kichochezi kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo niombe sana Serikali iendelee kutusaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ni mpya, tuna kilomita moja ya lami ambayo imepangiwa, lakini pamoja na haya tuna eneo ambalo kutoka Makao Makuu kwenda kwenye Hospitali ya Wilaya na barabara zetu ni za vumbi na kwa sababu tunatengeneza afya, ningepomba *TARURA* kupitia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri atusaidie sana maombi maalum, kwa sababu ni hospitali imejengwa kwa gharama kubwa, sasa huduma ya barabara kwenye hili inapokosekana tayari kunakuwa na changamoto kubwa sana. Tuendelee kuomba watutengee angalau lami kilomita tano kwa kila mwaka, itatusaidia sana kuhakikisha wananchi wa eneo hilo kuelekea Nguno mpaka Nanga itatusaidia sana kuhakikisha kwamba eneo hilo limekaa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la afya; Wabunge wenzangu wamezungumza humu Serikali inawekeza fedha nyingi sana inawekeza kwenye vituo vya afya, zahanati kwenye hospitali. Sasa ni jambo ambalo ni la kusikitisha, tunaweka miundombinu yenye gharama na kilio chetu kikubwa kila Mbunge anayesimama tunalalamikia mambo ya afya.

Sasa najjuliza tunapozidi kuendelea ku-*invest* lakini bado tuna changamoto kwenye maeneo haya mengine, mfano kwa Itilima tuna Hospitali ya Wilaya mwaka jana tumetengewa milioni 500 tumelipa *MSD* lakini fedha hiyo bado hata, zimekuja *items* tano tu, sasa utajuliza kwamba ni kitu gani tunachoendelea kukifanya katika maeneo yetu haya. Badala ya kuwa na kipaumbele tunaanza jambo moja tunamaliza tunahamia jambo lingine. Sasa nalo kama Serikali

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

walichukue walifanyie kazi hasa kwenye maeneo hayo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ninacho Kituo cha Afya Zagayu, ni cha muda mrefu, kimechakaa na hakina wodi ya wazazi, watoto na akinababa wala hakina maabara. Sasa yote hiyo ni changamoto, ningeomba sana Serikali iangalie sana maeneo hayo muhimu ili iweze kutuunganisha na wananchi waendeleo kupata huduma safi ili mambo yaende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Wizara ya TAMISEMI wanatakiwa walifanyie kazi, sisi hapa tunakuwa tunatenga bajeti. Tunatenga kwenye mifuko yetu ya kilimo, kahawa, tumbaku, pamba na kadhalika, vitu vingi. Hata hivyo, katika hali ya kawaida, tukiangalia yale mazao yetu muhimu tukatengeneza kiwango cha fedha, wananchi wetu tuna mpango wa kuwa na Bima ya Afya, kwenye yale uzalishaji unaozalishwa kila Taasisi, bodi inayozalishwa tukakata *percent* fulani tukawapelekea wananchi, tukapeleka bima kwa afya bure, kwa maana yake yule mwananchi atakuwa amechangia kutokana na mazao yake aliyoyazalisha, atakuwa anakwenda hospitalini kwa sababu ataamini akifika pale atapata matibabu, atahudumiwa na atatoka yuko salama.

Mheshimiwa Spika, leo tunatenga kwenye tumbaku, tunatenga kwenye pamba, tunatenga kwenye korosho; mazao yote ya kimkakati tunayatengea fedha kwenda kulima. Analima huku mtu mgonjwa baada ya kumtengea fedha hizo zikamsaidia huko mbeleni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Nianze kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mawaziri wake wote wanaomsaidia, Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Manaibu pia kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa kuwahudumia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia kwa kuanza na TAMISEMI. TAMISEMI ambayo ndiyo Wizara tunayoichangia na kwenda kuanza na *TARURA*. *TARURA* inafanya kazi nzuri sana katika kipindi hiki ambacho imepewa fedha baada ya sisi Wabunge kusema sana katika Bunge hili. Kumekuwa na changamoto, tumepewa fedha shilingi bilioni 1.5 iliyotolewa na Mheshimiwa Rais na tulitangaziwa kwenye Bunge hili. Hata hivyo, naweza kusema wakandarasi ambao wamepewa kazi katika kipindi hiki hasa kwenye jimbo langu kuna changamoto kubwa.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu imekuwa ikileta matatizo makubwa kwa wananchi kwa sababu tangu mwaka jana fedha zipo kwenye akaunti wakandarasi wamepewa kazi, wakandarasi ni dhaifu, hawafanyi kazi, matokeo yake wananchi wanalalamika usiku na mchana. Hapa ninapozungumza wananchi wa Kata ya Kihutu wameandamana ambao tumewaambia kwenye mikutano kwamba barabara inatengenezwa toka mwaka jana, wanasema, Mheshimiwa Rais utusaidie Mkandarasi hayupo kazi, wanaona sisi ni waongo, hatufanyi kazi, tunawadanganya kwenye mikutano ya hadhara, wakati Serikali imeshatoa fedha, lakini udhaifu wa wakandarasi. Naomba *TARURA* waliangalie jambo hili kwa sababu wanatudhalilisha. Fedha za *UVIKO* zimekuja juzi tu miradi ilishatekelezwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu ya usimamizi mzuri. *TARURA* wanafanya kazi nzuri lakini wakandarasi wanawaangusha, hawafanyi kazi na sisi wanatudhalilisha.

Mheshimiwa Spika, naomba pia katika mgao wa fedha za *TARURA* kwa majimbo tuangalie kwa sababu kuna majimbo ambayo ni magumu sana kama Jimbo langu la Arumeru Magharibi. Jimbo langu la Arumeru Magharibi lina makorongo, barabara zake zote ni mbovu, kwa hiyo naomba

katika mgao watuangelie kwa jicho la huruma kwa sababu wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi na majimbo mengine makubwa, kwa kweli wanahitaji fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara zinatengenezwa. Barabara katika Jimbo langu ni kilometa 685 za changarawe. Sasa kwa fedha ambazo tunazipata ni kidogo sana kwa hiyo naomba mtuangelie.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye ahadi za Rais ambazo Mheshimiwa Rais amezitoa katika Jimbo la Arumeru Magharibi na katika majimbo mengine yote. Naomba ahadi hizi ambazo zinatolewa na Mheshimiwa Rais ziangaliwe sana kwa makini na Waheshimiwa Mawaziri katika kuingiiza kwenye mipango yao. Kwa sababu mwisho wa siku Taasisi ya Rais inaonekana kwamba haiheshimiwi na wananchi pale inapotoa tamko kwamba itatekeleza jambo fulani, kwa mfano, Mheshimiwa Rais kwenye Jimbo langu ameahidi ukarabati na marekebisho makubwa kwenye Hospitali ya Wilaya ambayo yeye ameizindua, kwamba itaongezewa majengo, itawekwa na kila kitu lakini tangu Serikali ianze kugawa fedha za Hospitali za Wilaya, Hospitali hiyo ya Wilaya ya Oturumeti Arusha *DC* haijawahi kupata hata shilingi moja kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aniambie ni lini atapeleka fedha kwa ajili ya kuboresha hospitali hiyo. Vinginevyo nitashika mshahara wake kwa sababu wale wananchi wa Jimbo la Arumeru Magharibi nao wana haki katika mgao wa fedha za hospitali. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, suala la kujenga barabara kilomita tatu katika hospitali hiyohiyo, Rais ametoa ahadi hiyo hadi leo hakuna namna ambayo kuna namna ambayo wanatekeleza ahadi hiyo ya Rais. Siyo kwangu tu na kwa majimbo mengine yote, lazima sasa wafike mahali Mawaziri wote ahadi za viongozi wetu ambao wanazitoa kwa kuwajengea heshima na hasa Taasisi ya Rais ambaye ndiye msemaji wa mwisho katika Taifa hili na ndiyo tumaini la wananchi anaposema jambo lazima zitekelezwe. Kwa hiyo

naomba ahadi za Rais ziwekwe kwenye kitabu maalum kitakachoonyesha kila Bunge kwamba zinatekelezwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna zahanati ambazo hazijakamilika mmetuma milioni 50, lakini bado tunaomba TAMISEMI warudie tena kutoa fedha kwa ajili ya zahanati hizo na vifaa tiba pia.

Mheshimiwa Spika, posho za Madiwani na Wenyeviti wa Vitongoji; hawa watu wanafanya kazi kubwa sana kwenye majimbo yetu na kwenye halmashauri zetu. Wao ndiyo wanasimamia miradi yote, wao ndiyo wanasimamia llani ya Chama cha Mapinduzi lakini kwa mshangao mkubwa tunasema tunawapa posho. Ifike mahali sasa Madiwani hawa wapewe mshahara kama watu wengine, wanafanya kazi kubwa. Kuna zile shilingi 350,000 ambazo wamesema wametoa shilingi 100,000 kwa ajili ya kuwapa watendaji, hizi fedha nazo waziweke kwa ajili ya Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji waweze kupata posho. Serikali sasa iangalie Madiwani kwa sababu wanateseka, hawana uwezo wa kuwasimamia watu wanaolipwa shilingi 700,000 au shilingi 800,000 na wao wanapata mshahara lakini wao wanafanya kazi kama wanafanya bure, halafu tunawatumaini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nakwenda kuingia kwenye eneo la chakula mashuleni. Tunasema watoto wafaulu, ni mtoto yupi anaweza kukaa kuanzia asubuhi hajala chochote lakini unategemea afanye vizuri au amsikilize Mwalimu? Naomba eneo hili TAMISEMI waliangalie na watoe waraka maalum na unaoelekeza namna ya watoto kupata chakula shuleni kwa lazima, kwa sababu ndiyo tunatengeneza Taifa la watoto ambao wanakuwa na *kwashiorkor*, kwa sababu haiwezekani mtoto kukaa kuanzia asubuhi bila kula chakula alafu tunaona ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, suala la mfumuko wa bei. Kule vijijini kwa sasa hizi hali ya vyakula, vitunguu, nyanya, chumvi, mafuta ya kula, hali ni tete. Kwa hiyo naomba waende waangalie Serikali watoe namna kwamba kuna

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wafanyabiashara baadhi ambao wanapandisha bei eti tu kwa sababu wamesikia mafuta yamepanda. Naomba Serikali ifanye uchunguzi ili iwape wananchi maelezo na matumaini ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, suala la bajeti hii kutekelezwa. Lazima bajeti hii itekelezwe bila kuwepo na wizi, rushwa, ufisadi na ujanja ujanja. Bajeti kitekelezwa bila rushwa tutatekeleza vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kila mmoja achukie rushwa, wizi na ufisadi ili mwisho wa siku Taifa hili lipone. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge huyu alikuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa kipindi chetu cha kwanza, wengine watachangia mchana. Niwataje Wabunge ambao wataanza kuchangia; Mheshimiwa Ally Juma Makoa, Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, Mheshimiwa Jonas William Mbunda na wengine wataendelea kutajwa kadri muda unavyoenda na Mheshimiwa Grace Tendega.

Waheshimiwa Wabunge, imezungumzwa hoja hapa kwa kirefu sana, hoja ya maslahi ya Waheshimiwa Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji na kwa sababu nadhani kimsingi sote tunakubaliana kwamba wanafanya kazi nzuri sana.

Pengine katika hao wote tuliowataja Wenyeviti kwa kweli usiku wa manane aamshwe mgonjwa, kuna msiba, kuna changamoto fulani hivi, usuluhishi. Kwa hivyo nafikiri hoja imezungumzwa kwa kirefu sana hapa, Mheshimiwa Waziri lakini sasa kwa mujibu wa Kanuni zetu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Kamati itaichukua hii kama mojawapo ya hoja zitakazojadiliwa baada ya kuhitimisha mjadala wa Wizara zote za Fedha ule muda tutakapokuwa tunajadiliana hoja zilizojitokeza, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti wachukue hii kama mojawapo ya hoja hizo ambazo zinatakiwa kufanyiwa kazi kwa maana ya maslahi ya Wenyeviti na Waheshimiwa Madiwani. *(Makofi)*

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe jambo moja, ni muhimu sana Mbunge unaposimama utazame anayezungumza yupo upande gani ili usipite katikati ya Kiti na huyo anayezungumza, ndiyo Kanuni zetu zinatumika hivyo. Kwa hiyo tuzingatie Kanuni yetu 73 kwa sababu leo amepita Naibu Waziri mmoja katikati mwenzake anajibu swali hapa, Mbunge anayeuliza swali yuko upande mwingine yeye amepita katikati. Waheshimiwa Wabunge kama watatu hivi majina pia yako mbele hapa na wao wanakatiza tu, usimame kabla hujajua anayezungumza yuko upande gani.

Lingine usigeuze kiti, usikipe Kiti mgongo, hilo nalo limeshaelezwa mara kadhaa, niwakumbushe, viti vyetu vinazunguka kwa maana ya wewe kuzungumza na jirani lakini hakikisha namna kiti kimekaa usikipe kiti mgongo yaani usigeuze kiti kwamba wewe unaangalia upande ule. Kwa sababu ndiyo maana viti vyetu vimekaa kwa namna ambavyo mimi lazima nione kila mtu aliyeko humu ndani. Maana unaweza ukasingiziwa jambo kumbe wewe uliangalia kule na kiti na wewe ulikuwepo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi kamili Jioni leo.

*(Saa 7.18 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Tunaendelea na majadiliano. Mchangiaji wetu wa kwanza kama ilivyotangazwa wakati ule atakuwa ni Mheshimiwa Ally Juma Makoa, akifuatiwa na Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo, wakati huo huo Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Nami nianze kuchangia kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake yote kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM na utekelezaji mzuri wa bajeti hii ambayo tunaendelea nayo. Pia



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nawapongeza Mawaziri na TAMISEMI wote kwa ujumla kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa ajili ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukiwapongeza hapa, kutokana na muda wetu hatutakamilisha shukrani kwa sababu kwa kweli TAMISEMI katika bajeti hii wamefanya vizuri sana. Nimepitia utekelezaji kwa kuona kwa macho yale yote ambayo tuliyaomba, bajeti hii tunayoendelea nayo kwa kweli asilimia karibu 99 wameyatekeleza na miradi inaendelea kutekelezwa kwenye Jimbo langu kwenye Kata zote. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika bajeti hii inayoendelea, naomba mambo machache; moja, ni kwamba kuna shilingi milioni 130 zile kwa ajili ya ile Sekondari ambayo tunaendelea kujenga. Pale kwenye Jimbo langu ile Sekondari ni kama imekamilika kwa sababu Naibu Waziri wa Elimu alipita juzi akaelekeza tuanze usajili. Kwa maana hiyo aliridhika na kiwango cha ujenzi wa ile Sekondari, na ninawakaribisha mje mwone namna watendaji wamepambana, ile Sekondari imekamilika na natarajia tuanze kuitumia mwezi wa Saba. Kwa hiyo, ile shilingi milioni 130 tunaomba ije kwa wakati ili tuweze kukamilisha katika kipande chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upande wa bajeti hii tunayoendelea nayo, tunashukuru Serikali ilitupa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara mbili katika kila Sekondari, lakini tukumbuke kila Sekondari ina maabara tatu. Sasa tunamalizia majengo mawili na bahati nzuri huwa yanafuatana, linabaki moja. Kwa hiyo, tunaomba zile za ukamilishaji wa maabara ya tatu katika Sekondari na zenyewe zifanyiwe kazi mapema ili watoto wetu waweze kusoma kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika bajeti hii tunayoendelea nayo, tatizo la walimu ni kubwa, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumza lakini sasa hapa nina ushauri kwamba, hebu wale walimu ambao wapo

tayari mashuleni wanajitolea, wawe ni wa kwanza kuajiriwa kwa sababu unakuta wale walimu ambao wapo mashuleni na wamejitolea kufundisha wanakosa ajira lakini anapewa ajira mtu mwenye elimu, lakini kipindi hicho chetu usikute yuko kwenye maeneo tofauti ya kutafuta riziki, tunawaacha wale ambao wamejitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukianza na wale, maana yake hata shule zetu zitakuwa hazina upungufu wa walimu kwa sababu walimu wataona tukijitolea itakuwa ni kipaumbele katika kupewa ajira. Kwa hiyo, tujitahidi katika hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya kwenye *TARURA*, nadhani tumefanya vizuri, lakini maeneo yetu ya mijini ambayo tunaratajia huo mradi wa *TACTIC*, ni vyema sasa nasi tukawahisha. Tumepewa shilingi milioni 500, lakini maeneo mengine wamepewa shilingi bilioni moja kwa sababu tunatarajia tutapata huo mradi wa *TACTIC* kwa ajili ya barabara zetu za mijini; lami pamoja na taa na ujenzi wa stendi. Sasa tunatamani wananchi wajue, tunawaeleza kwamba tuna mradi huu utakuja, lakini sasa tufafanuliwe ni lini hasa tutaanza mradi huu katika Halmashauri zetu za Miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipitia bajeti hii ambayo sasa tunakwenda kuipitisha, nimeona yale ambayo mmetuwekea, tunashukuru na tunaona ni katika yale yale ambayo ni matarajio ya Wabunge pamoja na wananchi wanaowawakilisha. Hapa naomba Mheshimiwa Waziri alinukuu jambo hili liwe kama dharura kwake. Tuna Shule ya Msingi inaitwa Iboni. Nimeona hapa kuna fedha kwa ajili ya kukarabati shule zilizochakaa, lakini shule hii imechakaa *over kuchakaa*. Leo hata ukiwa na feni tu ukasema upulize kwa kasi kubwa, bati zote zile zinang'oka. Shule ile imejengwa miaka mingi sana; wamesoma babu zetu na baba zetu. Sasa hii siyo tu ku-*repair*, hii inahitaji madarasa ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu *special* zaidi, shule hii ina wanafunzi wa kawaida, lakini pia ina wenye mahitaji maalum na ndiyo shule pekee yenye watoto wenye uhitaji

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

maalum. Pale wapo wasio na usikivu, wasioona, wenye mtindio wa ubongo. Bahati mbaya madarasa yao mawili yote yameanguka, leo wanasoma chini ya mikwaju, na hawa watoto ni maalum kabisa. Naomba jambo hili na lenyewe katika ile idadi ya madarasa, basi japo tupate madarasa yao mawili, ni muhimu sana kwa sababu watoto hawa ni wale wa uhitaji maalum. Kwa hiyo, natarajia Mheshimiwa Waziri atalichukua hili kwa msisitizo wake na tutawasaidia watoto wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tena kuishauri Serikali kwamba sasa hivi tu-*invest* pia kwenye hosteli. Katika Halmashauri ya Mji, hatuna Sekondari hata moja yenye hosteli, lakini tunaona watoto wanashindwa kumaliza shule kutokana na mwendo wanaotembea. Wanaweza wakaanza shule watoto 60, wakamaliza 40, wengine wote wanaishia njiani. Kwa hiyo, nashauri, nami angalau pale Halmashauri ya Mji tupate japo hosteli, kuwe na sekondari japo moja yenye hosteli iliyokamilika, hasa hii sekondari mpya ambayo mmetuletea, ni shule ya kisasa sana, tukijengea mabweni, kwa kweli itakuwa ni *overshule*; itakuwa ni shule zaidi ya shule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nigusie kidogo kwenye upande wa Madiwani. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI hawa Madiwani wanatakiwa wote wapewe heshima inayofanana. Bahati mbaya, sasa sijui ndiyo maelekezo ya TAMISEMI, kuna baadhi ya maeneo ya Halmashauri Madiwani hawa wanakuwa hawapewi thamani kama ile thamani ambayo Madiwani wa sehemu nyingine wanapewa. Mfano, unakuta Diwani anatoka kilometa 30, anakodi pikipiki shilingi 15,000/=; kwenda na kurudi ni shilingi 30,000/=; akifika kwenye Kikao anapewa posho ya shilingi 40,000/=. Kwa maana hiyo, Diwani huyu kweli anawezaje kwenda kutekeleza majukumu yake kwa kupewa posho ya shilingi 40,000/= ? Ukiuliza, tunaambiwa ndiyo mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue, ni kweli TAMISEMI mmewaongoza wao kuwalipa Madiwani posho shilingi 40,000 wakati Halmashauri nyingine wanalipwa

kutokana na stahiki halali? Wengine wanalipwa posho shilingi 100,000/= na zaidi, lakini Halmashauri nyingine ikiwemo Halmashauri yangu, posho shilingi 40,000/= Diwani anatomia nauli kwenda na kurudi shilingi 30,000/=, itakuwa siyo sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine utaona kwamba Wabunge wengi wamechangia kwamba Madiwani waongeze maslahi, ni kwa sababu mmepeleka fedha nyingi sana kule kwenye Kata ambazo zinasimamiwa na Madiwani, halafu Diwani unampa shilingi 40,000 au unampa shilingi 300,000 anakwenda kusimamia fedha nyingi, matokeo yake Madiwani wetu wanakata tamaa na wanakuwa hawafanyi kazi kwa ufanisi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi sana nilitaka nielezee jambo moja. Kulikuwa na mchangiaji ambaye alizungumzia ujenzi wa stendi na soko la kisasa ambalo limejengwa Dodoma hapa; na wakasema yamejengwa mbali. Naipongeza Serikali na niipongeze sana TAMISEMI kwa kujenga yale masoko na stendi, kwa sababu leo soko kama lile na stendi kama ile, mjini hapa katikati unaweza ukalijenga sehemu gani ukalipata? Kujenga maeneo haya pembezoni mwa miji, maana yake mnakwenda kuutanua mji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi leo wakitaka kununua viwanja katika Dodoma hii, hawawezi kununua huku, wanakwenda kununua Mtumba na maeneo kama hayo. Maana yake ni nini sasa? Mji unakua na watu wanapata fursa. Hapa cha kusaidia ni kwamba, Jiji letu la Dodoma linapaswa viwanja vile vinavyozunguka soko na stendi wagawiwe wananchi wajenge ili lile soko na ile stendi iwe na thamani. Wasifanye tena vile viwanja vikawa ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya *public*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwapongeze na niwape hongera; tumekwenda Nyamagana kule llemela, tumekuta stendi moja ya kisasa sana. Kwa hiyo, kama kuna mpango huu, hata Kondoa tuna uhitaji wa stendi, na tumeisogeza pembeni ili kuukuza mji. Nawaomba sasa Wizara

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya TAMISEMI katika maeneo, na tunajua Kondoa ipo katikati ya Manyara na Dodoma. Kondoa ipo karibu na Makao Makuu ya nchi. Kwa maana hiyo, tukipata na ile stendi yetu ambayo tumeiandaa pale pembezeni mwa mji, mtasaidia kukua kwa mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninashukuru sana na ninawapongeza Wizara. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Juma Makoa. Sasa namwita Mheshimiwa Abeid Ramadhani Ighondo aweze kuchangia.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi. Nami nichukue fursa hii kwanza kwa kuanza kuwatakia heri Waislam wote ambao wapo kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, na niombe kwa Mwenyezi Mungu atupokelee funga zetu na dua zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii pia kupongeza uwasilishaji mzuri wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, lakini pia niwapongeze vijana wenzangu hawa; Waziri pamoja na Manaibu Waziri wote wawili. Ni vijana wachapa kazi, nami nasema upele umepata mkunaji. Kazi kubwa kwenu ni kuingia *field*, kutokukaa ofisini, njooni mtukute kule Singida Kaskazini mwone kazi nzuri tunayoendelea kuichapa kule ambapo kimsingi inatokana na uwezeshaji ambao nyie mnaoufanya huku Wizarani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya kipekee naomba nichukue fursa hii kuwasilisha shukrani na pongezi nyingi za wana Jimbo la Singida Kaskazini kwa fedha nyingi walizoletewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi wa yale mabilioni tuliyosema ya Mheshimiwa Samia. Nashangaa watu wanasema fedha za UVIKO; zile siyo fedha za UVIKO, yale ni mabilioni ya Mheshimiwa Samia. Naomba hilo lirekebishwe. Tumepata fedha nyingi ambazo zimetuwezesha kujenga madarasa 67, Shule Shikizi pamoja na Sekondari. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza mwaka huu, wanafunzi wote wameripoti shule kwa awamu moja, tena wakiwa wamekaa kwenye madawati. Tumepata madawati zaidi ya 2,500, sasa haya kwa mwaka huu hata wazazi wamehamasika kuwapeleka watoto wao shuleni. Maana watu walikuwa wanahamasisha watoto wasiende shule. Mtoto anafaulu lakini anaambiwa asiende shule kwa sababu mzazi anabanwa kwenye michango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu, kwa haya mabilioni ya Mheshimiwa Samia, kwa kweli tunapaswa tumpongeze sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake kwa matrilioni ya fedha. Kwa mazingira haya, wananchi wa Singida Kaskazini wamenionba nije hapa na zawadi kwa Mheshimiwa Rais. Wamesema wanampa Rais zawadi ya dumu 10 za asali; wanampa dumu 10 za mafuta ya alizeti; lakini wanampa na kuku wa kienyeji 50 wa Singida ili wakati anakunywa supu hii ya kuku wa kienyeji, huku anawafikiria kuwaletea zaidi na zaidi ili kuhakikisha wanapata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitaje mambo machache ambayo yamefanyika pamoja na hayo madarasa. Tumepata fedha kwa ajili kukamilisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya ambayo tumepata fedha kwa ajili ya ICU na vifaa vingine muhimu. Mimi hili nimelitazama kwa heshima ya kipekee na ndiyo nasema sasa hapa kuna umuhimu wa kuunga mkono juhudi hizi ili tuendeele kuwatumikia wananchi wetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha kwa ajili ya shule sekondari mpya shilingi milioni 470, Kata ya Kinyeto katika Kijiji cha Mkimbii, hili linaenda kukomboa watoto wetu ambao walikuwa wanakosa elimu kwa kutembea umbali mrefu kufuata huduma ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, kwenye barabara tumepata mamilioni ya fedha. Kwa mara ya kwanza tumepata bajeti mara tatu ya kawaida, tulikuwa tunapata shilingi milioni 600; mwaka huu wa fedha tumepata

## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

shilingi bilioni 2.2. Sasa barabara zinatengenezwa na kazi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto kidogo kwamba, kuna madaraja mawili yanakula watu kila mwaka. Kuna daraja la Mgori na daraja la Pambaa. Madaraja haya naomba yafanyiwe kazi, yajengwe, yanyanyuliwe; wametengeneza zile *drift*, sasa maji yanapopita juu; juzi hapa katikati daraja la Mgori, mama wa watu amekwenda kujifungulia pale darajani, maana alishindwa kuvuka wakati anakwenda hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana jambo hili lifanyiwe kazi, tuhakikishe miundombinu yetu ya barabara inakaa vizuri na haya madaraja yakanyanyuliwe. Hapo hapo kwenye barabara, kuna suala hili la barabara za Miji Midogo pamoja na Makao Makuu ya Halmashauri za Wilaya. Serikali hii imetuletea shilingi bilioni mbili na mamilioni mengine mengi kujenga jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Jimbo la Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli tumepata fedha nyingi sana, lakini barabara zake zile ni mbaya na pia tunahitaji tuboreshe miundombinu zaidi. Hatuwezi kuwa na jengo zuri lakini barabara ni mbaya. Kwa hiyo, naomba sana Mawaziri waje watujengee mbiundombinu ya barabara katika hii Miji Midogo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, naona unanipigia kengele ya kwanza, nami nina mambo mengi mengi kidogo hapa.

Kuna suala hili la Madiwani linalozungumzwa hapa. Posho kwa ajili ya Madiwani; Diwani ndiyo kiungo, ndiyo msimamizi wa mamilioni haya tunayoyazungumza, shilingi trilioni 1.3, Msimamizi Mkuu alikuwa ni Diwani kule chini. Sasa unakuja kumpa posho ya shilingi 300,000; hivi nikikupa wewe

Mwenyekiti hapo, itachukua hata masaa mawili bado ipo mfukoni? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana, bajeti hii iwe ni mkombozi wa Mheshimiwa Diwani. Yeye anasimamia wataalam, wana mamilioni ya fedha wanalipwa. Wataalam kwa kiwango cha chini wana *Degrees* ambapo unakuta mshahara wake ni shilingi 700,000; shilingi milioni moja na kuendelea. Diwani analipwa posho ya shilingi 300,000; anaweza kumsimamia mtaalam huyu? Hebu tuache utani kwenye hili eneo. Mheshimiwa Waziri, usipoangalia katika hili, nitashika shilingi yako, tumkomboe Diwani. Tutunze heshima ya hawa Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba kwa heshima ya kipekee, kwenye eneo la afya, nashukuru sana tumepata Vituo vya Afya viwili vinavyofanya kazi, lakini kuna Kituo cha Afya ambacho tumepata kile cha Makuro. Naomba sasa tupate vifaa tiba. Hospitali ya Wilaya ile nzuri tuliyoipata, Wilaya ya Ilongero, haina vifaa tiba, haijaanza kufanya kazi; ya Msange hakuna vifaa tiba, Mgori hakuna vifaa tiba. Hata hii Makuro tunayoikamilisha sasa, haina vifaa tiba. Naomba sana tupate vifaa tiba ili angalau sasa isiwe ni *white elephants*, zianze kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine hapo hapo, nawasilisha ombi sasa kwa Mheshimiwa Waziri. Kuna boma la Kituo cha Afya cha Ngimu, lina miaka 14 sasa, ni boma karibu limechakaa. Nakuomba sana sana, mwaka huu katika bajeti hii nione ukiniletea fedha kwa ajili ya kukamilisha lile boma la Kituo cha Afya lililokaa miaka na miaka halijapauliwa pamoja na lile la Kohama. Yamekaa miaka nenda rudi, wananchi wamejitolea kwa kuuza kuku wao, lakini sisi tumeshindwa kuwapokea, tatizo ni nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa Mheshimiwa Waziri kwa heshima kubwa sana ulitazame hili kwa heshima ya kipekee na unilettee fedha Mheshimiwa na uje wewe mwenyewe uone ile hali ilivyo, jinsi wananchi wanavyopata



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

taabu kule mabondeni kwenye bonde la ufa, wanatembea umbali mrefu kufuata huduma za afya Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imekwisha! Ahsante sana, naunga mkono hoja. Ila upungufu wa watumishi katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ni mkubwa sana, hasa walimu, sekta ya afya na utawala. Naomba pia mnitazame kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Jonas William Mbunda, wakati huo huo Mheshimiwa Charles Kaijage, Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete wajandae.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuhudhuria katika Bunge hili la Bajeti. Pia, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, jinsi anavyosimamia shughuli za maendeleo ya nchi hii hususani Wizara hii ya TAMISEMI kwa sababu iko katika Ofisi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Waziri Innocent Bashungwa na wasaidizi wake Mheshimiwa Silinde na Mheshimiwa Dugange, Katibu Mkuu Profesa Shemdoe na Manaibu wake wawili; kwa jinsi wanavyochapa kazi kuhakikisha kwamba shughuli za maendeleo katika nchi hii zinaendelea. Vile vile niwapongeze sana kwa kuandaa taarifa ya bajeti ya mwaka 2022/2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla niipongeze Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, jinsi ilivyotoa fedha nyingi kwa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Majimbo yetu na katika nchi yetu kwa ujumla. Naomba nianze kuchangia upande wa *TARURA*. Kwa upande wa *TARURA* kwanza niishukuru Serikali kwa kutoa fedha za nyongeza shilingi bilioni moja kwa miradi ya utengenezaji wa barabara katika Jimbo langu la Mbinga Mjini. Pia nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kupitia Mkurugenzi Mkuu wa *TARURA* kwa kutoa gari aina ya *Landcruiser* mpya hivi karibuni, ambayo imesaidia sana wahandasi kuzunguka katika maeneo ya Jimbo la Mbinga Mjini na kufuatilia maeneo mbalimbali ambayo barabara zina shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia hotuba ya Waziri imeeleza kwamba *TARURA* inasimamia mtandao wa barabara wenye kilomita 144,229. Katika kilomita hizo kilomita 2,473 ni kiwango cha lami, kilomita 30,756 ni kiwango cha changarawe, lakini kilomita 111,199 ni udongo. Mimi binafsi nataka nichangie hasa kwenye barabara zinazotengenezwa kwa kutumia udongo. Katika Jimbo langu kuna Barabara ya Mbinga – Kitanda – Masimeli – Miembeni, lakini kuna Barabara nyingine ya Mbinga – Kikolo – Kiungu na Barabara nyingine ya Mbinga – Magamao – Mpepai – Mto Lumeme. Barabara hizi zote zinatengenezwa kwa kutumia udongo. Maeneo ya Jimbo la Mbinga haya maeneo niliyoyatamka ni maeneo ambayo yapo kwenye miteremko, kiasi kwamba kama barabara inatengenezwa kwa kutumia udongo ina maana kwamba kipindi cha mvua barabara ile yote inaharibika; na wananchi hawawezi kupita katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua kwamba Serikali inapeleka miradi mbalimbali katika maeneo ya Kata hizo ni kwamba hasa kipindi kile cha mvua ujenzi wa miradi mbalimbali pamoja na kutengeneza barabara hizo, inakuwa ni ngumu kwa sababu tayari mvua zinakuwa zimeharibu miundombinu, kwa hiyo inakuwa ni shida. Ushauri wangu hapa naiomba Serikali kwa maeneo hayo ambayo yana hali ya kijiografia tofauti, barabara zake zingekuwa

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zinatengenezwa angalau kwa kutumia changarawe na kwa barabara hizo zinazotengenezwa, Serikali izingatie kujenga mifereji katika maeneo hayo ili kulinda uharibifu wa barabara hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ni kwenye suala la afya. Kwenye upande wa afya naipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa ajili ya kujenga zahanati kwenye vijiji mbalimbali pamoja na vituo vya afya. Lakini changamoto iliyopo katika Jimbo la Mbinga kuna changamoto ya uchakavu wa majengo ya hospitali ya wilaya. Hospitali ya Wilaya ya Jimbo la Mbinga Mjini inahudumia takribani Kata 13 mpaka Kata 14, lakini hospitali hiyo ilijengwa mwaka 1970 mpaka sasa hivi majengo yale yamechakaa na ipo katika hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kabisa Waziri atakapohitimisha aniambie kwamba ni lini atasimamia kuhakikisha kwamba majengo ya hospitali ile yanajengwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jonas William Mbunda. Nilimwita Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, wakati huo Mheshimiwa Grace Tendega ajiandae.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja mimi, Mwijage?

**MWENYEKITI:** Ndio unaongea sasa hivi sasa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri...

**MWENYEKITI:** Anaongea Mheshimiwa Charles Mwijage, anafuata Maimuna Pathan, baada ya hapo ni Mheshimiwa Tendega.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja hapa. Nafikiri hiyo nafasi ilikuwa ni ya kwangu kama sikosei.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage endelea.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Kwanza niipongeze bajeti ya TAMISEMI, kwa taarifa nzuri ya utekelezaji. Utekelezaji unaakisi hali halisi tuliyoiacha huko kwenye Majimbo yetu, lakini napongeza Mpango unatupa matumaini makubwa sana. Nianze na masuala ya Kitaifa kabla ya kwenda Jimboni. Suala la kwanza katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia magari yaendayo kasi Mpango wa Dar es Salaam *DARTS*. Inaelezwa kwamba abiria 180,000 wanasafirishwa kwa siku na tutafikia watu milioni 2,500,000 kwa siku. Ushauri kwa Serikali, wekeza katika magari yanayotumia gesi asilia haraka sana (*natural gas vehicles*) haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, naishauri Serikali tunayo mahitaji ya watendaji lakini tunao watendaji wengi wamehitimu na hawajapata kazi, lakini jambo la kufurahisha kwa taarifa za uhakika Serikali imeanza kuajiri. Hata hivyo, haiwezi kumaliza kuajiri kwa mwaka huu, lakini kuna uhakika mwaka kesho na mwaka kesho kutwa itamaliza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pendekezo langu, vijana wote ambao wako tayari waende katika Taasisi iwe afya iwe shule kusudi wajitolee; na wanapojitolea uwepo utaratibu wa kuwa-*monitor* na kuwa-*mentor*. Kusudi wanapokwenda kuajiri sasa wamchukue yule mtaalam aliyekwenda kuwa *mentored* na wataalam kuliko kwenda kuokoteza. Sio sawa mtu ambaye miaka sita amemaliza shule hajawahi kufundisha unampeleka kwenda kufundisha. Hii itatusaidia sisi kwamba wale vijana kuliko kwenda kuzurura wawe na kazi maalum. Huo ni ushauri wangu kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Jimbo langu na Mkoa wangu. Nashukuru kwa ajili ya Jimbo langu la

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Muleba Kaskazini, yote waliyotekeleza na Mpango wao. Nashukuru kwa niaba ya Wilaya yangu ya Muleba na Mkoa wangu wa Kagera. Nataka niwaeleze katika Wilaya yangu ya Muleba tunazo shule za msingi 250, za sekondari 40, tuna wanafunzi 157,372, kwetu sisi tunao wanafunzi wa sekondari 33,255. Hoja yangu ni kwamba tunahitaji Walimu wa shule za msingi, Walimu tunaowahitaji ni 1,390. Wakati *ratio* ya Taifa ni 1:60 Muleba *ratio* yetu ni 1:71, naomba wanapokuja kugawa Walimu sisi watuangelie kwa macho matatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, sisi Muleba tunao watoto 23,500 ambao wanaingia *form one*, mwaka kesho katika mwaka kilele wa elimu bila usumbufu. Wanaopaswa kuingia darasa la tisa ni watoto 23,500. Kwa uwezekano wa ushindi wa asilimia 85, Muleba watoto 19,000 watakuwa tayari kwenda shuleni. Naomba watuangelie kwa jicho zuri na nimeiona mipango ya Serikali, tunahitaji vyumba 243 ili kuweza kuwapokea watoto hao. Nimeona mpango wa Serikali kwamba tutasaidiana kujenga na sisi Wabunge wa Muleba tumeshajiandaa, mwezi Mei tutaomba ruhusa kwa Spika tunakwenda kuanzisha ule mchezo wetu wa *Bank* ya Matofali. Kwa hiyo, watatukuta huko safarini aje atupe *lift* Mheshimiwa Waziri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie sekta ya afya. Tunavyo vijiji 166, zahanati 142 lakini vijiji ambavyo havina na kata ambazo hazina, wananchi wameshaanza, kwa hiyo kumbe Mheshimiwa Waziri atawakuta njiani. Jambo ambalo sisi hatuwezi tunao upungufu wa wataalam 505, Mheshimiwa Waziri anapogawa wataalam chonde chonde atuangelie kwa macho matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimpe salamu zake Waziri kutoka Bumbile, Mazinga na Ikuza wanamshukuru kwa kutoa boti ambayo itakwenda visiwani; na nimewaambia hiyo boti inayokuja inaitwa *ambulance*, atuletee *ambulance* usafiri mwingine tutajijua. Sisi tuna *square kilometer* 10,200 wanasema kama *kobowagabiyolengela*, wanaomba boti ya pili, 10,200 boti moja haitatosha, lakini tunashukuru kwa hicho kidogo kilipotoka kingine kitaongezeka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye sekta ya elimu. Kumbe sasa hatua tuliyofikia Tanzania kufikia 2025 watoto wote wa msingi wanaweza kwenda sekondari. Jambo lililonifurahisha katika Wizara hii kuna kauli inasema utawala bora TAMISEMI ya wananchi na Mheshimiwa Waziri wanasema *you are walking the talk*, kauli yako uliyoitoa juzi, ikamfanya Mbunge wa Nyamagana aende kula chakula na Mkuu wa Mkoa na yule muuza ndizi, *you are walking the talk*. Hata hivyo, sasa ndugu yangu akipiga watoto awapige watoto wote, yeye vijiji vyake vyote vimeandikwa chini ya TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kijiji changu kimoja cha Rutoro, kuna watoto asilimia 23 ndio wanafika shule asilimia zaidi ya 77 hawaendi shule, kuna shule nyingine *just* 53 ndio wanakwenda shule katika watoto 540, kitu gani. Ni kwamba kuna tatizo la utawala bora. Vijiji vilivyoandikishwa vya Kata ya Rutoro wamekuja watu wanafukuza watu kwenye vijiji vilivyoandikishwa. Kama ni utawala bora, a-*walk the talk*, aende akawaulize vijiji alivyovisajili chini ya TAMISEMI katika maeneo ya Kata nane, ni nani mwenye mamlaka ya kuja kupangua vijiji vile bila yeye kuhusishwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa Wakuu wa Mikoa wote wawe kama Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, mnakaa watu mnajadiliana. Yule kijana aliyekuwa anasukuma ndizi amenipigia simu, anasema ameridhia makosa yaliyotokea amewasamehe wote. Sasa na wengine waambie kama wanasikia Mbunge anahoji, wamuite Mbunge wakae naye wajadiliane, hatuwezi kuishi kwa kebehi. Mtu anakwenda anakatakata mashamba ya watu anasema Muhaya ukimpa heka sita zinatoshia, hiyo dharau isiletwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka 100 ya Nyerere, huwezi kusimama kuwabagua watu kikabila, unasema heka sita kwa Muhaya ni nyingi, nani alikuambia Muhaya hawezi kuwa na heka sita. Mimi nina zaidi ya heka 30, sio Muhaya? Hata hivyo, kwa nini tunatafuta ukabila? Hatuwezi kukubali kudharauliana, Mheshimiwa Waziri a-*walk the talk*, ahakikishe

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wale wote wanaohusika wakutane wote, Wizara zote zinazohusika, wakamalize matatizo yale, TAMISEMI ya wananchi, lakini sio wale wananchi ambao wanakuwa 75 kwenye *ranking* za FIFA. (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Charles Mwijage. Sasa namwita Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan, wakati huo Mheshimiwa Charles Iguta Kajege, anajiandaa na wachangiaji wengine wawili wakiwa wanajiandaa, Mheshimiwa Tendega na Mheshimiwa Mwaifunga.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuweza kuchangia siku hii ya leo. Pia, namshukuru sana Rais wetu kipenzi mama Samia Hassan Suluhu kwa kazi yake nzuri aliyofanya. Amemwaga fedha nyingi sana kwenye sehemu zetu za kazi kwa ajili ya afya na elimu. Tunamshukuru sana Rais wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali zetu za Mkoa wa Lindi zimechakaa sana na zinakatisha tamaa. Kuna hospitali za wilaya ukifika pale huwezi ukaamini kama ni hospitali ya wilaya, hospitali zile ni kongwe na zimechakaa sana. Hospitali hizo zina matatizo mengi, kwanza hazina vifaa tiba, zina matatizo ya watumishi, wataalam mbalimbali hakuna. Kuna tatizo lingine la kukosekana kwa umeme, unazimika mara kwa mara. Tunaomba wapatiwe hata *solar* kwenye zile sehemu muhimu katika Hospitali hizo. Zaidi kwa mfano kuna Hospitali ya Nachingwea tunahitaji kupatiwa *solar* kwenye jengo la mama na mtoto, pia kuna tatizo la taa ile kubwa ya *theatre* hakuna kabisa kwenye hospitali ile. Ni Hospitali ya Wilaya lakini haina hicho kitu, taa ile kubwa ya *theatre* hakuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la *ambulance*, Wilaya nzima kuna *ambulance* moja ambayo iko kwenye

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kituo cha Afya Kilimalondo, ni mbali sana kutoka pale Wilayani Nachingwea. Tunaomba sana sana tupate *ambulance* kwa sababu, kuna *Ambulance* ambayo ni mbovu zaidi ya miezi sita na haitengenezeki. Tunaomba sana watu angalie kwa jicho la pili tupate *ambulance* kwenye hospitali hiyo. Hakuna ukumbi wa mikutano, asubuhi kunakuwa na ile *morning report*, hakuna ukumbi wa kufanyia kile kitu, wanasimama tu wanapeana ripoti. Tunaomba watusaidie tupate ule ukumbi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wodi ya wanaume imechakaa sana, inakatisha tamaa. Hakuna kichomea taka kulingana na uwezo wa hospitali ile. *Incinerator* iliyopo ni ndogo sana tunaomba watusaidie tupate hiyo *incinerator*. Uzio wa Hospitali ya Nachingwea ule unakatisha tamaa, ni mbovu mbovu, mbovu mno. Tunaomba watusaidie tupate matengenezo ya hospitali hiyo. Pia, hakuna *dental chair* kwenye hospitali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kuna Hospitali ya Liwale, katika hospitali hiyo tunashukuru wametuletea *X-Ray*, lakini *X-Ray* hiyo kuna mtaalam mmoja tu, akiumwa au akiwa na dharura yoyote au akienda likizo, hakuna huduma inayoendelea pale. Tunaomba tuongezewe wataalam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, kuna hizi barabara. Barabara zinakatisha tamaa sana, kuna barabara ya kutoka Lupota kwenda Chingunduli, huwezi kupita imekufa ile barabara, inakatisha tamaa. Tunaomba watusaidie tutengenezewe hizi barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi niliuliza swali kuhusu barabara ya Nanganga – Nachingwea – Masasi – Liwale, lakini bahati mbaya nimejibiwa jibu la Mkoa wa Mtwara barabara tofauti kabisa. Naomba sana tupate jibu la msingi baadaye kabla hawaja-*wind up* Wizara husika, hizo barabara tupate majibu ya msingi ili tujijue na sisi tuko katika sehemu gani. Wananchi wa kule tangu tumezaliwa na wengine



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mpaka wamekufa, hatuijui lami jamani, hatuijui lami, inasikitisha na barabara hizo ni za mkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana watu angalie kwa jicho lingine, kwa jicho la huruma, barabara zinakatisha tamaa. Akinamama wajawazito wanajifungua njiani kwa kukosa barabara. Barabara na madaraja hakuna, tunaomba sana watusaidie, tunaomba sana TAMISEMI waangalie hilo suala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la watumishi naomba niongee kidogo nieleweke. Watumishi wengi wanaojiriwa wanaopelekwa Mkoa wa Lindi, wanakwenda kuchukua *check number*, then wanaomba uhamisho wanageuza. Matokeo yake kule kwetu kunakaa hakuna watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa hivi, kuna vijana wengi wanajitolea, kuna wanaojitolea nafasi za ualimu na nafasi zingine. Tunaomba sana wapewe kipaumbele wazawa wa kule kwa sababu wamezoea mazingira ya kule. Wakiajiriwa watu wa kule watakaa. Inasikitisha sana wanapojiriwa watu wengi tunasema tuna watumishi, lakini baada ya muda mfupi watumishi wote wanakuwa wameshaondoka. Sijui ni kwa nini, sijui kunaonekana vipi kule kwetu. Tunaomba sana hili suala lipewe kipaumbele. Watumishi wakiajiriwa waanze kuajiriwa wazawa wa kule. Kwanza wana uchungu na kwao; pili wamezoea mazingira magumu watakaa. Naomba sana, haya masuala yaangaliwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nalirudia ni barabara, jamani barabara, barabara jamani, barabara za kwetu zinasikitisha. Tunaomba jamani watufikirie kwa barabara za kwetu na sisi wenzao ni binadamu pia, tunaomba. Barabara za kwetu ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nasisitiza kuhusu suala la barabara. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Muda umekwisha na Taarifa lazima utoe ndani ya muda wake. *(Kicheko)*

Sasa namwita Mheshimiwa Charles Muguta Kajege, wakati huo Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga wanajiandaa.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Vilevile nichukue fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mwibara sasa hivi limeanza kung'ara, namshukuru sana. Pia, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri wa TAMISEMI na wasaidizi wake pamoja na Katibu Mkuu wa TAMISEMI kwa kazi kubwa na jukumu kubwa sana walilionalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia katika maeneo yafuatayo: Kwanza ni katika sekta ya afya. Huduma za afya katika Jimbo langu la Mwibara bado haziridhishi. Tunavyo tu vituo vitatu vya afya vya Kasahunga, Kisorya na Kasuguti, lakini bado huduma zinazotolewa siyo za kiwango cha vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza ni kwamba, hivi vituo vimejengwa kwa muda mrefu sana. Kwa mfano, Kituo cha Kasahunga kina zaidi ya miaka 20, lakini bado hakijakamilika. Kituo cha Kasuguti kina zaidi ya miaka 15 bado hakijakamilika na Kituo cha Kisorya kina zaidi ya miaka saba bado hakijakamilika. Naiomba Serikali yangu sasa hivi iweze kutufikiria vizuri sana na kutupa kipaumbele iweze kukamilisha vituo hivyo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuhusia na Mfuko wa Jimbo. Naipongeza sana Serikali kwa kuongeza fedha katika mfuko huu, lakini nataka niishauri Serikali, pesa hizi naomba zigawanywe sawa sawa katika kila Jimbo.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Hakuna *formula* ambayo tutatumia hapa ambayo itafanya Jimbo lingine liweze kupata inavyostahili. Hakuna *formula* nakwambia! Fedha hizi zigawanywe kama ambavyo zimegawiwa pesa za *TARURA*, kila Jimbo lipate pesa sawa sawa. Tukishagaiwa hivyo sasa, kila Mbunge atakwenda kupambana na mambo yake huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo letu la Mwibara lina ardhi ya kutosha na lina maji ya kutosha, tunachohitaji ni elimu sahihi na mafunzo sahihi ili tuweze kutumia fursa zilizopo katika sekta hizo za uvuvi na kilimo. Jimbo letu tumeshaenda hatua moja mbele katika kutafuta Chuo cha *VETA*. Kata yetu ya Butimba imetoa ekari 57 kwa ajili ya ujenzi wa *VETA* hiyo. Naomba Serikali sasa itufikirie katika mgawo wa *VETA* katika kipindi hiki ambacho kinakuja nasi tuweze kupata Chuo cha *VETA* katika Jimbo letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna shule kama tatu kongwe za msingi ambazo majengo yake yameshachakaa na baadhi ya viongozi wa elimu wamekuja na wamesema kwamba, hayo majengo sasa hivi hayastahili kutumiwa tena. Naomba Serikali yetu sasa iweze kufikiria namna ya kujenga shule hizi kongwe za zamani ili ziweze kuwa salama na ziweze kuendelea kutumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la posho za Madiwani limezungumzwa na wenzangu wengi waliotangulia. Wakati wa kampeni tunasema tunakwenda na mafiga matatu, yaani Rais, Mbunge na Diwani, lakini baada ya uchaguzi sisi wengine tunawafungia nje hawa Madiwani, tunakuwa tena hatuwatendei haki. Pamoja na mapendekezo ambayo yametolewa kwamba posho zao ziongezwe angalau ziwe shilingi 800,000/= kwa mwezi, mimi naona kama bado hazitoshi. Nashauri angalau wapate shilingi milioni moja kila mwezi ili waweze kufanya kazi nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao Madiwani ndio *first responders* wetu. Ndio wanaotatua matatizo ya wananchi sisi tukiwa huku Bungeni. Vilevile tuisahau kwamba na wao

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanatumika kama *ATM* huko majimboni mwetu. Kwa hiyo, naomba nasi tuweze kuwafikiria waweze kupata posho ya kutosha waweze kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya miaka 13 sasa hivi tangu mradi wa ujenzi wa barabara ya Bulamba hadi Kisorya ufanyike. Kuna wananchi ambao walitoa nyumba zao zikabomolewa kwa ajili ya kupisha mradi huu, lakini bado mpaka sasa hivi hawajalipwa.

Naomba Serikali yetu sasa iharakishe malipo ya hawa wazee ambao wengi wao sasa hivi maisha yao yamekuwa magumu; wengine walipoteza nyumba zao na kwa hiyo, wameshindwa kujenga nyumba zao upya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, Taarifa.

### T A A R I F A

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana na kaka yangu kwa mchango wake mzuri. Ni kweli, hiyo barabara ni ya muda mrefu na ni kweli kwamba sio wananchi tu wa upande wa Jimbo la Mwibara, hata wa Bunda Mjini mpaka kwenda kule Nyamuswa na wenyewe mpaka sasa hivi hawajapisha na wametenga maeneo yao kwa sababu Wilaya ya Bunda wanahitaji barabara ya lami ambayo itaenda kuunganika na Arusha. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kajege, unapokea Taarifa?

**MHE. CHARLES M. KAJEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naichukua kabisa na kuikubali hiyo Taarifa. Nami nasisitiza tena kwamba, haya malipo yafanyike mapema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo. Naunga mkono hoja hii ya TAMISEMI. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Grace Tendega na wakati huo Mheshimiwa Hawa Mwaifunga anajiandaa.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata fursa hii. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu; vile vile niwashukuru Mheshimiwa Waziri na Manaibu Waziri pamoja na watendaji wa TAMISEMI kwa usikivu wenu. Usikivu huo muuendeleze kwa kuu-*transform* kwa watendaji ili waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia Wizara hii nikijielekeza katika fedha za maendeleo ambazo zinatolewa. Wizara hii inagusa moja kwa moja wananchi kule ngazi za chini. Wizara hii ni nguzo kabisa, ni kama uti wa mgongo wa Wizara zote katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi kwa sababu, fedha za maendeleo zimekuwa zikipelekwa tofauti kwa Halmashauri tofauti. Kuna Halmashauri zinapata fedha zaidi ya asilimia 100 waliyoomba, kuna Halmashauri ambazo zinapelekwa fedha za maendeleo chini ya asilimia 50 ya zile fedha ambazo wameziomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha atueleze nini kinasababisha hivyo? Kwa sababu, tumeona kuna Halmashauri ambazo zina uhitaji mkubwa na hazipati fedha kwa wakati. Kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Momba imekuwa inapata fedha ndogo sana ukilinganisha na Halmashauri nyingine ambazo zipo. Kwa hiyo, tunapenda kuwe angalao na msawazo, Halmashauri zipate fedha ambazo zitawakwamua katika miradi yao ya maendeleo, ili waweze kufanya maendeleo ya Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kukosa usimamizi wenye weledi na uratibu mzuri katika Wizara hii. Ninazungumza hivi kwa sababu, kumekuwa na miradi ya maendeleo ambayo imeratibiwa toka miaka mingi na mpaka sasa haijakamilika. Miradi ambayo inakamilika lakini

haitumiki na miradi ambayo inakamilika lakini katika ubora wa chini sana. Sasa hivi vyote vinaleta changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bora mkawa na miradi michache mizuri, ikamilike kwa wakati ndipo tutaona thamani ya fedha ambazo tunazipeleka katika Halmashauri zetu. Kupeleka miradi mingi ambayo haimalizi kwanza inaongeza fedha nyingi kwa sababu wakandarasi waki-*stop* kuna pesa wanakuja wanadai, na hii fedha wananchi wanaigharamia pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nitoe mfano. Kamati yetu ya LAAC, tulikwenda Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali; ninavyosema usimamizi, ni kwa sababu gani? Halmashauri ya Mbarali, ina mradi wa muda mrefu, lakini tumekwenda pale, kwa sababu tulitoa taarifa, ndiyo kwanza walianza kuchonga barabara, walikwenda kuchoma moto, kwa sababu kuliota nyasi nyingi sana. Wamechoma moto hadi *gutters* ziliungua; ujue hizo nyasi zilikuwa na urefu gani? Maana yake ni kwamba, usimamizi haupo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini usimamizi haupo? Wenzangu wamezungumza hapa, kuna Wenyeviti wa Vijiji, Watendaji, na Madiwani. Hawa wote ni wasimamizi katika zile ngazi. Kama hatuwawezeshi, hawawezi kuangalia hii miradi vizuri kwa ufasaha.

Kwa hiyo, tuangalie namna ambavyo hawa watawezesha kwa namna moja au nyingine, na kuwe na mfuko wa ufuatiliaji. Huu mfuko wa ufuatiliaji utasaidia wale ambao wako katika kufuatilia waweze kwenda na kuona fedha zinazowekwa pale. Mradi wa takribani shilingi bilioni nne na zaidi haukaguliwi, hakuna anayeufuatilia! (*Makofi*)

**MHE. ABUBAKARI D. ASENKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Asenga Abubakari.

## T A A R I F A

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba kumpa taarifa mzungumzaji, ukweli katika Mradi wa Hospitali ya Mbarali anaouzungumzia ni mradi *very serious* ambao umeharibiwa na wasimamizi wa mradi ule. Namkumbusha tu kwamba, tulikuta hata bohari ya dawa imewekwa dawa ikiwa kuna joto kali sana. Hakuna vipooza joto. Kwa hiyo, anachosema ni sahihi, namwongezea taarifa hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega, unapokea taarifa?

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa kwa sababu, bohari ya dawa iliwekwa sehemu za joto na wanaharibu dawa nyingi sana ambazo ni fedha za wananchi na ni dawa ambazo zingeweza kutumika. Kwa hiyo, hivi ndivyo vitu tunavyovizungumza kwamba usimamizi hakuna. Kwa hili niko *serious* kwa sababu, kama hamtasimamia hizi fedha takribani shilingi trilion nane zinakwenda kule chini, tutakuta madudu makubwa yako kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumzia pia manunuzi yasiyozingatia sheria. Haya manunuzi hayazingatii sheria, lakini vilevile sheria yetu ina changamoto; unakuta bati linalouzwa shilingi 30,000/= wananunua kwa shilingi 110,000/= . Kwa hiyo, hizi ndiyo changamoto. Namwomba Mheshimiwa Waziri waangalie, kama hizi sheria zina shida walete turekebishe humu ndani ili tunusuru Watanzania pesa zile zitumike vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya CAG inasema, Halmashauri 40 zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.37 bila ushindani. Halmashauri 59 zilifanya matumizi ya shilingi bilioni 8.86 bila idhini ya Bodi ya Zabuni na Halmashauri tatu zilitekeleza miradi isiyokidhi viwango na kusababisha hasara ya shilingi milioni 32.64. Hii maana yake ni kwamba, kama...

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Hitimisha hoja yako, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha. Nawaomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI, muwe mnazingatia usimamizi kwa mali za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, wakati huo huo wajiandae Mheshimiwa Daniel Awak, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta na Mheshimiwa Flatey Gregory Massay.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara hii ya TAMISEMI na Serikali za Mitaa. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kanijalila afya na nimeweza kusimama hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, naomba nijielekeze moja kwa moja kwenye Halmashauri yangu. Mimi ni Diwani kwenye Halmashauri ya Tabora Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuzungumzia kuhusiana na suala la wamachinga. Hili ninalizungumza kwa sababu natamani sana kuwekwe utaratibu mzuri kuhusiana na suala zima la Wamachinga. Kwa sababu pale Tabora Mjini kilichotokea kwa kweli siyo kitendo cha kiungwana. Wamachinga wale wamevunjiwa vibanda vyao tena usiku wa manane, wao wenyewe wakiwa wamelala hawana Habari, asubuhi wanakuja wanakuta vibanda vyao vimevunjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kabisa Mheshimiwa Waziri atakuwa na taarifa hii, lakini naomba



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nitoe ombi kwa Mheshimiwa Waziri, kama bajeti yake itakuwa imepita hapa, namwomba sana aende Tabora. Nenda Tabora ukapate uhalisia wa jambo hili, ukapate ukweli wa jambo hili, usisikilize tu peke yake watendaji wako, nenda kawasikilize na wananchi shida iko wapi? Ni kweli wametengewa eneo, lakini eneo lile ni dogo. Je, watendaji hawa wamefanya tathmini ya kujua Wamachinga ni wangapi katika Manispaa ya Tabora? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mahali walipojenga wametenga eneo la watu 500 peke yake. Tabora Mjini haina Wamachinga 500 peke yake, wapo zaidi. Pia nenda kawape watendaji wako elimu, Wamachinga ni watu gani? Kwa sababu wao wanachochukulia, Wamachinga ni wale wanaouza bidhaa tu peke yake za kawaida, lakini hawa akinamama ntilie, wamama wa mbogamboga, wamama wa matunda, wamama wanaopika chapati, mandazi, wanasema wale sio Wamachinga, sasa wale ukiwakuta barabarani unawafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, watoe mwongozo kwenye Halmashauri zetu, kama ambavyo leo tuko hapa, eneo la Wamachinga linajengwa tena kwa ustadi mkubwa na kila kitu...

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Mdee, taarifa.

### T A A R I F A

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba changamoto za Tabora Manispaa ziko pia Jimbo la Kawe maeneo ya Tegeta, Magwepande na Bunju. Kwa hiyo, nakupa taarifa ili Waziri adake akijua akitoka Tabora Manispaa aende na Jimbo la Kawe kuna shida kubwa. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwaifunga unapokea taarifa?

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba dhana ya Wamachinga inaonekana viongozi wetu huko chini hawaiielewi. Ndiyo maana unakuta kumekuwa na changamoto kubwa sana kiasi kwamba, kunakuwa hakuna maelewano baina ya wananchi pamoja na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ukichukuliwa utaratibu kama uliofanyika maeneo ya Morogoro; leo hapa Dodoma Wamachinga tunapita tunakutana nao mitaani, wanasubiri eneo lao *special*. Wale wakishagawiwa ukimkuta barabarani yule kweli unaweza ukapambana naye; lakini unaenda kupambana na mtu ambaye hata eneo la kufanyia biashara hujampa, unategemea huyu mtu anakwenda wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba sana na namwomba sana Mheshimiwa Waziri, nenda mwenyewe kashuhudie hali halisi, vinginevyo hali ya Tabora Manispaa itakuwa haieleweki. Hali ni tete, wananchi mitaji yao imekufa kwa sababu wamevunjiwa wakati wakiwa wamelala na hawana walichokiokoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la afya. Kuna Sera ya Zahanati Kijiji kwa Kijiji. Hii sera inaonekana kwamba haitekelezwi ipasavyo. Katika Jimbo la Tabora Mjini lina kata za mjini na kata za vijijini. Katika Kata za vijijini unakuta kuna zahanati moja peke yake katika Kijiji ambacho kina vitongoji vitano ama sita.

Kwa hiyo, mtu kutoka Kitongoji kimoja kwenda Kitongoji kingine anatembea zaidi ya urefu wa kilometa tano mpaka kumi kufuata hiyo zahanati. Kwa hiyo, naomba sana, hii sera ya zahanati vijiji vyote, naomba iweze kutekelezwa. Pia mliiweka hata kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, tunawaomba sana mtusaidie ili wananchi wetu wa vijijini nao waweze kunufaika na sera hii.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Kata moja ya Isevya; ile Kata ina watu wengi sana. Kutokana na watu wengi sana, pale kuna zahanati. Tulikuwa tunaomba sisi wakazi wa Tabora, kikiwekwa kituo cha afya pale kitaweza kusaidia wananchi wa kata za karibu kuweza kufika pale, kwa sababu pale wanazalisha mpaka watu watano mpaka tisa kwa siku. Nafahamu Mheshimiwa Waziri taarifa hii anayo, naomba utusaidie, tupelekeeni fedha mtuwekee kituo cha afya na pale ili na kile kingine kilichopo maili tano kiweze kusaidia wananchi wa eneo la kata za mjini, ili waweze kupata huduma sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na masuala ya elimu. Kwenye suala la elimu kumepolekwa fedha nyingi sana katika ujenzi wa shule hasa za sekondari, lakini shule za msingi zimesahaulika kabisa. Pale Tabora Mjini kuna shule kongwe, kama Shule ya Isike, Shule ya Msingi Gongon na Shule ya Msingi Kitete. Shule hizi ni kongwe na zimekuwa ni za zamani sana. Leo imefika mahali mabati yanavuja, mvua zikinyesha yale madarasa wanafunzi hawaingii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chonde chonde, Waziri mwenye dhamana tunaomba mtusaidie, hizi shule za zamani mtusaidie kuzifanyia ukarabati. Nazungumzia shule za msingi, lakini pia msaidie kuongeza madarasa kwenye hizi shule ili wananchi wengi ambao wanaishi maeneo ya mjini watoto wao waweze kupata elimu karibu na maeneo ambayo wanakaa kuliko ilivyo hivi sasa mtoto anatoka umbali mrefu kufuata shule wakati kuna shule ambazo unaweza ukajenga madarasa na zinaweza zikasaidia watoto wetu kusoma karibu na maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante nilikwita Mheshimiwa Daniel Awack Tlamai, wakati huo Mheshimiwa Massay na Mheshimiwa Simwanza Sitta wanajiandaa.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu na pili nimshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais kwa kuendelea kufanya shughuli ya nchi yetu kwa ufasaha zaidi. Katika Jimbo la Karatu tumepata mafanikio makubwa wakati huu kwa mwaka wa fedha tulipokea bilioni 1.2 ambayo ilikuwa inaitwa hela ya Mama Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tuliweza kupata milioni 700 kwa kukarabati sekondari kongwe ya Karatu, lakini vile vile tulipata milioni 470 kwa ajili ya shule ya kata ya sekondari ambayo inajengwa katika Kata ya Ganako. Pia tuliweza kupata milioni 500 kwa kujenga Kituo cha Afya cha Mbuga Nyekundu. Hata hivyo, niseme kwamba asubuhi Mheshimiwa Getere aliongea kwamba kule TAMISEMI kuna vifungu kwenye hizi milioni 500 tulizopokea ya Kituo cha Afya cha Mbuga Nyekundu, mpaka sasa hivi tulipokea awamu ya kwanza milioni 250, lakini awamu ya pili tumepokea milioni 250. Mpaka sasa tunapongea, tuna zaidi ya mwezi mmoja shilingi 250 wanaendelea kusema vifungu vya kuhamisha hizo hela mpaka sasa hivi bado, sasa inashangaza kidogo, kama hela inatolewa kutoka Wizarani, halafu inaweza kuchukua siku 30 halafu huduma hiyo isiendeleo, kwa kweli hii ni changamoto, mpaka leo hii tuna zaidi ya siku 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana niliweza kuongea katika Bunge hili kwamba, tulikuwa tuna tatizo la fidia katika eneo la uwanja wa Lake Manyara, lakini nimpongeze Mheshimiwa Rais wananchi wale wamelipwa zaidi ya bilioni 5.9, katika eneo hili la fidia eneo la Lake Manyara. Sisi pia tulifanikiwa kupata hela kwenye hospitali ya wilaya lakini iko hatua zaidi ya 85% na naamini kwamba inaweza kukamilika wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea eneo la *TARURA* kidogo, hili eneo la *TARURA* Kwa mwaka jana tulitenga fedha, lakini kwenye hili eneo kuna changamoto kubwa. Mwaka 2010 Karatu tuliahidiwa tupate kilomita mbili za lami, lakini Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano mwaka

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2015 alituhidi kilometa nane pamoja na ile ya Mheshimiwa Jakaya 2010 ikawa jumla ni kilomita 10. Mpaka sasa hivi tunapoongea kilomita zilizojengwa katika Jimbo la Karatu ni 0.6 mita, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri shahidi, toka mwaka 2019 mpaka leo hii, kuna kilometa 0.9, mpaka leo haijakamilika, ukiuliza changamoto ni nini? Barabara ilifumuliwa kutoka mwaka 2019, mpaka leo tunapoongelea mwaka 2022. Sasa nina wasiwasi sana kwenye ahadi hizi za viongozi wetu kwamba tutaendelea kupata changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa Awamu ya Tano mwaka 2020 wakati akininadi mimi kama mgombea wa jimbo lile, aliweza kusema kwamba tunaweza kwenda kujenga sasa kilometa 10; kama mita 0.9 imeweza kuchukua muda wa miaka mitatu, sasa TAMISEMI ijipange, hizi ahadi za viongozi kwa mwaka wa fedha unaokuja wajipange ni namna gani wanaweza kutimiza ahadi za viongozi wetu wakuu wanaohidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipenda kuongelea eneo hilo hilo la *TARURA* kwamba ufanisi wa *TARURA* ni changamoto kwa sababu wao bajeti inaisha mwezi wa Sita tarehe 30, *TARURA* wanakwenda kwenye kujenga barabara mwezi Januari au Februari. Sasa nashangaa kidogo kwa nini bajeti ikiisha *TARURA* isijipange kama wenzetu wa *TANROADS* wanavyojipanga. Nafikiri kuna changamoto *TARURA* kwa kujipanga, hofu yangu ni kwamba wataalam walioko *TARURA* bado ni wababaishaji. Nafikiri waangaliwe upya *ma-engineer* hawa tunaopewa huku *TARURA*. Nitatoa mfano, Mkoa wa Arusha tulipewa bilioni 19, lakini ufanisi wa bilioni 19 unakuwa na changamoto katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hili kuna muda tulipewa milioni 500. Milioni hiyo 500 tuliambiwa kwamba inaweza kujenga kilometa moja ya lami kwa Jimbo la Karatu ilitangazwa mara nne, mtu wa chini sana aliomba kilometa ile kwa shilingi milioni 750. Sasa nashangaa kidogo kwa nini TAMISEMI wasifanye tathmini ya kutosha kuona kwamba kilometa moja ya lami inajengwa kwa kiwango gani. Nafikiri hii inakuwa ni changamoto mpaka sasa hivi mkandarasi

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

imeshindikana kupatikana kwa kilometa moja hii ya lami ambayo wameweza kutupatia shilingi milioni 500 kwa ajili ya kujengwa kiwango cha lami kilometa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto katika watumishi; kwa Jimbo la Karatu jumla ya eneo la shule ya msingi tunahitaji watumishi 1,500 lakini walioko ni 964. Ukienda shule ya sekondari tuna upungufu wa zaidi ya 129, ukienda afya tuna upungufu wa watumishi 188. Lakini ukiangalia Wizara watakwambia sasa wameajiri, lakini Serikali iliacha kuajiri muda mrefu, kwa idadi iliyotangazwa ya waajiriwa ambao sasa wataajiriwa, hata wale tu waliostaafu kwa miaka yote Serikali haijaaajiri, nafikiri idadi hiyo haitoshi. Kwa maana hiyo ina maana wenzetu wa Utawala Bora wajipange katika eneo la ajira kwamba hao wanaoajiriwa hawatatosha. Tunaomba waangalie eneo hili la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu ni mkubwa katika maeneo yetu...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Daniel Awack Tlamai kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, wakati huo Mheshimiwa Flatei Gregory Massay pamoja na Mheshimiwa Joseph Kamonga wakijiandaa.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii. Pia nawashukuru wananchi wa Urambo kwa ushirikiano wanaonipa pamoja na familia yangu.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Waziri Mheshimiwa Bashungwa na Naibu Mawaziri Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Dugange na Profesa Shemdoe kwa kazi kubwa wanazofanya, Manaibu wake, Ndugu Mweli, Dkt Grace, Ntuli naweza kuwataja wote, nawajua kichwani nawajua kwa sababu wanafanya kazi kubwa sana wakina Dkt Ntuli mambo ya afya hayo, akina *Engineer* Seif, Komba wa *TARURA* wanafanya kazi, jamani tuwapigie makofi *TARURA* wanafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana, wanafanya kazi kubwa, hii Wizara ni kubwa, Mheshimiwa Waziri anajua Wizara yake ni kubwa sana, lakini nawapongeza sana. Pia nichukue nafasi hii kumshukuru sana Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza Serikali ya Awamu ya Sita, ametoa misaada mingi sana siwezi kusahau, jinsi ambavyo ametusaidia Urambo, ametupa vituo vya afya vingi, ametupa madarasa mengi. Tunamwombea kwa Mwenyezi Mungu, ampe afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi tu kwa niaba ya wananchi wa Urambo ni kwamba kutokana na madarasa mengi tuliopata tuna upungufu wa Walimu zaidi ya 600 ambapo tutashukuru sana Serikali ikitupa ili kazi nzuri iendelee. Pia kwa upande wa afya tumepata vituo vya afya, zahanati, tunahitaji wafanyakazi zaidi ya 269, kwa hiyo tutashukuru sana kama Serikali ikituwezesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo nawaunga mkono wenzangu ambao tayari wameshaongea, kwa mfano, kuwaongeza posho Watendaji wa Kata, Wenyeviti wa Vijiji na Madiwani. Hawa wanafanya kazi kubwa sana, naomba kweli suala lao lizingatiwe ili waweze kumudu kazi zao vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo naunga mkono wenzangu wote, kulikuwa na Mheshimiwa Mbunge alizungumzia juu ya chakula cha mchana, naomba sana suala la chakula cha mchana litolewe mwongozo kwa

sababu watoto wengine wanatoka mbali, ni vizuri kukawa na chakula cha mchana. Wakati huo huo tumekuwa tukiomba sana suala la taulo za kike kwa ajili ya watoto wa kike. Kwa hiyo tunaomba suala la taulo za kike ziweze kupatikana kutokana na fedha za halmashauri. Suala ni mipango tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimesikia wengi wakizungumzia kuhusu wafanyakazi wanaopelekwa vijijini. Mtu anapelekwa kijijini kwa *style* ya kizamani, wanawekwa kwenye malori halafu wanashushwa wanaambiwa wewe shuka hapa, mtu hapajui na wengine hata shule yenyewe haijui au kituo cha afya hakijui. Kwa hiyo napendekeza hivi, Ofisi hii ya Rais TAMISEMI watoe mwongozo wa jinsi ya kupokea wafanyakazi, kuwe na mpango maalum wa kupokea wafanyakazi, siyo lazima hela tu, lakini wanaweza kuweka utaratibu wa kuandaa nyumba ambayo wanajua akifika, atakaa, atalipa mwenyewe lakini kuwe na maandalizi ambayo yatamfanya mfanyakazi asijisikie kufanya kazi, kuliko wanavyofanya *style* ambayo mtu anashushwa tu porini anaambiwa nenda kule utaiona shule au utaona kituo cha afya. Kwa hiyo nafikiri kuwe na maelekezo ya jinsi ya kupokea wafanyakazi wanapokwenda kwenye vituo vyao vipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikienda kwa upande wa Walimu; Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya uhaba wa Walimu, wamesema wengi sana na mimi mwenyewe nimesema tunahitaji Walimu zaidi ya 600; Walimu 547 kwa upande wa msingi na Walimu 152 kwa upande wa sekondari. Kwa hiyo zaidi ya Walimu 600, lakini sasa nafikiria jinsi Walimu wanavyozidi kuwa wengi kulikuwa pia na haja ya kurudi kuiangalia Tume iliyoundwa ya Walimu kwa ajili ya kuwashughulikia Walimu ambayo inaitwa *TSC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati ya USEMI tuliomba tathmini ifanyike kuhusu Tume inayohudumia Walimu kutokana na wingi wao na maeneo wanayofanyia kazi, lakini naishukuru sana ofisi ya Mheshimiwa Bashungwa kwa sababu wamesema ukweli kwamba kazi ya kuichunguza *TSC* kuona kama inafanya kazi yake iliyokusudiwa haikufanyika ipasavyo.



## *NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Kwa ruhusa yako naomba nisome kitabu; kazi za Tume ya Walimu (*TSC*) wameeleza vizuri kabisa kwenye Dhima, kuhakikisha Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari wanapata huduma bora kuhusu masuala ya ajira, kupandishwa vyeo na kukuza maadili. Halafu wakaanza kuzichambua zile kazi, siwezi kusoma zote kwa sababu ya muda, nimechagua tatu tu wanasema kuajiri, kupandisha vyeo na kuchukua hatua za nidhamu kwa walimu; Kuhakikisha uwiano sawa katika usambazaji wa Walimu ndani ya Serikali za Mitaa na shule. Hivi ndiyo kazi wanazofanya hawa? Halafu (g) Kusimamia *program* za mafunzo ya Walimu kazini, hizi ndiyo kazi baadhi ya kazi ambazo zimetajwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nampongeza sana Waziri kwa sababu ile Tume iliyofanya hii kazi wamekuwa wakweli sana, wamefanya tathmini ya *TSC* na wenyewe wameeleza vizuri kabisa wanasema hivi, wao wenyewe, kwamba, Sekretarieti ya Tume imejitathmini yenyewe na ni vyema utafiti mwingine ukafanywa kwa kutumia watathmini wa nje ili kuangalia kwa jicho la mtu mwingine bila kuwepo na upendeleo namna Tume ilivyofikia kusudi la kuanzishwa kwake. Wao wenyewe kabisa wameomba Tume nyingine iundwe. Kwa hiyo napendekeza Tume nyingine iundwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, wao wenyewe wamekubali kwenye kitabu chao, muda wa kufanya utafiti huu ulikuwa mfupi sana na pia kulikuwa na uhaba wa fedha za kufanyia utafiti. Ili uweze kukamilika kwa wakati, ni matumaini yetu kwamba katika tafiti nyingine muda pamoja na uwezeshwaji utolewe wa kutosha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Magreth Simwanza Sitta,.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sekunde moja nimalizie.

**MWENYEKITI:** Basi nakuongeza dakika moja, lakini muda wako ulikwisha.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Muda wake ulikwisha, namwongeza dakika moja ya Kiti, hitimisha hoja yako.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Bila taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Margaret Sitta, nimekuongeza dakika moja, muda wako ulikwisha ili uhitimisha hoja yako. Kwa hiyo sitegemei taarifa kwenye kuhitimisha hoja yako.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi yao nzuri sana, wanasema hivi; (3) Tafiti kama hizi ziendeleo kufanyika ili kuweza kumshauri kikamilifu Waziri kuhusu masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya Walimu, kwa sababu mpaka sasa *TSC* bado kazi zingine hazifanywi vizuri ili kuwahudumia Walimu kutokana na wingi wao waweze kufanya kazi vizuri, walipwe haki zao kwa wakati ili watumikie vizuri kwa sababu elimu ndiyo namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini naamini Mheshimiwa Waziri hii kazi atafanya tena. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nilimwita Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, wakati huo huo Mheshimiwa Joseph Kamonga, Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa John Daniel Pallangyo wajandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nianze kumshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii, lakini pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kupanga hii timu ya TAMISEMI ambayo inaanza na namba moja ile inayochezwa na Mheshimiwa Bashungwa; namba mbili anacheza Silinde;

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anafuata huyo anayeitwa Dugange; anafuata huyo anayeitwa Shemdoe; anafuata huyo anayeitwa Seif kwa *TARURA*. Nimpongeze tu Mheshimiwa Rais kwa kupanga hii timu. Sasa baada ya hii timu kupangwa inafanya vizuri, kwanza ni wanyenyekevu sana kwenye Wizara hii, ukipeleka matatizo ya wananchi wanasikiliza na wanafanya hii kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe leo kupitia hotuba hii wajinyenyekeze zaidi katika kusikiliza, lakini muwe wakali kwa watendaji hasa kwenye maeneo yetu ya kazi ili nchi iende vizuri. Hizi pongezi nataka niziweke vizuri kabisa ili waelewe na kwa kweli wanafanya kazi kubwa na kutokana na fedha ambazo zimekuja katika Majimbo yetu hasa Mbulu Vijijini nishukuru kwa ajili ya hilo. Niliomba fedha za kumalizia hospitali ya halmashauri, wamepelekea juzi na imeingia, nawashukuru kwa hilo. Biblia inasema; moyo usioshukuru ukarudisha mema mengi, nawashukuru kwa niaba ya wananchi wa Mbulu Vijijini kwa haya waliyotutendea sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TARURA*, nimeshukuru wameongeza fedha, ila kuna ombi ambalo tumeleta maalum Mbulu Vijijini, liko Daraja la Hudaya ambalo linaunganisha kata nne Kata ya Masieda na Kata ya Endagichani na kwa upande wa Mji wa Mbulu, lakini sasa shida iliyoko pale daraja lile likijaa wanafunzi hawaendi kabisa shule na nimeleta picha nimeleta video kwa ajili hiyo tu, niwaombe sana muone kama kuna namna ya *special* (maalum) watenge fedha kwa ajili ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa daraja lile lisipojengwa wanafunzi hawawezi kwenda shule, wametupa milioni 600 ya kujenga shule ya sekondari kwenye Kata ya Endagichan. Vifaa haviwezi kwenda kwa sababu ya mvua daraja lile halipitiki. Naamini kutokana na usikivu na unyenyekevu wa ndugu hawa ambao wameteuliwa na Mheshimiwa Rais watafanya haya ninayoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi niende kwenye suala la afya. Tuna kituo ambacho kimejengwa na wananchi

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kituo cha Maretab, naomba sasa waone namna ya kuwasaidia wananchi wale kwa kuwapelekea fedha. Pia Kituo cha Afya cha Masieda wananchi wameshajenga, kule kwetu tunajichangisha wenyewe kwa kujenga hivi vituo vya afya. Basi waone namna gani ya kuendeleza mchango huu wa wananchi kwa kuwapelekea fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili la Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji, Wenyeviti wa Vitongoji. Kama unavyojua Mwenyekiti wa Vitongoji kesi ya kwanza ya ndoa kabla ya kukufikia wewe Mbunge inafika kwake, wanafanya kazi nzuri. Naomba basi Wizara ione namna gani ya kufanya, hata namna ya kuona tu, najua hali ya bajeti ni tata kidogo, lakini wawawekee fedha kidogo ku-*appreciate* utendaji wao wa kazi ili angalau Mwenyekiti wa Kitongoji aone kwamba alaa! Nimetambuliwa na Serikali na naamini kwa mama Samia Suluhu Hassan watatekeleza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mwenyekiti wa Kijiji, anafanya kazi Januari to Desemba, anatoka tupu, niombe hili kama Wabunge tumelisemea na naomba tuendeleo na TAMISEMI walione hili, wawatengee kidogo, lakini pia Madiwani posho zao zimeonekana posho tu, mshahara ni haki ya mtumishi yeyote, wanapokwenda kwenye halmashauri unakuta mtumishi ana fedha za mshahara wa kwake, lakini Diwani ana posho tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la msingi sana nimeshaongea na Waziri na naomba niliseme hapa, Madiwani wanalipwa *sitting* haina shida hiyo iko kwa mujibu wa sheria, lakini posho zina tofauti diwani wa *angle* nyingine analipwa Sh.100,000, mwingine analipwa Sh.40,000, mwingine analipwa Sh.30,000, kwa nini hizi hela zisiwekwe kwa uwiano wa nchi nzima kila Diwani awe wa Temeke, Manyara au Bukoba walipwe sawasawa kama watumishi wengine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe TAMISEMI wajipange waweke *flat rate* ili Diwani ajulikane huyu Diwani siyo mwingine anaonekana Diwani maalum, mwingine

*special*, hata wao wameanza kuchanganyana kule, mwingine anaonekana yuko maalum sana kwa sababu anatoka mbali, mwingine anaonekana yuko namna Fulani, kwa hiyo tuunde utaratibu, waweke kwenye kanuni, wazilete hapa tuone namna ya kufanya, wawe kwenye *level*/moja tu ili kila mtu ajue huyu ni Diwani ana stahili hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine najua tunakwenda kuajiri, naomba ajira hizi zinapotoka zitoke kwa uwiano waone mikoa yetu ambayo imesahaulika kule watupelekee hizi ajira na wakati wanazigawa ajira hizi Walimu wa sayansi ndugu yangu Mheshimiwa Bashungwa, kule kwetu hali ni mbaya, ziko sekondari ambazo hakuna kabisa Walimu wa sayansi, nikisema sayansi nafikiri Waziri ananielewa. Tuna upungufu wa Walimu 900 kwenye Jimbo zima, lakini tuna Walimu 37 tu wa sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria kwenye Jimbo hilo la Mbulu Vijijini, kama kuna upungufu wa namna hiyo, ni hatari sana. Kwa hiyo ufaulu wetu unategemea nini? Hautegemei moja kwa moja Walimu, ile 25% inayosemwa kitaaluma tunaikosa. Kwa hiyo niombe ndugu yangu Mheshimiwa Waziri aliangalie eneo hilo na atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi ya viongozi ambayo imeahidiwa katika wakati mzuri kabisa wa Mheshimiwa marehemu John Joseph Pombe Magufuli, kilomita tano za lami katika Mji wa Hydrom, tunashukuru zimejengwa 1.8, lakini vizuri sasa basi ahadi za viongozi zikapewa kipaumbele ili zitimizwe na hii itasaidia sana kuonekana kuwa, viongozi wetu wanavyoahidi huwa inatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi, niombe pia yapo maeneo muhimu ambayo tunapaswa kuyaona vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Najua muda umekwisha, ahsante sana. Nitapeleka mchango wangu kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Flatei Massay. Nilimwita Mheshimiwa Joseph Kamonga, wakati huo huo Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni na Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo wajandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ludewa walinizuia kabisa leo kumpongeza Mheshimiwa Bashungwa kwa sababu wana changamoto hasa wale wananchi wa Mwambao, lakini kwa namna Mheshimiwa Bashungwa alivyo muungwana, ukimpigia simu anapokea na juzi nimewasilisha changamoto zangu mbalimbali za Jimboni ikiwemo kile kituo cha afya cha Mundindi wamekamilisha ujenzi, lakini wanakosa vifaa tiba ili waweze kuanza kutao huduma. Nilimpigia Mheshimiwa Waziri usiku alipokea simu na alinisikiliza vizuri. Kwa hiyo, kwa namna hiyo na kwa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyo mnyenyekevu na Manaibu wake, nitakuwa sio muugwana nisipompongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kutoa pongezi kwa Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Jimboni Ludewa kuna changamoto ambazo ningependa Mheshimiwa Waziri azitilie maanani. Kuna Tarafa ya Mwambao ambayo ipo kando kando ya Ziwa Nyasa. Tarafa hii kwa miaka mingi walikuwa wanategemea usafiri wa meli, bahati mbaya ile meli imekuwa na changamoto na muda mwingi haifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa hii ina Kata nne ambazo hazijaunganishwa kabisa kwa barabara. Kuna Kata ya Lifuma haifikiki kwa gari na wananchi hawajawahi kuwa na gari maisha yao yote, kuna Kata na Makonde haifikiki kwa

gari na wananchi hawajawahi kuona gari maisha yao yote, kuna Kata ya Kilondo na Kata ya Lumbila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo jitihada za Serikali kupitia *TARURA*, nilikwenda kwa *CEO* wa *TARURA* nikiwa na Madiwani wangu, waliweza kuwasikiliza vizuri, lakini changamoto kubwa, bajeti ambayo wanapewa kwa ajili ya hizi barabara ni finyu sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iweze kuwaongezea fedha hawa watu wa *TARURA* na ikiwezekana wahandisi kutoka *TARURA* Makao Makuu waende wakasaidiane na wale walioko Mkoani na Jimboni, wafanye tathmini maana wananchi wa huku wanaona kama Serikali imewasahau na wanaona mimi Mbunge wao kama siwasemei. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba ulipe uzito. Kimsingi kuna barabara nyingine kupitia *TARURA* nazo wamekuwa wakifanya kazi nzuri, lakini changamoto ni bajeti wanayopewa, haitoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi nilikwenda kuwapa pole wananchi wa Kiogo; kutoka pale Masasi kwenda Kiogo, barabara ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, siku ile nilimwona Mheshimiwa Bashe wakati anazungumzia mapinduzi ya Kilimo; Kilimo Biashara, alikupa nafasi ulizungumza pale. Kwa hiyo, mimi ni miongoni mwa Wabunge ambao tunaamini maendeleo na mapinduzi ya kilimo yanaenda sambamba na kuboreshwa kwa barabara za vijijini. Kwa sababu kama Wizara ya Kilimo watakuwa wamepeva bajeti kubwa, halafu *TAMISEMI* kupitia *TARURA* wananchi wanalima mazao halafu hawawezi kuyatoa shambani kuyafikisha kwa walaji, kwa kweli hata ufanisi wa kilimo biashara utakuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana barabara za vijijini; na ninamshukuru pia Mheshimiwa Waziri siku ile aliona *clip* ya gari iliyokuwa inapata shida kwenye Kijiji cha Ilininda, wananchi wanahangaika sana kwenye matope. Mheshimiwa Waziri alinitafuta na kuniambia kwamba anataka kwenda kule. Nakushukuru alitoa maelekezo kupitia *TARURA*, wameanza kujenga zile *concrete strips*. Kwa hiyo, ninaamini ule ni ufumbuzi wa kudumu. Kwa

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hiyo, nakuomba ahadi yake ya kutembelea Jimbo la Ludewa ibakie pale pale kwa sababu kumekuwa kuna malalamiko ya wananchi kwamba Waheshimiwa Mawaziri wengi wanarudia pale Njombe, hawaendi Ludewa kule kusikiliza changamoto na nimaamini sasa tutaendelea kupata Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine ambayo inalikabili Jimbo la Ludewa ni uhaba wa watumishi. Unakuta shule ya msingi ina walimu watatu; mmoja yupo masomoni, mwingine yupo *maternity leave*, shule imebaki na mwalimu mmoja, labda na walimu wawili au watatu wa kujitolea. Hawa walimu wa kujitolea nafasi zinavyotangazwa Serikalini nao hawapewi kipaumbele cha kupata ajira. Changamoto ya kule walimu wengi wakipelekwa wanahama. Kwa hiyo, naomba wale wanaojitolea kule Mheshimiwa Waziri nipo tayari kukuletea orodha ili wapewe kipaumbele cha kupata ajira kwenye sekta ya elimu na afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ludewa tuna upungufu wa watumishi 986, wengi ni kwenye sekta ya elimu na afya. Kwa hiyo, naomba kwenye ajira hizi Ludewa tuweze kupata kipaumbele ili tuwaondolee wazazi usumbufu wa kuchangishwa fedha ili kulipa walimu wanaojitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Ludewa wamejitolea sana kujenga vituo vya afya kata saba, lakini havijakamilika muda mrefu. Kwa hiyo, hili nalo naomba Mheshimiwa Waziri alichukue kwa sababu tulishazungumza ili wananchi jasho lao lisipotee bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya haya machache. naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, wakati huo wanajiandaa Mheshimiwa Dkt. John Daniel Pallangyo, Mheshimiwa Jonas



Van Zeeland, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila pamoja na Mheshimiwa Tarimo ndio atahitimisha.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya njema. Kabla sijaenda mbali sana, naomba nitoe haki kwa viongozi wa Wizara ya TAMISEMI, nikimaanisha Waziri, Mheshimiwa Bashungwa, Manaibu wake, Mheshimiwa Dugange na Mheshimiwa Silinde. Kwa nini nimesema nitoe shukrani na pongezi kwa hawa watu?

Kwa uzoefu wangu nadhani na Wabunge wengine, hakuna Mawaziri rahisi kuwapata kama hawa jamaa. Ukiwa na shida yako ni rahisi sana kuwapata hawa Waheshimiwa (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwapongeze sana. Wamekuwa ni watu, wasikivu na ni wepesi wa kujibu shida za Wabunge. Ninapoleta shida TAMISEMI nakuwa na amani kwa sababu ya watu wanaosimamia Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ni wakati muafaka kwa watu wengine kujifunza pia. Kuna Waziri mmoja mpaka nilimwandikia *message* nikamwambia Mheshimiwa Waziri nikitaka kukupata ninafanyaje? Kwa sababu huwezi kumpata. Ndugu zangu, zichonganishi lakini ninasema ukweli, mmekuwa watu wema sana, mnatusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze kwenye kuwashauri hawa ndugu zangu wema. Wizara ya TAMISEMI ni Wizara kubwa sana, inasimamia vitu vingi sana. Mheshimiwa Rais amewapa kazi kubwa sana ya kusukuma maendeleo. Mheshimiwa Rais anatafuta fedha, analeta kwenye maendeleo. Sisi sote ni mashahidi na nchi ni shahidi, kama kuna wakati miradi ya maendeleo imepelekwa vijijini kwa watu, ni wakati huu wa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. Sasa ninyi TAMISEMI ndiyo mna jukumu la kusimamia hizi fedha Mheshimiwa Rais anazotupelekea kwenye maendeleo. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasimamizi wa hizi fedha, leo ninarudia, kwenye bajeti iliyopita nilisema, nashukuru Serikali sikivu ilinisikia, ikahamisha posho za Madiwani katoka kulipwa kwenye Halmashauri zikaanza kulipwa na Serikali Kuu; kwenye Bajeti iliyopita tulisema kuhusu Madiwani kutokulipiwa Bima zao za Afya, tunashukuru Serikali sikivu ya CCM imeamua sasa kuchangia Bima za Afya za Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, kada ya Udiwani ni muhimu sana kwako. Naweza kukwambia, inawezekana hawa ndio walinzi wa nyumba yako. Fedha zote zinazopelekwa Halmashauri, wanaozilinda ni hao Madiwani lakini walinzi wako hawana vifaa vya kulindia fedha. Unapeleka mabilioni ya fedha kwenye Halmashauri, lakini unawalipa watu shilingi 300,000 walinde mabilioni, siyo sawa na tunajidanganya. Fedha zetu zitaendelea kuliwa na kuibiwa kwenye Halmashauri mpaka siku tutakapotambua umuhimu wa Madiwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nataka nichangie hili kwa uchungu kwa sababu wakati nipo Diwani, mfano nilipokuwa nikienda kwenye kikao, Halmashauri zetu hazifanani. Halmashauri ya Dar es Salaam na Ilala na Kwimba ni tofauti, inabidi mimi niende nikalale Ngudu kutoka Lyoma.

Kwa hiyo, siku ninapoenda kwenye kikao nilikuwa nalipwa *night*, nikiamka naenda kwenye kikao, kesho yake naenda kwenye kikao cha Kata, kesho yake kikao cha *Full Council*, siku inayofuata nitatoka jioni, nitalala, kesho yake naondoka. Nilikuwa nalipwa siku nne. Nashangaa sijui huu utaratibu umetoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni utaratibu umebadilishwa, Diwani anaambiwa yule anayelala, alale siku mbili; haya makabrasha wanayapitia saa ngapi? Ndugu zangu kama mnahudhuria vikao vya Madiwani yanakuja mabuku makubwa hivi, yanahitaji muda wa kuyapitia. Sasa wanayapitia saa ngapi? Cha ajabu siku za karibuni, na nilikwenda kumwona Mheshimiwa Waziri pale nikamwambia; Madiwani wameanza kulipwa, lakini wengi hawalipwi fedha

za kulala, wanaambiwa aende arudi. Huu uzoefu ni wa wapi?  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Wilaya ya Kwimba kuna Kata ipo kilometa kama sita kutoka Halmashauri, inaitwa Kata ya Mwang'halanga, kuna mto pale wa Mahiga, ukijaa maji, Diwani kama kalala kwake, hahudhuri vikao. Kwenye Jimbo la Sumve, Kata ya Wala tunamshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu amejenga daraja baada ya kumeomba. Diwani akilala kwake, ni kilometa kumi tu, hawezi kuhudhuria kikao. Nyambiti kuna Mto Solwe haupitiki mvua ikinyesha, ndio maana Madiwani walikuwa wanatakiwa wakakae kwenye Halmashauri wamalize vikao halafu waondoke.? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii akili ya kuanza kuwaambia Madiwani wahudhuri vikao warudi nyumbani, mmeitoa wapi? *Otherwise* mmeamua Halmashauri iwe shamba la bibi. Tutaibiwa kweli kweli, nakuhakikishia Mheshimiwa Waziri. Utakuja na bajeti hapa, tutakuwa tumepigwa, mtafukuza watu, mtaasimamisha watu, lakini kama hamwelewi kuwawezesha Madiwani posho yao ya mwezi, unamlipa mtu shilingi 300,000/= unasema asimamie mabilioni; Mheshimiwa Waziri naomba sana, wewe ni msikivu, ni wakati sasa umefika Serikali kuelewa umuhimu wa Madiwani. Kama hamtaki kuelewa, mtaendelea kuibiwa, tutaendelea kukamata watu, kufukuza watu na tutakuwa hatujaisaidia nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa msingi kabisa ulikuwa ni huu. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kasalali Mageni Diwani wa zamani. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo aweze kuchangia. (*Makofi*)

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kutoa mchango wangu kwa hoja hii ambayo ipo mezani. Nitangulie kwa kuungana na wenzangu waliozungumza

hapa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai, afya na nguvu hata tukaweza kukutana hapa leo. Napenda pia kuendelea kuwashukuru wananchi wangu kule Arumeru Mashariki kuendelea kuniamini na niwahakikishie kwamba kazi inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Bashungwa na Manaibu wake wawili Mheshimiwa Dugange na Mheshimiwa Silinde kwa kazi nzuri sana ambayo wanafanya. Ni vijana wema, wasikivu na ndiyoy maana wameimudu hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nisipowashukuru na kuwapongeza watendaji wakuu kuanzia Katibu Mkuu na watendaji wengine, nitakuwa sijatenda haki. Nawapongeza watumishi wote kwenye hii Wizara. Ukisoma vizuri hii hotuba ya Waziri wa TAMISEMI, utakubaliana nami kwamba ile *reflection* ya siku 365 za Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan akiwa ofisini. Ni kipindi hiki ambacho tumeona utekelezaji wa llani chini ya uongozi mahiri wa Mama ukifanyika kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kipindi hiki, kila Jimbo lilipata shilingi bilioni moja na nusu kwa ajili ya barabara kwa kupitia *TARURA*. Nasi tulipata hivyo hivyo, tunavyozungumza sasa hivi barabara ya King'ori ambayo nilikuwa naizungumzia hapa mara kwa mara, imefunguka, ni barabara. Nashukuru sana na ninaipongeza Wizara kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ahadi za viongozi wakuu wa nchi ambazo zilitolewa, hazijatekelezwa. Mwaka 2012 Januari wakati wa maziko ya aliyekuwa Mbunge wetu, Marehemu Jeremiah Sumari, tulipewa ahadi na aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, kwamba barabara inayoanzia Sangisi kwenda Keri hadi Ndoombwe ingejengwa kwa kiwango la lami. Leo hii ni miaka 10 na ushee, bado ile ahadi hajiatekelezwa. Naomba wakati wa kuhitimisha Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusu barabara hii.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kwenye suala la afya bado kuna ahadi nyingine. Mwaka 2020 Rais wa Awamu ya Tano, Marehemu Dkt. John Pombe Magufuli alitoa ahadi mbele ya wananchi wengi sana pale Usa River kwamba barabara ya King'ori kuanzia maeneo ya Kibaoni hadi Ngare Nanyuki kwa kupitia King'ori Madukani - Maruvango - Leguruki ingejegwa kwa kiwango cha lami. Ninaamini Mheshimiwa Waziri katika kuhitimisha pia atatoa tamko kuhusu ahadi hiyo ya Rais, kwa sababu pia hata kwenye maelezo ya hotuba yake amesema haya mambo ni ilani na ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye afya niseme pia kwamba, ni kwa kipindi hiki cha siku 365 ambapo tumeshuhudia vituo vya afya vinajengwa vingi, nchi nzima. Kule Meru pia nasi tumepata Kituo cha Afya cha King'ori, lakini niseme pia kwamba tuna matatizo ya vituo vya afya. Vituo vingi vya afya kule zilikuwa zahanati, ni maboma yaliyochoka, Mheshimiwa Waziri ukumbuke, ukipata nafasi twende tukatembee uone hali ilivyo kwenye vituo vya afya. Tunashukuru sana tulipata Kituo cha Afya na tulipata pia fedha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kujenga *Emergence Unit* pale kwenye Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika kipindi cha siku 365 tuliweza kupata madarasa 70 ndani wa wiki nane. Ndani ya miezi miwili tulipata madarasa 70 kule Meru, kwa kweli tunapongeza Serikali kwa hilo. Tunashukuru sana, imetupunguzia mzigo, wananchi hawauzi tena kuku wakikimbizana kujenga maboma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba kuna shule nyingi kule Jimboni ambazo zinahitaji ukarabati. Naomba Wizara ilitazame hilo ili ije na *operation* ya kukarabati zile shule, kwa sababu miundombinu imekaa vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu pia kuwatetea Madiwani. Kwakweli Madiwani wanafanya kazi kubwa sana kwenye Majimbo yetu, lakini ukiangalia stahiki zao hazitoshelezi. Wanapata *sitting* lakini wanahangaika huku

na kule kusimamia miradi ambayo inatekelezwa kwa fedha za ndani, lakini pia na fedha ambazo zinatoka Serikali Kuu. Wakati umefika sasa tuangalie maslahi yao. Wabunge wamesema nadhani Mheshimiwa Waziri utaliangalia hilo ili Madiwani wetu wapate ahueni kwenye bajeti inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nitoe mchango wangu huo kwa ufupi sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. John Pallangyo. Sasa namwita Mheshimiwa Jonas Van Zeeland wakati huo Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila pamoja na Mheshimiwa Priscus Tarimo wanajiandaa.

**MHE. JONAS V. ZEELAND:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu jioni ya leo. Nianze kwanza kumshukuru Mwenyekiti Mungu kwa kunjalia, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na na Manaibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Manaibu wake kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya katika Wizara hii ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi kifupi, sisi Mvomero, tumepokea fedha nyingi sana za miradi na kipekee naomba nichukue nafasi hii nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, mwaka jana nilisema, niliomba fedha mbalimbali kwa ajili ya miradi na tumepata fedha nyingi na sasa hivi ninavyozungumza hapa miradi mingine inaendelea na utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Bashungwa hivi karibuni alifanya ziara Mvomero na alijionea mwenyewe miradi inavyoendelea. Pia alipata nafasi ya kwenda kuangalia sekondari ya kumbukumbu ya Sokoine, ambayo Serikali imetupatia fedha nyingi sana na hivi juzi juzi wametupa milioni 700 kwa ajili ya kuiendeleza ile sekondari ya Sokoine. Kwa bahati mbaya kulikuwa kuna shida kidogo kwenye milioni 700 na nimpongeze sana

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Waziri alifika akatoa maelekezo, kuna ubadhirifu wa zaidi ya milioni 200 na kitu, akatoa maelekezo watumishi zaidi ya tisa wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze tena kwa mara nyingine Mheshimiwa Waziri, lakini mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa Bungeni, hakuna mtumishi hata mmoja aliyechukuliwa hatua Mheshimiwa Waziri. Kama watumishi hawa wataendelea kubaki pale bila kuchukuliwa hatua zozote hata za kinidhamu, Mheshimiwa Waziri ataendelea kutupa fedha lakini kuna watu wamejiandaa kuendelea kuzitafuna hizi fedha. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri maelekezo yake yazingatiwe na wale watumishi wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sisi tumepokea fedha bilioni 2.2 kwa ajili ya madarasa 107 yale ya COVID, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. Hapa nimpongeze pia Mkuu wangu wa Wilaya, Mwenyekiti wa Halmashauri na Madiwani kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya ya kutekeleza kujenga vyumba hivi 107 katika kipindi cha miezi miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Mvomero tuna maboma mengi sana ya madarasa, tunaomba sana safari hii watutengee fedha katika bajeti kwa ajili ya kumalizia haya maboma, hii ni miradi viporo vya muda mrefu sana. Tunawakatisha tamaa wananchi, wanaanzisha wao wenyewe, lakini mwisho wa siku Serikali inachukua muda mrefu sana kuleta fedha za umaliziaji.

Sisi moja kazi ya mwanasiasa ni kuhamasisha, nikiwa jimboni kule nahamasisha tuanzishe ujenzi wa zahanati, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa nyumba za Walimu, lakini tunapofika kwenye hatua ya *lenter*, Serikali inachukua muda mrefu sana kuleta fedha za umaliziaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao ujenzi wa zahanati iko pale Dakawa, ina zaidi ya miaka kumi ile haijamaliziwa na tumeomba sana, kila bajeti tunaomba fedha kwa ajili ya kuimalizia. Tuna imani sasa hivi watatuletea fedha ili tuweze

kumaliza. Pia nimpongeze Waziri, wametupa milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mziha na ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda niende moja kwa moja kwenye suala la Madiwani. Mwaka jana nilisimama nikasema suala la Madiwani na wenzangu walizungumza sana masuala ya Madiwani lakini hata bajeti unaona kila Mbunge karibuni anachangia suala la Madiwani. Nimwombe sana Waziri, mwaka jana wamewapa nafuu halmashauri kwa maana Serikali moja kwa moja inakwenda kulipa zile posho za mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Waziri kumlipa moja kwa moja Mkurugenzi ili awalipe Madiwani wamewasaidia watu wa Benki, kwa sababu zile 350,000 asilimia zaidi ya 90 Madiwani wamekopa. Kwa hiyo, zile fedha zikienda kwenye halmashauri zinakwenda benki, Diwani kama Diwani pengine anabakia na 50,000. Kwa hiyo, nimwombe pamoja na jambo nzuri wallilolifanya, safari hii Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kuongeza bajeti katika suala zima la Madiwani, angalau hata wakipata kwa kuanza shilingi 500,000, sasa hivi wanalipwa shilingi 350,000 ongeza shilingi 150,000, mpaka 2025 huko angalau watafikia hata kwenye shilingi 700,000 au shilingi 800,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimwombe Mheshimiwa Waziri na hawa wenzetu wapewe kibali cha msamaha wa kodi wawe na *exemption* upande wa magari. Waheshimiwa Madiwani, wanafanya kazi kubwa sana, wana uwezo wa kununua magari sio wote lakini wakipata msamaha wa kodi watakuwa na uwezo wa kununua magari na wenyewe watafanya kazi kwa urahisi, wataweza kuzunguka kwenye kata zao. Niombe sana suala hili linawezekana. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri angalau wapate msamaha wa kodi ili na wenyewe waweze kununua vyombo vya moto, waweze kufanya kazi usiku na mchana, za kusimamia fedha ambazo unazipeleka kwenye majimbo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa *TBA*, kama kuna bomu lingine lipo nchi hii ni hawa watu wa *TBA*, miradi



## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yote ambayo inasimamiwa na *TBA*, miradi hii ina mambo matatu, moja lazima kutakuwa na ongezeko la mradi, thamani ya mradi ongezeko ni kubwa sana, kama mradi wa bilioni moja, hawa *TBA* wakisimamia watakwenda mpaka bilioni mbili na kitu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, muda, miradi hii haitaisha kwa wakati, kama *TBA* wanasimamia. La tatu, *value for money* katika miradi hii hakuna. Mheshimiwa Waziri anafanya kazi nzuri, miradi mingi siyo yote ambayo inasimamiwa na *TBA* kuna shida afuatilie, atupie jicho la tatu huo upande wa *TBA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Jonas Van Zeeland. Namwita Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela, wakati huo Mheshimiwa Priscus Tarimo ajiandae.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niendeleo kuishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri sana zinazofanyika chini ya jemadari wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja na wenzetu wa *TARURA*, kuna vitu ambavyo vinashangaza sana. *TARURA* na *TANROADS* wanaishi kama watoto ambao hawajatoka baba mmoja, mama mmoja, kuna tatizo kubwa sana. Nimeshuhudia kwenye wilaya kwenye Jimbo la Kyela, wakati tuna matatizo ya madaraja, wananchi wanatembea kilomita 30 kwenda kulikuta daraja, barabara mpya ilipojengwa, madaraja mawili makubwa yamepotea wakati kuna uhitaji wa zaidi ya madaraja nane kwenye Wilaya ya Kyela. Sasa unajuliza hivi *TARURA* na *TANROADS* ni watoto wa nani? Je, wanafanya kazi wanafanya kazi ambazo zinaendaje? Mwisho wa siku, mpaka naamini kwamba inawezekana kanuni iliyounda *TARURA* kuna sehemu haikuwa sawa. (*Makofi*)

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani leo, *TANROADS*, wako hapo hapo lakini wanabeba daraja kwa sababu tu eti hiyo barabara ambayo daraja hilo lingefaa wanaoshughulikia ni *TARURA*. Sasa ningepomba kuwe na *coordination* nzuri kati ya *TANROADS* na *TARURA*, mambo yote yataenda sawa. Kwa sababu mama ameamua kupeleka na kufungua pochi yake kwa ajili ya wananchi walioko huko vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote, kipindi kilichopita nilisema hapa katika wilaya zinazopata mvua kwa wingi, lakini wilaya ambayo iko chini mno, ambayo inapokea mvua zote na maji ya mvua zote kutoka milimani ni Kyela, maana yake nini? Maana yake ni kwamba, kama Kyela ipo chini madhara makubwa yapo kwenye miundombinu iliyoko kule. Sasa matokeo yake Kyela huu ni mwaka wa sita haijawahi kupata fedha za *development* kwenye miundombinu. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba kila barabara iliyopo kule imegeuka kuwa ni sehemu ya kupitisha maji, imegeuka kuwa mto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe ni shahidi, unapita mara nyingi, mafuriko yakitokea unatuma kule vijana wako wa *Red Cross*, wewe unajua. Unapoenda kule Bwato, hakuna barabara, kuna daraja limejengwa pale Ngorwa, limeishia ukingoni, barabara hakuna na daraja lingine la kumalizia hakuna. Sasa ningepomba niseme hivi, nataka kujua sababu ni kwa nini Kyela imenyimwa siku zote hizo fedha za *development*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwahidi Mheshimiwa Waziri, kama hajawahi kushikiwa shilingi yake, basi kesho nisipopata majibu sahihi, nitashika shilingi kwenye mshahara wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye fedha za UVIKO, Wabunge hapa watashangaa kama hawajawahi kushangaa sasa hivi watashangaa. Tulipopata fedha za kujenga madarasa 67 nilitafuta mdau ambaye alikuwa tayari kutoa bilioni 1.1 kuongeza kwenye fedha hizo kumuunga

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mkono Mheshimiwa Mama Suluhu Hassan. Kilichotokea mpaka leo hizo fedha mhisani ameondoka nazo na hazijafanya kazi kwa sababu ya *coordination*, watu kutafuta umwamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme, tumefika mahali ambapo mtu anakuwa anaamua badala ya wananchi kuamua nini wanakitaka. Nataka kusema hata kama ni fedha ambayo haifai, lakini kwa vile nilikuwa najenga madarasa, mhisani alisema mnajenga 67, hizo fedha leteni tuchanganye, nitajenga madarasa 154, mwisho wa siku tumeishia 67 tu, sasa hili linasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili lazima nimshukuru sana ndugu yangu Naibu Waziri wa TAMISEMI alishughulisha sana walihangaika, lakini yule mhisani yupo anaendelea kusaidia sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu kimetokea hapa, katika ujenzi huu nataka nijifunze kutoka TAMISEMI, nani alisema *cement* inayotakiwa kutumika ni ile ya 42.5? Kila sehemu nani amewaambia? Nimejaribu kupekua kila *literature* kujua kuna tofauti gani, kwa nini utumie hii 42 badala ya 32? Kila sehemu unaambiwa ya 42 inatumika kwenye *structural elements* kama *beam*, lakini hili limetumika kama kivuli cha kuiba fedha. Fedha mama Samia alizitoa ili zikasaidie na wananchi, lakini nawaambia hapa ndugu zangu *reflection* ya fedha zile kwa wananchi haziko, walikuwa wanachukua wanapeleka kwenye makampuni, badala ya kununua kwa wazubuni walioko hapa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mlaghila, muda wako umekwisha, tunakushukuru sana kwa mchango wako.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, utakuwa mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa mwisho na nitajitahidi niende kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wizara kwa juhudi zao hasa Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri wake kwa kweli wako *field* muda wote na nimekuwa nikiwafikia mara kwa mara. Niwashukuru pia watendaji, ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu na Dkt. Ntuli ambaye anashughulikia masuala ya afya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee yale ambayo tumeshafanya hasa kwenye barabara ambapo sisi tuna mradi wa *TACTIC* kwenye Jimbo la Moshi Mjini ambayo ilichelewa kwa mwaka mmoja lakini tunategemea watalisukuma ili mwaka huu basi liweze kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye hospitali ya wilaya kuendana na jiografia yetu tulishapewa milioni 500, lakini kutokana na ufinyu wa maeneo sisi tunajenga gorofa, tumeleta ramani kwao wameshapitisha, tuliomba watuongezee ili fedha ya kuanza ili ile fedha ya kwanza kitu kitachowekwa pale kiweze kuonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye kituo cha afya wametupa milioni 250, Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde alikuja aliona namna tunavyokwenda kwa kasi, tunaomba basi ile 250 ya kumalizia nayo iweze kufika ili tuweze kukamilisha kwa haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika kwenye shule, ambayo tunajenga kwenye Kata ya Msalanga, ile milioni 470 tumeifanyia kazi vizuri, tunaomba sana sisi tumejipanga kwa kutumia nguvu za wananchi, tuanze kuongeza mabweni. Sasa tunaomba juhudi hizo za wananchi zikianza, kwa sababu kati ile iko pembezoni, basi Serikali iangalie namna ya kutuongezua, ili basi tuweze kuwa na mabweni.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningenda kwenye suala la Wamachinga, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hatua aliyochukua kwa ile *incident* ya Mwanza. Nimwambie maeneo yote yenye Wamachinga kumekuwa na tabia hiyo ya kuwanyang'anya watu vitu na sidhani kama ni njia nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, kule Moshi, kuna watu walikuwa wanauza mabegi, walinyang'anywa na wanapofanya ile *operation* wananchukua maeneo yote. Sasa inapokuja kwenda kuwarudisha, vile vitu wanavyovichukua hawaandiki vitu gani ni vya nani? Tunawasababishia wale Wamachinga umaskini na sioni sababu ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu au mawazo yangu, ni vizuri wawatumie wenyeviti wa Serikali za Mtaa kwenye hizo *operation*, wanawafahamu wale watu na vitu vyao ili vinapochukuliwa, baadaye itakapobidi kuwarudishia basi warudishiwe vitu vyao, lakini kuvichukua na kupotea, ni sawasawa kabisa na kusema Serikali inawanyang'anya wananchi mali zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwenye kuwapanga, naamini tukiweza kuwatumia Wenyeviti wa Serikali za Mtaa tunaweza kuwapanga vizuri badala ya kuwa na zile *operation* za kuwanyemelea kuvunja na kuchukua vitu na kuvipoteza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye masoko mbalimbali, tumekuwa na *incident* za kuwaka moto masoko. Ninawazo ambalo nadhani linaweza likasaidia, kwa nini tusibadilishe mtindo wa ujengaji kwenye masoko haya ambayo siyo rasmi, badala ya kutumia mbao tutumie chuma ili kupunguza haya matatizo yanayotokana na moto ambao unajitokeza mara kwa mara. Kule Moshi umetokea lakini bado watu wanarudia kujenga kwa kutumia mbao. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba hilo mliangalie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna mradi wa kimkakati wa stendi pale Moshi, mradi ule umesimama kwa muda

mrefu, ningepomba Mheshimiwa Waziri anapohitimisha aangalie namna ya kusaidia miradi hii ya kimkakati ambayo ilikuwa kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, stendi yetu ya Ngaka – Mfumuni imesimama na hakuna kinachoendelea.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtemvu taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issa Mtemvu, taarifa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mzungumzaji wakati anamalizia kuzungumzia juu ya masoko ya kimkakati, pamoja na stendi. Tunalo soko ambalo ni sambamba na stendi pale Mbezi Louis ya Magufuli, mpaka sasa tunatambua stendi ile inaingiza takribani bilioni 50 za Watanzania za ndani lakini bado haijakamilika, kwa sababu ya VAT na kadhalika baada ya kutokea kwenye jiji kuja ndani ya Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo. Tunawaomba sana ili ile fedha za Watanzania zikatumike, zikawe na tija, basi ni vizuri mhakikishe stendi ile inakamilika ili iweze kuleta tija ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni taarifa siyo?

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea tu kwa sababu ni ndugu yangu huyu. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningepomba niende pia kwenye suala kupanga miji, hili linahusisha Wizara mbili, mfano wa Moshi, tulishafanya vikao na Wilaya ya Hai, pamoja na Moshi Vijijini kupanua maeneo. Sasa kwa sababu inahusisha TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi, imeendelea kuwa na mkwamo mkubwa na matokeo yake ni nini yale maeneo

ambayo tulikuwa tupanukie yameendelea kujengwa bila mpangilio, kwa sababu kule hakujawa mjini, kwa hiyo, kumekuwa na *slums* zinatokea kule na baadaye tukija kupanua mji, basi tunaenda kurasimisha maeneo ambayo hayatakuwa na miundombinu wowote. Sioni ugumu wa kuongeza yale maeneo ya kiutawala na iwe hivyo kwa miji yote ambayo inakuwa, tuwe tuna *plan ahead*, bada ya kuwa ya *slum* ambazo kila mara tunazirasimisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala ambalo liko TAMISEMI, lakini linahusisha pia ajira, watu wa bodaboda. Bodaboda ni ajira rasmi na kama ni ajira rasmi ni vizuri wale watu waendeshaji ambao sio wamiliki na wale ambao ni wamiliki wanaendesha waweze kuingizwa kwenye mfumo wa *WCF* kwa kuwatumia TAMISEMI, kwa nini nasema hivyo? Hawa watu ndio wanapata ajali sana na wakipata ajali, wamekuwa ni mzigo kwenye matibabu yao, wangeweza kurasimishwa wakawekwa kwenye Mfuko ule wa *WCF*, wanaweza kutibiwa na kupata fidia pale wanapopata ajali badala ya hali ilivyo sasa ambao wanakuwa mzigo kwa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, pamoja na watu wengi kuongelea kuwaongezea posho Madiwani pamoja na Wenyeviti, hili ni la muhimu sana, lakini tuangalie kwa upana. Isipokuwa ningeomba pia suala la ajira hizi mpya tuangalie zile kada za Walimu pamoja na watumishi wa afya, hasa wale ambao tayari wanajitolea kule ili waweze kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa Mkutano wetu wa Saba, Kikao cha Nane, kwa maana ya jioni hii. Msisitizo hoja ya Madiwani imezungumzwa tena, lakini bahati njema sana Mheshimiwa Spika alikwishatolea mwongozo, Kamati ya Bajeti ilichukue jambo hilo ifanye uratibu na kuona namna ya kulifanyia kazi. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa ajili ya hilo. (*Makofi*)

*NAKALA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

Pia kuna hoja imetolewa hapa ambayo Serikali ni vizuri ikaichukua ni ushiriki wa wahisani katika kuchangia maendeleo, ni namna gani sasa wale wahisani ambao kimsingi tunahitaji michango yao wasiwe *discouraged*, tuwasaidie utaratibu ili mchango wao ule uka-*add value* kwenye maendeleo yetu, ni vizuri pia hilo kama Serikali mkalichukua. *(Makofi)*

Limezungumzwa jambo lingine la tatu kwa kirefu sana, kuhusiana na suala la watumishi, kuna baadhi ya mikoa imejenga watumishi wanakwenda kule kama wanapatiwa *check number* kisha wanaondoka. Ni vizuri sasa Wizara mkachakata ushauri wa Wabunge, wengine wamekwenda mbele zaidi kuona kwamba pengine maeneo yale yatazamwe, ninyi kama Wizara kwa utaratibu mnaoona unafaa, mkalichakate na namna ya kuona linaweza kusaidia Watanzania wapate huduma hizo. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo, tumefika mwisho wa kikao chetu cha leo, hivyo naahirisha mpaka kesho saa tatu asubuhi, tarehe 20 Aprili, 2022

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 20 Aprili, 2022, Saa Tatu Asubuhi)*